

**KUCHUNGUZA MTINDO KATIKA NYIMBO ZA TIBA ASILI: MIFANO
KUTOKA NYIMBO ZA WAGANGA WA MKOA WA RUVUMA**

WILLY MIGODELA

**TASINIFU YA ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SHARTI
PEKEE LA KUTUNUKU SHAHADA YA UZAMIVU (Ph.D) YA KISWAHILI
KATIKA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2020

UTHIBITISHO

Sisi, Prof. **Emmanuel Mbogo** na Dkt. **Mohamed Omary Maguo**, tunathibitisha kwamba, tumeisoma tasnifu hii inayohusu: “**Kuchunguza Mtindo katika Nyimbo za Tiba Asili: Mifano Kutoka Nyimbo za Waganga wa Mkoa wa Ruvuma**”, na tunaipendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sharti pekee la kutahiniwa ili kutunukiwa shahada ya Uzamivu (PhD) ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Prof. Emmanuel Mbogo

(Msimamizi)

Tarehe _____

Dkt. Mohamed Omary **Maguo**

(Msimamizi)

Tarehe _____

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili sehemu yoyote ile ya tasinifu hii, kwa njia yoyote kama vile kielektroniki, kurudufu nakala au kurekodi bila ya idhini ya mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TAMKO

Mimi, **Willy Migodela**, ninakiri rasmi kwamba, tasinifu yenye kichwa: **“Kuchunguza Mtindo katika Nyimbo za Tiba Asili: Mifano Kutoka Nyimbo za Waganga wa Mkoa wa Ruvuma”** ni kazi yangu mwenyewe. Haijatolewa na haitatolewa kwa mahitaji ya kutunukiwa shahada ya Uzamivu au shahada nyingine yoyote katika Chuo Kikuu kingine chochote.

Willy Migodela

Tarehe

TABARUKU

Tasinifu hii ninaitabaruku kwa rafiki na mwalimu wangu, nguli wa fasihi na falsafa ya Kiafrika, Profesa Euphrase Kezilahabi. Alinipa hamasa ya kuanza shahada ya Uzamivu, nikaitikia wito na kazi nimeimaliza. Nakuombea kwa Mungu akulaze mahali pema peponi.

SHUKURANI

Kwanza kabisa, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuikamilisha kazi hii. Aidha, ninatoa shukurani za pekee kwa wasimamizi wangu, Prof. Emmanuel Mbogo na Dkt. Mohamed Omary Maguo, kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Hawakusita wala kuchoka, kunishauri na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Mungu Awabariki sana.

Pia, ninamshukuru mke wangu mpendwa, Mwajja Ngenzi na wanangu: Brian Willy Migodela na Barack Willy Migodela, kwa uvumilivu wao katika kipindi chote nilichokuwa masomoni. Kwa kweli, haikuwa rahisi kutimiza wajibu wa kuwa mzazi kwa asilimia zote. Wengine ni Fr. Dkt. Longino Rutagwerela, Dkt. Julius Frank, Dkt. Anold Msigwa, Dkt. Ramadhan Thomas Kadallah, Dkt. Gerephace Mwangosi, Bw. Gelvas Kawonga, Bw. Baraka Makosa, Bw. Lazaro Ngole, Bw. Denis Mpagaze na Bw. Timothy Mapunda. Nashukuru kwa ushirikiano wao walionionesha tangu mwanzo wa utafiti huu hadi kukamilika kwake.

Halikadhalika, ninawashukuru wafanyakazi wote wa TATAKI kwa mchango wao na kwa kunipa faraja wakati wote wa masomo yangu. Kwa hakika, si rahisi kuwakumbuka wote walionisaidia, bali ninawashukuru wote walioshiriki katika kufanikisha utafiti huu.

ORODHA YA VIFUPISHO

CKM	Chuo Kikuu cha Moi
Dkt.	Daktari
DUP	<i>Dar es Salaam University Press</i>
Fr	<i>Father</i>
Ltd.	<i>Limited</i>
PhD	<i>Doctor of Philosophy</i>
Prof	Profesa
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
TUMI	Taasisi ya Ukuzaji Mitaala

IKISIRI

Utafiti huu ulihusu ‘**Kuchunguza Mtindo katika Nyimbo za Tiba Asili: Mifano Kutoka Nyimbo za Waganga wa Mkoa wa Ruvuma**’. Utafiti ulikuwa na malengo mahsusi matatu. Lengo mahsusi la kwanza lilihusu kuainisha nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma. Lengo mahsusi la pili lilihusu kubainisha mtindo wa nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma. Lengo la tatu lilikuwa ni kutathmini matokeo ya mtindo wa nyimbo za tiba asili kwa wagonjwa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili za Mitindo na Simiotiki, pamoja na mbinu ya maelezo ya kinathari. Matokeo yanaonesha kwamba, kuna aina saba za nyimbo za tiba asili zinazotokana na dhima ya nyimbo hizo. Aina hizo ni nyimbo za maombi, kuomboleza, kufurahisha mizimu, kueleza historia, shkurani, kutolea tiba na nyimbo za kuaga. Vilevile, kuna mitindo mbalimbali inayotokana na matumizi na viziaadalugha. Mitindo hiyo, inahusiana na matumizi ya lugha ya kawaida na lugha ya kisanaa namatumizi ya nyimbo ndefu na fupi. Pia, kuna mishororo, fomula, dailojia, vina na mizani, uchezaji, utendaji wa kimuziki na matumizi ya maleba na vifaa. aidha, upo uhusiano wa moja kwa moja baina ya nyimbo na matibabu katika tiba asili. Matokeo ya nyimbo hizo kwa wagonjwa yamebainika kuwa ni pamoja na kuwatia moyo wagonjwa, kuwashirikisha katika mchakato wa tiba, kuburudika, kuwaongezea imani ya tiba na kufukuza majini wabaya. Utafiti huu ni kwamba, serikali ibuni sera za kuwaendeleza waganga wa tiba asili na kutoa kipaumbele kwenye tafiti za kitamaduni ili kulinda amali za taifa. Watafiti wengine wanaweza kufanya tafiti zaidi kuhusu maudhui ya nyimbo za tiba asili na jinsi zinavyofungamana na utamaduni na falsafa ya Kiafrika.

YALIYOMO

UTHIBITISHO.....	ii
HAKIMILIKI.....	iii
TAMKO.....	iii
TABARUKU.....	iv
SHUKURANI.....	v
ORODHA YA VIFUPISHO.....	vi
IKISIRI.....	vii
YALIYOMO.....	viii
ORODHA YA JEDWALI.....	xiv
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI WA JUMLA.....	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti.....	1
1.3 Tatizo la Utafiti.....	5
1.3.1 Malengo ya Utafiti.....	6
1.3.2 Lengo Kuu la Utafiti.....	6
1.3.3 Malengo Mahsusi ya Utafiti.....	6
1.3.4 Maswali ya Utafiti.....	6
1.4 Umuhimu wa Utafiti.....	6
1.5 Mawanda ya Utafiti.....	9
1.6 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake.....	9
1.7 Mpangilio wa Tasinifu.....	10

1.8	Hitimisho	11
SURA YA PILI		12
MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA.....		12
2.1	Utangulizi	12
2.2	Maandiko ya Kinadharia	12
2.2.1	Historia na Maendeleo ya Nyimbo	12
2.2.2	Nyimbo na Tiba Asili	13
2.2.3	Matumizi ya Nyimbo katika Tiba	16
2.3	Maandiko ya Kitafiti	18
2.3.1	Mtindo katika Nyimbo	18
2.4	Pengo la Utafiti	23
2.5	Kiunzi cha Nadharia.....	24
2.5.1	Nadharia ya Mitindo.....	24
2.5.1.1	Mihimili ya Nadharia ya Mitindo	28
2.5.1.1.1	Mhimili wa Uchambuzi wa Lugha.....	28
2.5.1.1.2	Mhimili wa Uchambuzi wa Vizaida-Lugha	30
2.5.2	Nadharia ya Simiotiki.....	31
2.5.3	Uhusiano wa Nadharia Zilizotumika.....	36
2.6	Hitimisho	37
SURA YA TATU		38
MBINU ZA UTAFITI.....		38
3.1	Utangulizi	38

3.2	Eneo la Utafiti	38
3.3	Usanifu wa Utafiti	39
3.4	Wango, Sampuli na Usampulishaji	40
3.4.1	Wango.....	40
3.4.2	Sampuli.....	40
3.4.3	Usampulishaji	41
3.3.3.1	Usampulishaji Nasibu Taratibishi.....	42
3.3.3.2	Usampulishaji Nujumu.....	42
3.4	Aina ya Utafiti.....	43
3.5	Vyanzo vya Data	43
3.6	Ukusanyaji wa Data	44
3.6.1	Ushuhudiaji.....	44
3.6.2	Mahojiano	45
3.7	Ukweli na Uhalali wa Data.....	45
3.8	Uchambuzi wa Data	46
3.9	Itikeli ya Utafiti	47
3.10	Hitimisho	50
	SURA YA NNE.....	51
	UAINISHAJI WA NYIMBO ZA TIBA ASILI ZA WAGANGA	51
4.1	Utangulizi	51
4.2	Aina za Nyimbo za Tiba Asili	51
4.2.1	Nyimbo za Maombi.....	53
4.2.1.1	Nyimbo za Maombi kabla ya Tiba.....	56

4.2.1.2	Nyimbo za Wakati wa Kuchimba Dawa	58
4.2.1.3	Nyimbo za Wakati wa Kutumia Dawa.....	59
4.2.2	Nyimbo za Kuomboleza	60
4.2.3	Nyimbo za Kufurahisha Mizimu.....	61
4.2.4	Nyimbo za Historia	63
4.2.5	Nyimbo za Shukrani.....	64
4.2.6	Nyimbo za Kutolea Tiba.....	65
4.2.7	Nyimbo za Kuaga.....	67
4.3	Hitimisho	67
SURA YA TANO		69
MTINDO KATIKA NYIMBO ZA TIBA ASILI ZA WAGANGA.....		69
5.1	Utangulizi	69
5.2	Mtindo wa Lugha katika Nyimbo za Tiba Asili	70
5.2.1	Matumizi ya Lugha ya Kawaida	72
5.2.2	Matumizi ya Lugha ya Kisanaa	76
5.2.2.1	Uchanganyaji Msimbo	77
5.2.2.2	Lugha ya Picha.....	84
5.2.2.3	Uradidi.....	85
5.2.3	Mtindo wa Nyimbo za Tiba Asili kutokana na Urefu.....	87
5.2.3.1	Urefu kwa Kigezo cha Idadi ya Maneno.....	87
5.2.3.2	Urefu kwa Kigezo cha Beti.....	89
5.2.3.3	Urefu wa Nyimbo kwa Kigezo cha Wakaa	92
5.3	Mishororo	94

5.3.1	Fomula.....	96
5.3.2	Daiolojia	99
5.3.3	Viunganishi.....	101
5.3.4	Vina na Mizani.....	103
5.3.5	Uchezaji.....	106
5.3.6	Utendaji wa Kimuziki	110
5.3.6.1	Muziki wa Ala.....	111
5.3.6.2	Muziki wa Sauti za Uimbaji	113
5.3.7	Sauti za Waimbaji	117
5.3.8	Maleba na Vifaa	119
5.3.8.1	Mavazi Kulingana na Makundi.....	121
5.3.8.2	Vifaa vya Uimbaji	126
5.3.9	Muktadha.....	130
5.4	Hitimisho	131
SURA YA SITA		132
TATHIMINI YA MATOKEO YA MTINDO WA NYIMBO ZA TIBA ASILI		
KWA WAGONJWA		132
6.1	Utangulizi	132
6.2	Mtindo wa Nyimbo za Tiba Asili	132
6.2.1	Matumizi ya Lugha ya Kawaida	132
6.2.2	Matumizi ya Lugha ya Kisanaa	133
6.2.2.1	Uchanganyaji Msimbo	134
6.2.2.2	Lugha ya Picha.....	135

6.2.2.3	Uradidi.....	136
6.2.3	Urefu.....	137
6.2.4	Daiolojia	138
6.2.5	Vina na Mizani.....	139
6.2.6	Uchezaji.....	141
6.2.7	Utendaji wa Kimuziki	141
6.2.8	Maleba na Vifaa	142
6.3	Hitimisho	142
SURA YA SABA.....		144
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO		144
7.1	Utangulizi	144
7.2	Muhtasari wa Tasinifu.....	144
7.3	Utoshelevu wa Nadharia Zilizotumika.....	145
7.4	Matokeo ya Utafiti	145
7.4.1	Lengo la Kwanza.....	146
7.4.2	Lengo la Pili.....	146
7.4.3	Lengo la Tatu	147
7.5	Mchango wa Utafiti.....	147
7.6	Mapendekezo ya Utafiti	148
7.7	Hitimisho	149
MAREJEO.....		150
VIAMBATANISHO		158

ORODHA YA JEDWALI

Jedwali Na 4.1:	Aina za Nyimbo za Tiba Asili.....	52
Jedwali Na 4.2:	Vipengele vya Mtindo.....	69

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Utafiti kuhusu nyimbo za kijamii umefanywa na wataalamu tofauti tofauti kwa mitazamo, misimamo na malengo mbalimbali, lakini bado haujafanywa kwa kiwango cha kuridhisha (Sengo, 2009). Tasinifu hii imefanywa kama sehemu mojawapo ya kushughulikia pengo lililobainishwa, kukuza na kuimarisha utafiti katika nyimbo za kiasili za kijamii kwa lengo la kuongeza machapisho na marejeleo katika fasihi ya Kiswahili. Ili kutimiza jukumu hilo, sura hii imewasilisha vipengele vya kiutangulizi vinavyohusu usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu na malengo mahsusi ya utafiti. Pia, kuna maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake; pamoja na mpangilio wa tasinifu nzima. Vipengele vyote hivi ndivyo vilivyoweka msingi wa kufanyika kwa tasinifu hii.

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Utafiti huu umechunguza mtindo katika nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma. Katika jamii nyingi, tiba asili zimekuwa zikitolewa kwa kuambatana na nyimbo wakati wa utoaji wake. Hali hii imeibua shauku katika uga wa fasihi wa kutaka kuona namna nyimbo zinavyotumika na mtindo wake unavyojipambanua; pamoja na kubaini umuhimu wa nyimbo hizo katika masuala yote yanayohusiana na tiba za asili za kijamii. Hivyo, dhana ya mtindo imepewa nafasi kubwa katika uchambuzi na uhakiki wa mitindo ya nyimbo teule.

Mtindo ni kipengele muhimu katika fasihi ambacho aghalabu hutumiwa kutofautisha kazi za kifasihi na zisizo za kifasihi. Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kuwa mtindo ni tabia ya pekee inayomtofautisha mtunzi au mwandishi mmoja na mtunzi mwingine. Kiini cha tofauti hizo hutegemea ufundi katika kubuni visa, mbinu za uwasilishaji, kiasi cha matokeo katika mguso wa hisia na unafsi wa mtunzi katika matumizi ya mbinu zinazomwezesha kufanikiwa kutawala fikra na vionjo vya hadhira yake. Mtindo haufundishiki, bali hutokana na ubunifu, umahiri, tajiriba na vitabia vya pekee vya mtunzi (Enkvist na Erik; 1973). Kifasihi, mtindo unaweza kufasiliwa kama sanaa ya uwasilishaji na ubunifu wa kazi ya fasihi inayoweza kumpambanua msanii mmoja na mwingine.

Mtindo ni matokeo ya matumizi ya lugha kwa njia isiyo ya kawaida ili kuleta athari maalumu kwa mpokeaji wa kazi ya fasihi (Eagleton, 1983). Mtindo huifanya lugha kuwa na utajiri wa tamathali, misemo, nahau na ubunifu wa hali ya juu ambao unahusisha ukiukwaji wa kaida za lugha. Ukiukaji huo hujitokeza katika matumizi ya lugha, katika sarufi, maana, sauti na hata msamiati ili kumvutia na kumuathiri msikilizaji au msomaji. Mtindo ndio humfanya msikilizaji au msomaji kuifurahia lugha iliyotumika huku akitafakari ujumbe uliobebwa katika matini inayohusika. Mtazamo huu unamakinikia mtindo katika ufundi na ubunifu (sanaa) wa kutumia lugha kwa namna ambayo itachagiza matokeo fulani ambayo msanii huyakusudia. Hivyo, mtindo ni mbinu ya matumizi ya lugha kimkakati.

Katika kuendelea kufafanua dhana ya mtindo, Wamitila (2008) anasema kwamba, mitindo hutumiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi unaohusisha maarifa ya isimu

na huweza kuelezwa kama nadharia ambayo ipo katikati ya isimu na fasihi. Nadharia hii ina mwelekeo wa kifani; na ina chunguza mtindo wa matini za kifasihi. Anahitimisha kwa kusema kwamba, mtindo huweza kuchunguza kinachosemwa au kuwasilishwa. Pia, mtindo huchunguza jinsi lugha inavyotumiwa katika fasihi. Mtazamo huu ni wa kimamboleo zaidi unafungamanisha mtindo katika mkabala wa kifasihi na kiisimu. Hivyo, mtindo unabainishwa kama sanaa ya fasihi inayowasilishwa kwa mbinu teule za matumizi ya lugha yenye lengo la kuchagiza matokeo fulani.

Mtindo ni upekee wa uundaji wa kazi za fasihi na hutofautiana baina ya msanii mmoja na mwingine kulingana na hisia za msanii huyo (Senkoro, 2011). Utofauti huo unaweza kujitokeza kwenye matumizi ya nafsi, uteuzi wa msamiati, mwanzo na mwendelezo wa kazi yake, usimulizi wa mwandishi, uchanganyaji wa tanzu mbalimbali za fasihi kama vile kuingiza kipengele cha wimbo katika fasihi andishi. Hoja hii inapambanua mtindo kama upekee katika uundaji wa kazi za fasihi. Aidha, inaonesha namna mtindo unavyoweza kuipambanua kazi za fasihi na kuupambanua utanzu mmoja na mwingine. Kwa upande mwingine, hisia za msanii mmoja ni tofauti na za msanii mwingine. Hata hivyo, utanzu mmoja unaweza kupambanuliwa kutokana na ufundi wa msanii katika matumizi ya lugha, uteuzi wa msamiati na namna ya uwasilishaji; na hata katika uchanganyaji tanzu.

Wapo wataalamu walionesha jinsi mtindo ulivyo na matokeo makubwa katika utendaji wa kazi za kifasihi kwa ujumla. Riffaterre (1983) akifafanua mtindo katika ushairi anaeleza kuwa ni kitendo cha msomaji au msikilizaji kukutana na matini ya

fasihi; na ni kukutana na kitu cha pekee ambacho sifa yake kuu bainifu. Mtindo huo unajidhihirisha kwa msomaji au msikilizaji kutokana na ukiukwaji wa taratibu za kisarufi zilizomo kwenye matini inayohusika. Ikumbukwe kuwa, matini yoyote ya kifasihi ina upekee ambao ni fasili rahisi ya ufasihi. Upekee huo ndio unaoitwa mtindo. Mtazamo huu ambao umejikita katika kufafanua sifa bainifu za mtindo katika mashairi kuwa ni ukiukaji wa taratibu za kisarufi. Ukiushi huu wa kaida hutofautiana kati ya msanii mmoja na mwingine. Mtindo humfanya msomaji au msikiliza kuweza kumtofautisha msanii mmoja na mwingine, utanzu mmoja na mwingine ama aina moja ya mashairi na nyingine. Mtindo unaonesha jinsi ushairi ulivyotofauti na tanzu nyingine zisizojikita katika ukiushi wa kisarufi.

Aidha, Miall na Kuiken (1994) wakifafanua mtindo katika nyimbo wanasema kuwa, mtindo huondoa vizuizi vya mtazamo wa msikilizaji na husaidia kuona baadhi ya vipengele vya ulimwengu vikiwa vipya, na wakati mwingine kuviona kwa mara ya kwanza.

Kwa upande wa fasihi, Wambua (2001) alichambua mtindo katika nyimbo zilizoimbwa na Kakai. Katika utafiti wake alibainisha uteuzi wa maneno na mbinu ya kuwasilisha maudhui ya msanii huyo. Vilevile, Mwanza (2007) alichunguza mtindo wa nyimbo za watoto unaoweza kutumika kama mbinu ya kufundishia na kujifunzia. Wataalamu hawa walichunguza mitindo kwa kugusia baadhi ya vipengele vya kifani na kimaudhui katika nyimbo walizozishughulikia. Mapitio hayo yalibainisha wazi kuwapo kwa haja ya kufanya utafiti kuhusu mtindo katika nyimbo za kijamii. Utafiti huu umeziteua nyimbo za tiba asili zinazotumiwa na waganga wa jamii za mkoani Ruvuma.

Kwa ujumla, dhana ya mtindo imefafanuliwa kwa mkabala jumuishi usiofungamana na kipera mahsusi cha fasihi. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba, mgawanyo wa kazi za kifasihi katika tanzu mbalimbali ni zao la mtindo. Kwa muktadha huo, kuna kila sababu ya kuuchunguza utanzu unaohusikan kwa kuzingatia sifa bainifu mahsusikwa kuzingatia muongozo wa mkabala jumuishi kama ulivyotumiwa na wataalamu watangulizi. Kwa kufanya hivyo, utafiti huu ulilitumia pengo la kimkabala kuidurusu na kushughulikia suala la mtindo kwa kuzingatia utanzu wa nyimbo za tiba asili. Kwa kuwa mtindo umebainishwa kuwa na umuhimu mkubwa kifani na kimaudhui katika kazi za kifasihi, utafiti huu umechunguza namna mtindo ulivyotumika katika nyimbo za tiba asili zinazotumiwa na waganga wa jadi wa jamii za mkoa wa Ruvuma.

1.3 Tatizo la Utafiti

Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu mtindo katika nyimbo za tiba asili (Juma, 2007; Wathome, 2009; Musyoka, 2010; Welsh, 2010 na Haji, 2011). Hata hivyo, hakuajawa na uthabiti katika uainishaji wa nyimbo za tiba asili. Tafiti zilizofanywa zilichunguza mtindo wa nyimbo za tiba asili kwa kuzingatia kigezo cha utumizi wa lugha bila kueleza nafasi ya mtindo wa nyimbo hizo katika tiba asili. Pamoja na ukweli kuwa matumizi ya nyimbo katika tiba asili yanaonekana kuwa sehemu muhimu ya tiba hizo; mpaka sasa uhusiano uliopo baina ya tiba zinazotolewa na nyimbo zinazotumika haupo bayana. Ipo haja ya kufanya utafiti kuhusu kipengele cha mtindo katika nyimbo za tiba asili. Hivyo, tasnifu hii imeshughulikia pengo hilo kwa kuchunguza mtindo katika nyimbo za tiba asili za Waganga wa jamii za mkoa wa Ruvuma.

1.3.1 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahsusi.

1.3.2 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mtindo na uhusika wake katika nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma.

1.3.3 Malengo Mahsusi ya Utafiti

- i. Kuainisha nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma.
- ii. Kubainisha mtindo unaotumika katika nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma.
- iii. Kutathimini matokeo ya mtindo wa nyimbo za tiba asili kwa wagonjwa.

1.3.4 Maswali ya Utafiti

- i. Nyimbo zipi za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma?
- ii. Mtindo gani hutumika katika nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma?
- iii. Mtindo wa nyimbo za tiba asili una matokeo gani kwa wagonjwa?

1.4 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa kufanya utafiti huu umechochewa na shauku ya mtafiti ya kutaka kukuza na kuendeleza fasihi simulizi ya Kiafrika kwa kutumia utanzu wa nyimbo za tiba asili ambazo hazijachunguzwa kwa kiasi cha kutosha, hasa katika kipengele cha mtindo. Hivyo, katika kuchunguza mtindo wa nyimbo za tiba asili za waganga mkoani Ruvuma, utafiti huu unatarajia kuchangia ukuzaji wa maarifa ya kutibu kwa

kutumia nyimbo, utunzi, uwasilishaji, utafiti, ufundishaji, upokezi na uhifadhi wa sanaa jadiya ya nyimbo na ushairi simulizi kwa ujumla.

Matokeo ya utafiti huu yanatoa mchango mkubwa kwa jamii kwa kuonesha jinsi nyimbo zilivyo na umuhimu katika suala la tiba. Katika jamii ya sasa, maendeleo ya sayansi na teknolojia yanawafanya watu wengi kutojua na kusahau tiba asili, kwa kuwa tiba nyingi hufanyika hospitalini. Hivyo, kupitia utafiti huu, jamii inaoneshwa umuhimu wa nyimbo katika tiba asili.

Matokeo ya utafiti huu ni hazina kubwa katika mbinu za utunzi na uwasilishaji wa nyimbo katika jamii mbalimbali za Kiafrika, kwani pamoja na mambo mengine, utafiti umeshughulikia miktadha ya kijamii inayoambatana na kuzuka, kukua na kustawi kwa nyimbo za tiba asili. Watunzi na wasanii wanahimizwa kuzingatia miktadha mahsusi ya kijamii katika utunzi na uhakiki wa tungo za kifasihi, zikiwemo nyimbo za kiasili.

Matokeo ya utafiti huu yanaweza kutumika katika kufanya tafiti linganishi za mitindo ya kiutendaji katika fasihi simulizi ya jamii nyinginezo za Kiafrika. Ingawa utafiti huu umejikita katika ushairi simulizi wa nyimbo za tiba asili pekee, matokeo na mapendekezo yaliyotolewa yanaweza kuchochea uchunguzi zaidi kwenye vipengele vingine vya fasihi simulizi na sanaa jadiya katika jamii nyingine za Kiafrika. Kwa hiyo, utafiti huu nirejeleo muhimu kwa watafiti wengine watakaopenda kufanya uchunguzi katika nyimbo na fasihi simulizi na vipera vyake.

Aidha, utafiti huu ni muhimu kwa sababu utaimarisha jitihada za ufundishaji wa fasihi simulizi katika viwango mbalimbali vya elimu. Kwa ujumla, ufundishaji wa fasihi simulizi unakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na data ya kutosha kuhusu tanzu za fasihi simulizi, hasa nyimbo. Kwa hiyo, utafiti huu uliochunguza mtindo wa nyimbo za tiba asili utachochea jitihada za ufundishaji na ujifunzaji wa nyimbo.

Vilevile, utafiti huu ni muhimu kwa sababu utaongeza kasi ya usambazaji na upokezi wa fasihi simulizi ya mkoa wa Ruvuma katika hadhira pana ya Waswahili na ulimwenguni kwa ujumla. Mpaka sasa, jamii nyingi za Kiafrika zimejibana mno katika hadhira finyu kwa kuwa zinawasilishwa kwa kutumia lugha za asili. Uchambuzi na uhakiki wa data zilizowasilishwa ulihusisha nyimbo za tiba asili za mkoa wa Ruvuma, zilizotafsiriwa kwa Kiswahili kutoka katika lugha za asili ili kuwekewa msingi imara wa kuifika hadhira pana. Utafiti huu umepanua, umeikuza na kuindeleza fasihi simulizi ya mkoa wa Ruvuma.

Kulingana na kasi ya mabadiliko ya kijamii yanayotokana na nguvu za sayansi, teknolojia na utandawazi, kuna hofu ya kupotea kwa fani za fasihi simulizi za Kiafrika kama vile nyimbo, hadithi na mivigha. Tofauti na jamii za zamani ambazo wanajamii walitumia fasihi simulizi kwa kiasi kikubwa, jamii ya sasa inakabiliwa na changamoto ya kupuuza matumizi ya fasihi simulizi kutokana na matumizi makubwa ya redio, televisheni, intaneti na simu. Kutokana na hofu hii, utafiti huu utachangia katika kuhifadhi sehemu kubwa ya fani hizi za jadi zinazopotea siku hadi siku. Kwa hiyo, utafiti huu utakuwa utatumika kama zana ya kulinda, kuhifadhi na kuenzi fani za jadi za Kiafrika dhidi ya upotevu unaosababishwa na mfumo mpya wa maisha ya kisasa. Kwa ujumla, utafiti huu umekuwa marejeo muhimu kwa upande wa aina za

nyimbo. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, kipengele cha nyimbo za tiba asili ni eneo ambalo halijashughulikiwa kwa mawanda mapana na wahakiki, watafiti na waandishi wengi. Hivyo, kukamilika kwa utafiti huu kumesaidia kupunguza tatizo la marejeo ya eneo hili, kwani watafiti wengi wameshughulikia nyimbo za aina nyingine na kuacha eneo hili bila kulifanyia wa kutosha. Aidha, umeibua mtazamo mpya kuhusu namna nyimbo za tiba asili zinavyotumika kama tiba katika jamii mbalimbali. Kwa kufanya hivyo, watafiti wengine wataibuka na kushughulikia vipengele vingine ili kuongeza hazina ya mawazo ya kitaaluma katika uwanja wa fasihi.

1.5 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchunguzi mtindo katika nyimbo za tiba asili za waganga wanaoishi mkoani Ruvuma. Baadhi ya vipengele vilivyoshughulikiwa vinavyohusu uainishaji wa nyimbo teule, uchambuzi wa mitindo na matokeo yake yameleezwa. Nyimbo zinazohusu tiba asili za jamii za mkoa wa Ruvuma zimechunguzwa kwa kuwa zina data za kutosha zilizohitajika ili kukamilisha malengo mahsusi ya tasnifu hii. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika tasnifu hii uliongozwa na nadharia ya Mitindo na ile ya Simiotiki.

1.6 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Mtafiti katika kazi hii alikumbana vikwazo mbalimbali. Kikwazo kimojawapo kilikuwa ni ugumu wa kupiga picha za mnato na video. Watafiti walisema ni kinyume na taratibu kupiga picha katika matendo yanayoshirikisha mizimu. Vilevile, kimaadili, ilisisitizwa kuwa si vema kumpiga kupigwa picha mgonjwa akiwa katika

harakati za kimatibabu. Kwa mujibu wa watafitiwa, kitendo hicho hakiifurahishi mizimu katika shughuli za uganga na tiba za asili. kwa hiyo, waganga wote walikataa na kusisitiza kuwa endapo picha zingepigwa nguvu zao zingechukuliwa na mizimu. Hivyo, kikwazo hiki kilitatuliwa kwa makubaliano na watafitiwa kuwa kazi ya ukusanyaji wa data ingefanyika kwa kutumia tepurekoda, kwa kuwa kinachohitajika ni sauti za nyimbo, siopicha. Kwa hiyo, utafiti ulikamilika kwa kurekodi sauti za nyimbo.

1.7 Mpangilio wa Tasinifu

Utafiti huu umekamilika ukiwa na sura sita. Sura ya kwanza imeelezea utangulizi wa jumla, usuli wa tatizo la utafiti na tatizo la utafiti. Pia, ina malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mawanda ya utafiti yameelezwa. Vipengele vingine vinahusu vikwazo vya utafiti na utatuzi wake ; na mwisho kuna mpangilio wa tasinifu nzima.

Sura ya pili inahusu mapitio ya machapisho pamoja na nadharia zilizotumika katika utafiti huu zimeelezwa. Nadharia ya mitindo na Simiotiki zilibainishwa na misingi yake kufafanuliwa. Aidha, pengo la utafiti limebainishwa katika sura hii.

Sura ya tatu imeeleza mbinu za utafiti zilizotumiwa katika ukusanyaji, uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa. Vipengele vingine katika sura hii ni eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji. Pia, mbinu za ukusanyaji data kama ushuhudiaji na mahojiano zimebainishwa na kufafanuliwa zana za utafiti; na zimeoneshwa jinsi zilivyotumika katika utafiti huu.

Sura ya nne, tano na ya sita zilihusu uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo. Sura hizi zimejengwa kwa kufuata malengo ya utafiti na uchambuzi wa data zilizochunguzwa na kuwasilishwa. Uwasilishaji na matokeo ya utafiti umefanywa kwa kujibu maswali ya utafiti. Uchambuzi na uhakiki wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya mitindo kwa kutumia mihimili ya uchanganuzi lugha na ile ya uchanganuzi wa viziada lugha. Pia, nadharia ya Simiotiki ya kijamii imetumika katika kuchambua maana za misimbo iliyojitokeza katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Sura ya saba inahusu muhtasari wa tasnifu, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, mapendekezo na hitimisho la utafiti.

1.8 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo, maswali, umuhimu, mawanda, vikwazo na mpangilio wa tasnifu. Katika sura hii ndipo msingi wa kufanyika kwa utafiti umejengwa kwa kuangalia usuli wa utafiti, kuweka malengo na namna utafiti ulivyofanyika. Pia, vikwazo vya utafiti vimeoneshwa na jinsi vilivyotatuliwa. Mwisho, sura hii imeonesha mpangilio wa tasnifu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumepitia kazi tangulizi zinazohusiana na malengo ya utafiti ili kupata maarifa na maoni ya wanazuoni waliotangulia. Kitaaluma, mtafiti anapaswa kutalii kazi za wanazuoni waliotangulia ili kuelewa mambo yaliyochunguzwa (Buchstaller na Khattab, 2013). Kipekee, ni jambo la msingi kutalii kazi hizo ili kuongeza maarifa na uzoefu zaidi katika taaluma ya uchunguzi. Miongoni mwa vipengele vilivyopewa nafasi katika sura hii vinahusu maandiko yanayohusu mtindo wa nyimbo, pengo la utafiti pamoja na kiunzi cha nadharia. Maandiko hayo tumeyagawa katika makundi mawili. Kundi la kwanza linahusu maandiko ya kinadharia na la pili linahusu maandiko ya kitafiti. Sura hii imeweka bayana pengo la utafiti. Mwisho, zimebainishwa nadharia zilizotumika katika utafiti huu.

2.2 Maandiko ya Kinadharia

Maandiko ya kinadharia yanasaidia kuonesha nadharia ambazo zipo, mahusiano baina ya nadharia hizo na jinsi zilivyofanyiwa kazi na husaidia kuunda nadharia mpya. Pia, maandiko ya kinadharia husaidia kuonesha nadharia zinazokosekana au zisizojitosheleza katika kufafanua matatizo mapya ya utafiti (Pearce, 2019).

2.2.1 Historia na Maendeleo ya Nyimbo

Thomson (1946) anasema kuwa nyimbo ni ushairi ambao huwasilishwa kwa lugha teule. Ili kujua historia ya ushairi, ni lazima kutambua historia na maendeleo ya lugha. Hii ni kusema kwamba, historia ya nyimbo imefungamana na binadamu

mwenyewe kwani utumizi wa lugha ni sifa bainifu ya binadamu. Hivyo, asili ya nyimbo ni harakati za binadamu mwenyewe katika jitihada za kukabiliana na harakati za maisha pamoja na mazingira yake. Historia hii inatadokeza kwamba, wimbo ni utanzu wa kidhima, ambapo binadamu huutunga na kuughana pale anapokuwa na jambo fulani linalopaswa kufanyika.

Senkoro (1988) anasema wimbo ndio fasihi ya mwanzo. Fasihi hii iliibuka baada ya kuzuka kwa lugha katika jamii. Wimbo ulitokana na kazi alizofanya mtu katika kupambana na mazingira yake. Pole pole alianza kutunga maneno na sauti zilizofuata mapigo ya zana za kazi. Baada ya muda alizitumia sauti hizo hizo za mapigo ya zana zake za kazi kujiambia nyimbo alipokuwa kifanya kazi. Wimbo wa kazi ulimpa nguvu mpya na ari zaidi ya kuendelea kufanya kazi. Senkoro anaendelea kufafanua kuwa, wimbo ulikuwa na nguvu za kisihiri zilizomfanya mtu asahau uchovu wake. Hivyo, mbali na dhima nyingine za nyimbo kama vile kuburudisha na kuadilisha, nyimbo zilitumika pia kama tiba. Mawazo haya ni yenye manufaa katika utafiti huu kwa sababu yanadokeza namna ya kuainisha nyimbo za tiba asili kikazi, jambo lililoshughulikiwa katika utafiti huu.

2.2.2 Nyimbo na Tiba Asili

Dickens (1969) anasema kuwa neno ‘tiba’ limetokana na kitenzi cha Kigiriki “therapium” na nomino “therapeia”. Kwa mtazamo wake, neno “therapium” lina maana ya kujali/kumjali na “therapeia” ni huduma na tiba. Anahitimisha kuwa, nyimbo za tiba ni sanaa ya kutumia sauti za nyimbo katika kuleta mabadiliko kutoka katika ugonjwa kwenda katika uzima.

Aidha, Nketia (1982) anaeleza kuwa tiba asili imekuwapo katika jamii nyingi za Kiafrika kwa muda mrefu, huku nyimbo zikitumika katika mchakato wa matibabu na kuwasiliana na Mungu mponyaji. Hapa anadokeza matumizi ya nyimbo za tiba asili. Katika utafiti huu, tumechunguza mtindo wa nyimbo za tiba asili na matokeo ya mtindo wa nyimbo hizo kwa wagonjwa wanaotibiwa. Mawazo ya Nketia yamesaidia kutoa mwanga kwa kuangalia jinsi mtindo wa nyimbo unavyotumika katika tiba asili na kuwasiliana na miungu. Mawazo hayo yamepeleka mbele utafiti huu kwa kuonesha umuhimu wa nyimbo katika tiba.

Edrtsieck (2001) anaeleza kuwa, historia ya tiba asili ni ndefu kama zilivyo historia za jamii mbalimbali ulimwenguni. Tiba asili ndio ilikuwa njia pekee ya kukabiliana na maradhi ya aina mbalimbali katika jamii nyingi za Kiafrika kabla ya Ukoloni kulingana na mfumo wa jamii inayohusika. Aina na mtindo wa nyimbo ulitofautiana kutoka jamii moja hadi jamii nyingine.

Katika kuangalia nyimbo na tiba asili ni vema tukadurusu historia ya nyimbo za tiba. Kwa kuanza, tujiulize nyimbo za tiba ni nini? Hizi ni nyimbo zinazoimbwa na kutumika wakati wa tendo la tiba. Nyimbo ni mojawapo ya sanaa zinazohusiana na muunganiko wa sauti zenye uzuri wa umbo na zenye kuelezea hisia fulani (Alvuede, 2006 na Patrick, 1972). Wimbo huweza kutumia ala za muziki. Hivyo, wimbo na muziki ni dhana zenye uhusiano. Huu ndio msingi wa Wamitila (2004) kueleza na kuisitiza kuwa, katika jamii nyingi, vyombo vya muziki huwa ndio msingi mkuu wa kugawa aina mbalimbali za nyimbo. Lengo mojawapo katika utafiti huu ni kuainisha nyimbo. Mawazo ya Wamitila (2004) yamekuwa chachu katika lengo hilo, ambapo

mkabala wa dhima unatumika, na si vyombo vya muziki kama anavyoeleza. Pia, tunatumia mfungamano wa matukio kama sehemu ya vifaa vinavyobainisha mitindo mbalimbali katika nyimbo za tiba asili.

Katika kipengele hiki, tumefafanua maana ya waimbaji wa nyimbo za tiba asili ambapo katika sehemu nyingi imebainishwa waimbaji ni mganga pamoja na wazumi. Dhana ya Wazumi (*chorus*), ilianzia Uyunani ya Kale, ikirejelea kikundi cha waimbaji na wachezaji katika sherehe za kidini, sanaa na sanaa za maonesho. Walikuwa ni kiungo kati ya waigizaji na hadhira. Kuna wakati waliitwa waigizaji. Walivaa maleba wakati tendo la uigizaji likifanyika (Weiner, 1980). Katika utafiti huu wazumi ni wagonjwa, wasaidizi wa mganga, wapiga ngoma na wote wanaoshiriki kuimba, ukimuondoa fanani. Tumewaita wazumi kwa sababu ushiriki wao katika uimbaji katika nyimbo za tiba asili unafanana na matendo ya wazumi wa Uyunani.

Alvuede (2006) anafafanua kuwa, wataalamu wa nyimbo za tiba wamegawanyika katika aina tatu. Kwanza, ni wataalamu wa mitishamba. Hawa ni wale ambao wana ujuzi wa kutibu kwa kutumia mimea na sehemu za mwili (viungo) vya wanyama. Pili, ni wale watumiao nguvu za mizimu katika kutibu. Tatu, wataalamu wanaotibu kwa imani. Katika kuwafafanua wataalamu wanaotibu kwa imani, Mume (1973) anasema kuwa, hawa ni waganga wanaotibu kwa nguvu za imani za kidini. Tofauti na mawazo hayo, Sengo (1995) anasema kuwa, kuna aina mbalimbali za uganga. Baadhi yake ni uganga wa nyago, uganga wa makafara, uganga wa mazinguo, uganga wa hirizi, uganga wa mizimu, uganga wa utabiri na uchawi. Anaeleza

kueleza kuwa, si uganga wote unaotumia nyimbo katika tiba, bali uganga wa mizimu.

Katika aina zote hizo za uganga zilizotajwa, utafiti huu umechunguza uganga wa mizimu ambao huambatana na nyimbo za tiba. Sengo (1995) anafafanua kuwa, katika aina hii ya uganga, nyimbo huimbwa ili kupunguza maumivu na kutibu wagonjwa waliodhoofika. Katika utafiti huu, tumebainisha na kuchambua aina za nyimbo za tiba asili, mtindo wa nyimbo unaotumika katika tiba asili na kuweka bayana matokeo ya mtindo wa nyimbo hizo kwa wagonjwa wanaotibiwa.

2.2.3 Matumizi ya Nyimbo katika Tiba

Historia inaonesha kwamba, muziki na nyimbo vimekuwa vikitumika katika tiba kwa karne nyingi hadi hivi leo ambapo nyimbo za tiba zinaendelea kutumika katika jamii mbalimbali. Nguvu za uponyaji kwa njia ya muziki na nyimbo upo katika historia ya tamaduni mbalimbali duniani (Gouk, 2000; Horden, 2000; Wigram na wenzake, 1995; Campbell 1991 & Pratt na Jones, 1988). Hata katika maandiko ya vitabu vitakatifu, katika masimulizi ya *Biblia*, Sauli na Daudi wanazungumziwa katika nukuu hiyo:

“Basi bwana wetu na atuamuru sisi watumishi wake waliopo hapa mbele yako watafute mtu aliye stadi wa kupiga kinubi; basi itakuwa, roho ile mbaya kutoka kwa Mungu itakapokujilia, yeye atapiga kinubi kwa mkono wake, nawe utapona (*1 Samwel, 16:16*).”

Maelezo hayo yanaonesha jinsi nyimbo na muziki ulivyoanza kutumika karne nyingi kama njia mojawapo ya tiba. Katika nukuu hiyo ya *Biblia* inaonesha kuwa kifaa kilichotumika. Matumizi ya kifaa hicho yanabainisha mtindo uliotumika katika kutoa

tiba, kwani utafiti huu umeonesha vifaa vya kimuziki kama sehemu ya mtindo. Pia, utafiti huu umeonesha matokeo ya mtindo wa nyimbo za tiba asili uliotumika katika kutibu wagonjwa.

Historia inaendelea kuonesha kwamba, nyimbo za tiba zilikuwapo na zimekuwapo wakati na baada ya Vita ya Pili ya Dunia. Katika kipindi hicho, nyimbo za tiba zilitumika kuwashughulikia watu waliojeruhiwa kutokana na athari ya vita (Gioia, 2006). Akifafanua zaidi anasema kuwa, nyimbo za tiba zilianza kufundishwa huko Marekani katika Chuo cha Michigan mwaka 1944. Baadhi ya wataalamu wanahusianisha nyimbo na tiba na watu wa jamii ya Kigiriki na Warumi na Wamesopotamia ama Wamisri (Horden, 2000).

Gioia (2006) akifafanua zaidi kuhusu historia ya nyimbo za tiba anasema, nyimbo za tiba za Kiafrika zimekuwa zikiongezeka zaidi katika karne mbili zilizopita. Mawazo ya wataalamu hawa yanaonesha matokeo ya nyimbo za tiba asili kuwa ni kutoa tiba. Pia, wanaonesha jinsi nyimbo hizo zilivyoanza kutumika karne nyingi zilizopita. Maelezo hayo yana mchango mkubwa katika utafiti huu kwa kuwa yameonesha historia na namna nyimbo za tiba zilivyotumika. Hivyo, katika utafiti huu tunaangazia namna nyimbo zilivyotumika na zinavyotumika na matokeo yake katika kutoa tiba kwa wagonjwa.

Alvuede (2006) katika makala yake aliyoandika kuhusu nyimbo za tiba katika jamii za Kiafrika anaeleza kwamba, suala la ni lini na ni vipi nyimbo za tiba zilianza katika bara la Afrika, bado ni fumbo mpaka sasa. Hali hii inatokana na kukosekana kwa kumbukumbu za kimaandishi za watu wa zamani, ingawa kutoka katika vyanzo vya

taarifa za kihistoria zilizoandikwa na wasafiri wa Marekani na wafanyabiashara, suala la nyimbo za tiba lilizungumziwa kwa kiasi fulani (Sourthen, 1971). Hoja ya Alvuede haitofautiani na hoja zilizotolewa na Gioia (2006) ambaye anaishia kutaja mwaka ambao nyimbo zilianza kufundishwa kwa kuzihusisha na Wagiriki. Katika utafiti huu tumechunguza matumizi ya nyimbo kutoka enzi za kale.

Kwa ujumla, Bacharachi (1977) anasema kwamba, Wamisri wa kale walikuwa na vifaa vya muziki ambavyo baadaye vilienea mpaka Ugiriki; na wanaamini kuwa, vifaa vya muziki vilianza Misri na havikuishia kuburudisha tu, bali vilitumika katika kutoa taarifa ya vita na kutumika makanisani na katika tiba. Matumizi ya vifaa vya muziki yanabainisha mtindo utumikao katika nyimbo zinazohusika. Upigaji na ala sauti zinazotokana na vifaa hivyo, hutofautiana kati ya aina moja na nyingine. Utafiti huu unaonesha jinsi mtindo wa upigaji vifaa unavyobainisha aina za nyimbo za tiba asili na matokeo ya matumizi ya mtindo huo.

2.3 Maandiko ya Kitafiti

Maandiko ya kitafiti ni yale yanayotokana na tafiti zilizofanywa kwa njia kama vile za ushuhudiaji, ushiriki na mahojiano. Maandiko haya hudokeza maarifa na mbinu mbalimbali za kitafiti (Pearce, 2019) kama yanavyoelezwa katika sehemu inayofuata.

2.3.1 Mtindo katika Nyimbo

Musyoka (2012) alifanya utafiti wa mtindo wa nyimbo za mazishi ya Wakamba. Katika utafiti huo alichunguza nyimbo za mazishi ya Wakristo kutoka katika jamii ya Wakamba nchini Kenya. Katika utafiti wake alibaini kwamba, lugha iliyotumiwa ina tamathali za semi kwa wingi. Anaendelea kufafanua kwamba, matumizi ya tamathali

kwa wingi huvuta hisi za hadhira kwa njia ya upekee. Aidha, utafiti wa Musyoka ulijikita zaidi katika kipengele kimoja tu cha mtindo wa matumizi ya lugha. Utafiti huu tofauti na wa Musyoka (2012) umeangalia mtindo kwa mawanda mapana kwa kuonesha kila tendo linaloambatana na uimbaji pamoja na upekee katika matumizi ya lugha ni mtindo. Vilevile, umepiga hatua zaidi mbele kwa kuangalia namna mtindo wa nyimbo unavyoleta matokeo kwa wagonjwa. Haji (2011) alichunguza nyimbo za tiba asili kwa kumakinikia uganga wa pepo. Anaendelea kueleza kwamba, mganga wa pepo hujulikana kwa majina tofauti tofauti kama vile Jalim (mwalimu/maalim), fundi au mganga. Nchini Afrika Kusini, mganga wa aina hii huitwa Sangoma. Sangoma huimba, hucheza na kupiga ngoma kwa lengo la kumwita shetani na kusema naye (Encarta, 2009). Haji (2011) anaendelea kufafanua kwamba, katika hatua za mganga kumpandisha pepo mgonjwa, nyimbo huimbwa na ngoma kupigwa. Lengo la kumwita shetani au pepo aje kichwani mwa mgonjwa ni kwa ajili ya kutoa tiba.

Uchunguzi wa Haji ulituongoza katika utafiti huu ili kufikia malengo, hususani kujua matokeo ya nyimbo za tiba baada ya kuona matendo yanayoambatana na nyimbo katika tiba. Pia, ulisaidia kubainisha mtindo wa nyimbo za tiba asili kwa kuangalia matendo ya wagonjwa, hasa nyimbo zinaimbwa. Kulingana na uchunguzi wa Haji, kila hatua ya kufanya uganga ina nyimbo zake. Kuna nyimbo mahsusi katika hatua ya kumwita shetani, hatua ya kupewa chano, pamoja na hatua ya kupewa uzali (kilemba). kwa kurejelea uainishaji wa Haji, utafiti huu umelenga kubainisha aina za nyimbo kwa kutumia mtindo wa uimbaji unaoambatana na hatua mbalimbali za kufanya uganga linatoa mwanga kwa utafiti wetu.

Welsh (2010) alifanya utafiti wa nyimbo za tiba katika baadhi ya jamii za Afrika Magharibi, Afrika Mashariki na Kati, Afrika Kaskazini na Kusini. Katika utafiti wake alibaini kuwa, nyimbo za tiba asili huambatana na matendo mbalimbali kama vile upigaji ngoma, mavazi maalumu, kuamsha na kuwatuliza pepo. Utafiti huu wa Welsh ulichunguza matendo yatendekayo katika nyimbo za tiba asili tu; hakuchunguza mtindo wake. Utafiti wa Welsh utatusaidia katika utafiti huu kwenye ubainishaji wa matendo katika kuonesha jinsi maleba yanavyotumika. Utafiti huu unayaweka maleba katika muktadha wa mtindo.

Wathome (2009) alitafiti mabadiliko ya mtindo katika nyimbo za tohara za jamii ya Wakamba. Katika utafiti wake alishughulikia mabadiliko ya mitindo ya nyimbo za tohara. Vilevile, alitafiti athari ya elimu na dini katika mtindo wa nyimbo hizo. Mwisho, alichunguza athari ya ethnografia ya uzungumzaji katika kuainisha mabadiliko mbalimbali ya nyimbo hizo. Matokeo ya utafiti huo, yalionesha kwamba, mapisi ya kiwakati, mfumo wa kisasa wa elimu, dini za Kimagharibi na maendeleo ya sayansi na teknolojia ni mambo yaliyoathiri mtindo wa nyimbo hizo. Katika utafiti wetu, mtindo ni kila kitu kinachofanyika katika tendo la tiba kikiambatana na nyimbo. Hata hivyo, utafiti wake unasaidia katika kuchunguza baadhi ya vipengele vya mtindo katika nyimbo za tiba asili mkoani Ruvuma.

Rajwayi (2009) alifanya utafiti kuhusu maudhui na mtindo katika nyimbo za msanii Faustin Munishi. Katika utafiti wake alichambua maudhui na mtindo katika nyimbo za msanii huyo. Matokeo ya utafiti huo yalionesha jinsi maudhui ya nyimbo hizo yanavyobadilika kutokana na mpito wa wakati. Pia, mtafiti amezungumzia uhusiano

uliopo baina ya maudhui anayozungumzia mwimbaji huyo na tamathali alizotumia katika uwasilishaji wa maudhui. Vilevile, ameangalia mabadiliko kwa kuzingatia wakati na mazingira yake. Hivyo, bado utafiti huo ulitoa nafasi kwetu ya kutafiti nyimbo za tiba asili za waganga wa jadi mkoani Ruvuma, kwani baadhi ya vipengele kama tamathali za semi vimeshughulikiwa katika utafiti wetu.

Juma (2007) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya lugha katika nyimbo za uganga huko Zanzibar. Katika utafiti wake alibaini kwamba, nyimbo za uganga hutumia lugha ya mafumbo ambapo humfanya msikilizaji kufikiri sana ili kujua kilichokusudiwa. Anaendelea kufafanua kuwa, ufumbaji huo hutumia maneno machache yenye kugusa hisia za watu. Akifafanua zaidi anasema kuwa, nyimbo za uganga wa pepo hutumia ishara na taswira ili kuficha kilichokusudiwa. Anahitimisha kuwa, matumizi hayo ya lugha ya mafumbo husaidia kufikisha ujumbe kwa ufupi ili kuifanya hadhira kutafakari matumizi hayo ya lugha. Utafiti wa Juma ulishughulikia kwa kiasi suala la mtindo, hasa katika kipengele cha matumizi ya lugha. Hivyo, utafiti wake umetoa mchango katika uchanganuzi wetu wa data. Utafiti wetu umeonesha kwa kiwango kikubwa jinsi mtindo unavyojipambanua katika nyimbo za tiba asili.

Mwanza (2007) alifanya utafiti wa mtindo wa nyimbo za watoto wa shule za chekechekea. Katika utafiti wake aligundua kwamba, nyimbo za watoto zinaweza kutumika kufundishia lugha na maudhui kwa watoto wa chekechea kama ilivyo katika tanzu nyingine za kifasihi. Mchango wa utafiti huu ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa unasaidia kubainisha mtindo kwa kutumia lugha na maudhui yaliyopo

katika nyimbo za tiba asili. Pia, unasaidia uainishaji wa nyimbo za tiba asili. Hata hivyo, mtafiti amejikita katika kipengele cha lugha na maudhui kitu ambacho kinatoa nafasi katika utafiti wetu kusonga mbele zaidi na kuifafanua dhana ya mtindo kwa mapana kwa kuhusisha matendo yote yanafanyika uimbaji kama sehemu ya mtindo.

Edrtsieck (2001) alifanya utafiti wa nyimbo za tiba asili huko Mbozi, mkoani Songwe. Katika utafiti wake alichunguza jinsi nyimbo zinavyotumika katika matendo na matukio mbalimbali yanayoambatana na tiba. Baadhi ya matendo aliyoyabaini ni pamoja na tendo la tiba na utafutaji dawa. Katika utafiti huo alibaini kuwa, nyimbo zilitumika kupandisha pepo kwa mgonjwa na mganga. Pepo kwa mgonjwa hueleza yanayomkabili mgonjwa, ilhali pepo kwa mganga huonesha dawa za kumtibia mgonjwa. Utafiti huu haukuwa wa kifasihi, lakini umetoa mchango mkubwa katika tafiti za kuchunguza mtindo katika nyimbo za tiba asili.

Wambua (2001) alifanya utafiti wa mtindo katika nyimbo zilizoimbwa na Kakai Kilonzo. Katika utafiti huo, Wambua anaonesha namna msanii Kakai Kilonzo alivyoteua maneno na mbinu alizozitumia katika kuwasilisha maudhui yake. Pia, ameangalia uhusiano uliopo baina ya uteuzi wa maneno na maudhui katika kazi hizo alizoshughulikia. Utafiti huo wa mtindo katika nyimbo za mwanamuziki Kakai Kilonzo unasaidia katika utafiti huu ambao umeshughulikia mtindo wa nyimbo za tiba asili. Katika utafiti wake, Wambua (2001) ameshughulikia kipengele kimoja cha mtindo na kuonesha kinavyoibua maudhui. Katika utafiti huu tunauchukulia mtindo kama dhana pana kwa kuangalia vipengele mbalimbali vinavyojitokeza wakati wa

uimbaji kuwa nisehemu ya mtindo. Vilevile, Sengo (1995) alitafiti jamii ya Waswahili inavyotumia nyimbo kama sehemu ya kupunguza maumivu kwa vijana wafanyiwao jando na unyago. Anasema kuwa, wari huimbiwa nyimbo kama sehemu ya dawa na kuombewa wapone haraka. Maelezo haya ya Sengo yanaelekeza jinsi nyimbo zinavyotumika katika tiba. Sengo hajaonesha ni mtindo gani wa nyimbo hizo hutumika kama sehemu ya dawa. Hivyo, mawazo haya yanasaidia katika utafiti huu katika kubainisha matokeo ya nyimbo za tiba asili kwa wagonjwa.

Kwa kuhitimisha, sehemu hii tumedurusu mikabala mbalimbali ya kitafiti inayoelezea mtindo kwa namna tofauti. Mikabala hiyo inachagiza umuhimu wa kufanya tafiti zaidi kuhusiana na mtindo katika nyimbo. Hivyo, utafiti huu umedurusu mitazamo ya tafiti hizo tangulizi na kujikita katika kuchunguza mtindo katika nyimbo za tiba asili kwa mkabala wenye mapana na wa kina zaidi kutoka pale watafiti watangulizi walipoishia.

2.4 Pengo la Utafiti

Mapitio ya tafiti zinazohusu mtindo yamebainisha kuwa, watafiti wengi (Sengo, 1995; Wambua, 2001; Juma, 2007 na Wathone, 2009) wamefanyika kuhusu mtindo kwa ujumla wake, hasa katika matumizi ya kipengele cha lugha. Hapana shaka kuwa kuna uhaba mkuwa wa tafiti zinazochunguza mtindo katika nyimbo za tiba asili katika kipengele cha matumizi ya lugha; pamoja na uhusiano uliopo baina ya vipengele hivyo na matokeo ya tiba asili kwa wagonjwa. Pia, kuna uhaba wa tafiti za mtindo kwa kuhusisha na viziada lugha. Hivyo, tasnifu hii imeshughulikia pengo hilo kwa kuchunguza mtindo katika nyimbo za tiba asili za Waganga wa jamii za mkoa wa Ruvuma.

2.5 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ni zao la utamaduni na historia ya jamii inayohusika. Nadharia hutazamwa kama dira inayosaidia kupata ukweli na kuthibitisha jambo kwa madhumuni maalumu (Wafula & Njogu, 2007). Pia, hufungamana na muktadha, pamoja na masuala ya kijamii ya kihistoria yaliyoizalisha kazi inayohusika ; na ni mwongozo unaosaidia kutoa maelezo kuhusu namna jambo fulani linavyopaswa kufanyika ili kutoa matokeo yanayoweza kuaminika na kukubalika kitaaluma (Sengo, 2009). Kwa ujumla, nadharia ni zao la jamii mahsusi na zinaweza kutumiwa katika miktadha mbalimbali. .

Uchambuzi na mjadala wa data zilizowzsilishwa katika utafiti huu uliongozwa na nadharia za Mitindo na Simiotiki. Nadharia hizo ziliteuliwa kwa sababu uchambuzi, uhakiki na mjadala wa data uliwekewa mkazo katika utafiti wa vipengele vya mtindo katika nyimbo za tiba asili za Waganga wa jamii za mkoa wa Ruvuma. Nadharia hizi zilikuwa muafaka katika uchunguzi, uchambuzi, uhakiki na mjadala wa data katika vipengele vilivyolengwa. Uteuzi wa nadharia zilizobainishwa ulizingatia misingi imara ya kutegemeana na kukamilishana kwa kuzingatia mada ya utafiti uliofanyika.

2.5.1 Nadharia ya Mitindo

Nadharia ya Mitindo hii ina misingi yake tangu nyakati za wanafalsafa wa Kiyunani, hususani Aristotle. Baadhi ya wanazuoni (Chatman, 1967; Leech ,1969; Crystal na Davy, 1969; Leech na Short, 1981 na Simpson, 2004) walioindeleza nadharia hiyo wakiwa na mwelekeo uliokitwa kwenye msingi wa uchambuzi wa vipengele vya kisarufi vinavyoashiria upekee wa sifa za matini.

Baadaye, mtindo uliweza kuhusishwa na lugha ya maandishi, lugha ya kifasihi au isiyokuwa ya kifasihi, ingawa kwa kawaida huwa unahusishwa na matini za kifasihi zilizoandikwa. Katika uandishi wa fasihi, istilahi “mtindo” hutumika kwa maana nyingi kama sehemu ya mazoea ya lugha kama wanavyosema Wana-Mitindo (Crystal na Davy, 1969). Pia, wanasema kuwa, tunaweza kuhusisha mtindo na mazoea ya matumizi ya lugha ya mtu binafsi au jamii-lugha; ndiyo maana huwajia watu akilini wanapozungumza kuhusu mtindo wa uandishi wa mtu fulani, mtindo wa kuzungumza wa kutoa hotuba hadharani. Maelezo haya yanaweza kutumika katika kuonesha jinsi tanzu mbalimbali za fasihi na vipera vyake vinavyoweza kujipambanua.

Leech (1969) anaeleza kuwa, Mitindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu kama taaluma unaofungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu, ingawa haijismamii. Msamiati mpana wa kimsingi wa uhakiki wa kifasihi hususan sitiari, taswira, kinyume, kinaya, kejeli, usambamba na jazanda hauwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana za kiisimu. Kwa hivyo, kama msingi wa kutumia taaluma za kifasihi na za kiisimu. Mitindo ni uwanja ambamo masuala haya hushughulikiwa.

Kwa mujibu wa Kristek (1999) anaeleza kuwa, fasili kuhusu nadharia ya mitindo kwa muda mrefu imekitwa kwenye mawanda finyu yanayoakisi mtazamo wa kiisimu kuhusu dhana ya matini kuwa imeundwa na lugha. Kwa mtazamo huu, kazi ya mwanamitindo ni kuchambua vipengele vya lugha katika ngazi zote vinavyoashiria upekee wa matumizi ya lugha kwenye matini inayohusika. Katika utafiti huu, dhana ya matini inahusishwa na mtazamo wa Bakhtin (1986) kuwa ni kitu chochote

kinachoweza kutoa taarifa. Kwa kuzingatia mtazamo huu, dhana ya matini inavuka mipaka ya kiisimu na kuhusisha muktadha wa utendekaji wa tanzu mbalimbali za fasihi, ikiwa ni pamoja na mazingira ya uimbaji wa nyimbo. Kwa hiyo, vitu kama maleba, matendo, vifaa vya muziki na miondoko ya kimwili kwa pamoja vinaunda matini za fasihi simulizi katika kipera cha nyimbo.

Kwa kuzingatia upanuzi huu, dhana ya matini, hatuna budi kufasili upya. Nadharia ya Mitindo ilitoa mwanya kwa nadharia hiyo kufumbata vipengele vya kimtindo vinavyovuka mipaka ya kiisimu (lugha). Mwelekeo huu unazingatia maoni ya Kristek (1999) kwamba, uchambuzi wowote wa mtindo unapaswa kuzingatia muktadha ili kuweza kufasili dhima ya vipengele vya kimtindo katika matini. Kwa maelezo haya, matendo katika utendekaji wa fasihi yanapaswa kuchukuliwa kuwa ni vipengele vya mtindo.

Dhana ya utendaji katika fasihi imezungumziwa na wataalamu mbalimbali (Bauman, 1975; Foley, 1995 na Schechner; 2013). Kwa mujibu wa wataalamu hao, kama walivyonukuliwa na Kadallah (2018) wanaeleza kuwa, wahakiki wa matini za fasihi sharti wachunguze zaidi ya lugha na kuhusisha utendaji unaoambatana na matini inayohusika. Kuna mihimili mitatu inayosaidia kuumba, kuwasilisha na kufasiri tajriba za wanadamu katika matini za kifasihi. Baadhi ya mihimili hiyo inahusu muundo wa tukio la kiutendaji kulingana na muktadha wa uwasilishaji, utangamano wa fanani na hadhira wakati wa uwasilishaji wa matini ya fasihi na mfanyiko wa kimawasiliano kulingana na kaida za utamaduni wa jamii inayochunguzwa. Maelezo haya yana maana kwamba, vipengele vinavyounda matini za fasihi vinavuka mipaka

ya kilugha na kuhusisha vipengele vya viziada lugha ambavyo ni muhimu katika uchambuzi wa mtindo. Hivyo, mihimili hii imetusaidia katika utafiti huu kwenye kuchunguza mtindo wa nyimbo za tiba asili kwa kuuhusisha na muktadha, utangamano wa fanani na hadhira kwa kuhusisha na utamaduni.

Kwa mujibu wa Schechner (2013) utendaji ni tukio la aina yoyote ile linalowajumuisha hadhira pamoja na fanani wake kwa minajili ya kuigiza au kuonesha tabia za wanadamu. Katika utanzu wa nyimbo, kuna matendo yanatendeka wakati wa uimbaji yanayowahusisha wahusika wenye dhima tofauti tofauti. Katika nyimbo za tiba asili, wahusika ni mganga, wagonjwa, wauguzi, wasaidizi wa waganga na kikundi maalumu cha waimbaji (wazumi). Kutokana na maelezo ya Schechner (2013), matendo ya waimbaji, vifaa vya muziki, maleba na miondoko ya kimwili ndiyo kiini cha mtindo wa matini katika muktadha wa uimbaji. Mkabala huu wa Schechner umetusaidia katika uchambuzi wa viziada lugha katika nyimbo za tiba asili.

Katika mwendelezo wa uchambuzi wa viziada lugha, Okpewho (1992) anaona kuwa, utendaji wa fasihi simulizi ya Kiafrika unapaswa kuzingatia sio tu maneno yanayotamkwa kwa kutumia lugha ya mdomo, bali pia ujumbe unaowasilishwa kwa kutumia ishara au viziada lugha. Viziada lugha ni kitu chochote kinachotumika katika utendekaji wa kipera cha fasihi na kuwa sehemu ya mtindo wa matini inayohusika (Kadallah, 2018). Kwa hiyo, katika nyimbo za tiba asili, ngoma, maleba na mijongeo ya kimwili ya waimbaji inayotokana na ama kupagawa au urazini ni sehemu ya viziada lugha ambayo imechambuliwa katika utafiti huu.

Kwa ufupi, katika mwelekeo unaodokezwa na Okpewho (1992), ishara za uso, mikono, uchezaji pamoja na sauti za muziki zinaunda mtindo wa matini za kifasihi. Mtaalamu huyu anasisitiza kuwa, mbali na maneno ya mdomo, wasanii wa kifasihi simulizi hutumia mbinu mbadala katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira iliyolengwa. Katika uafiti huu mbinu ya viziada lugha imetumika.

2.5.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Mitindo

Nadharia ya mitindo tangu kuasisiwa kwake imejengwa katika mihimili changamani ambayo katika utafiti huu imeunganishwa na kupata mhimili mmoja tu wa uchambuzi wa lugha. Kutokana na upanuzi wa dhana ya matini; na kisha, upanuzi wa dhana ya mitindo, nadharia ya Mitindo inachukua sura ya mawanda mapana, na hivyo, kuongeza mhimili wa pili wa uchambuzi wa viziada lugha.

2.5.1.1.1 Mhimili wa Uchambuzi wa Lugha

Mhimili wa uchambuzi wa lugha unahusu vipengele vya lugha katika viwango vyote vya lugha. Simpson (2004) anasema kwamba, nadharia ya Mitindo ina viwango ambavyo mchanganuzi wa matini ya kifasihi anahitaji kuvizingatia ili kutekeleza uhakiki kwa njia inayofaa. Simpson anaendelea kufafanua kuwa, mambo ya kimsingi ambayo yanafaa kuchunguzwa katika kazi ya kifasihi na mhakiki ambaye anatumia mwelekeo wa kihakiki wa mtindo. Anayataja mambo hayo kuwa ni lugha ya kitamathali na mtindo, uteuzi na mtindo, sarufi na mtindo, uchimuji na mtindo, usimulizi na mtindo, itikadi na mtindo, muwala, mshikamano na mtindo. Pia, kuna mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo.

Leech na Short (2007) wanafafanua zaidi mawazo ya Simpson kwa kuelezea mihimili ya mtindo. Aidha, waliorodhesha aina za ukiushi wa kaida za matumizi ya lugha ambayo hutokea katika mtindo wa kazi za kifasihi. Aina hizo ni ukiushi wa kimsamiati, ukiushi wa kisarufi, ukiushi wa kilahaja, ukiushi wa sajili, ukiushi wa kifonolojia, ukiushi wa kimaandishi, ukiushi wa kihistoria na ukiushi wa kisemantiki. Maelezo haya yanaungwa mkono na Wamitila (2008) ambaye anaeleza kuwa, nadharia ya Mitindo inajikita kwenye uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa. Uchunguzi huu wa lugha unapania kubainisha ubunifu uliopo kwenye lugha hiyo; na unasaidia katika uelewekaji wa matini au kazi za kifasihi.

Wamitila (2008) anaendelea kusema, maarifa yanayotokana na isimu hutumiwa ili kubaini sifa za kimtindo za kazi. Sifa hizi zinaweza kuwa za kifonolojia (ruwaza za sauti, vina, mizani), kisintaksia (miundo ya sentensi, aina ya sentensi), kimsamiati (maneno dhahania na maneno dhabiti, kuwapo na idadi ya nomino, vielezi na vivumishi) na kibalagha (matumizi ya tamathali za usemi, urudiaji na mbinu za urudiaji huo, jazanda).

Katika utafiti huu, mhimili huu umetumika katika kuchambua data za lengo la kwanza ambalo linalohusu uainishaji wa nyimbo za tiba asili. Pia, umesaidia katika kuchunguza vipengele vya lengo la pili ambalo linahusu kuchunguza mtindo unaotumika katika nyimbo za tiba asili. Mhimili huu umechunguza matumizi ya lugha katika vipengele mbalimbali vinavyojitokeza kama vile vina, mizani, miundo ya sentensi, mipangilio ya mishororo katika beti, mpangilio wa viunganishi, urudiaji na mbinu za urudiaji. Baadhi ya vipengele katika lengo la pili havitaweza

kushughulikiwa kwa kutumia mhimili huu wa uchambuzi wa lugha bali tutatumia mhimili wa viziada lugha. Halikadhalika lengo la tatu baadhi ya vipengele vitachanganuliwa kwa kutumia mhimili huu kwa uchambuzi wa lugha na vingine vitachambuliwa kwa kutumia mhimili wa uchambuzi wa viziada lugha. Mhimili wa uchambuzi wa viziada lugha tunaofafanua katika sehemu inayofuata na kuonesha vipengele vitakavyochanganuliwa kwa mkabala huo.

2.5.1.1.2 Mhimili wa Uchambuzi wa Vizaida-Lugha

Mhimili wa uchambuzi wa viziada lugha unahusu uchambuzi wa vitu au matendo ambayo si lugha, lakini ni sehemu muhimu ya mtindo wa kazi ya fasihi simulizi. Matendo ambayo yamebainishwa na mhimili huu katika utafiti huu yanaambatana na dhima ya tendo linalohusika. Mhimili huu umetumika katika kuainisha nyimbo za tiba asili kama linavyofafanua lengo la kwanza la utafiti huu. Okpewho (1992) anaeleza kuwa, viziada lugha ni mtindo wa kiutendaji unaoambatana na dhima ya tendo linalohusika, unaotumiwa na wahusika katika kuwasilisha ujumbe usioegemea katika matumizi ya vipashio vya kiisimu.

Katika utafiti huu, mitindo ya viziada lugha iliyojadiliwa kwa kutumia mhimili huu imetokana na utendakazi wa nyimbo, hasa zinazohusumaombi, kuomboleza, kufurahisha mizimu, historia, shukrani na za kutolea tiba. Utendakazi huo, huibua uziada lugha kwa washiriki kama vile kujiviringisha chini, kuzungusha shingo, uchezaji wa kurukaruka kwa kutumia makalio, kudondoka na kupoteza fahamu na uchezaji wa kuweka mikono kichwani.

Nadharia ya mitindo imefaa katika uchambuzi wa data kwa kiasi kikubwa, lakini haikufaa katika kutambua maana ya misimbo au ishara zilizowasilishwa katika nyimbo za tiba asili. Ili kuona ni kwa namna gani misimbo na ishara hizo zina fafanuliwa na zinafikisha ujumbe tulitumia nadharia ya Simiotiki ya kijamii ambayo tunaifafanua sehemu inayofuata.

2.5.2 Nadharia ya Simiotiki

Simiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara au uashiriaji. Kihistoria, kuibuka kwa nadharia ya Simiotiki kunahusishwa na mawazo ya Ferdinand de Saussure na Charles S. Peirce katika karne ya 20 (Fenner 2010). Kadallah (2018) anaeleza kwamba Simiotiki ni nadharia inayochunguza uhusiano baina ya miundo ya ndani na miundo ya nje katika mifumo ya kijamii. Kulingana na Barthes (1964) nadharia ya Simiotiki inaundwa na kitajwa, ishara na kirejelewa. Dhana hizi hufanya kazi kutokana na athari za ushirikiano wa ishara, kitajwa na kirejelewa. Kwa ujumla, Simiotiki inasaidia kuchanganua miundo ya mifumo anuai ya kijamii kama vile lugha, fasihi, siasa na uchumi. Ili kuelewa vyema aina mahsusi ya mfumo wa kijamii, tunapaswa kuchunguza namna umbo la ndani linavyohusiana na umbo la nje. Umbo la ndani hurejelea maana na umbo la nje hurejelea ishara au elementi ndogo ndogo zinazojenga mfumo unaohusika.

Wahakiki wa Kisimiotiki ambao mitazamo yao inakidhi haja na matakwa ya mtindo unaotokea katika fasihi simulizi ni pamoja na Barthes (1964) na Eco (1984). Kwa mujibu wa Eco, ishara ni kila kitu kinachoweza kutumika kuwakilisha kitu kingine. Mtazamo huu unashabihiana na wa Barthes (1964) ambaye anasema kuwa, ishara ni

dhana inayorejelea hali ya kukifanya kitu kimoja kusimama badala ya kitu kingine. Kwa mujibu wa Barthes (1964), ishara za Kisimiotiki zinaundwa na kitendwa (*object*) na kibainishi (*modifier*).

Mitazamo ya Eco na Barthes kuhusu nadharia ya Simiotiki ina tija kubwa katika utafiti huu kwa kuwa muelekeo wake unaihusisha jamii. Aidha, maelezo ya wataalamu hawa yamezingatia hali halisi ya dhana ya udhihirikaji wa Simiotiki katika kazi za kifasihi. Kutokana na mtazamo huu, ishara sio lazima zitokane na misimbo ya kiisimu, bali zinaweza kuwa kitu chochote kinachotumika kupashia maana katika mchakato wa kimawasiliano. Hivyo, kuna utangamano mkubwa baina ya muktadha, maana na ishara. Tumechanganua utangamano huu kwa kuzingatia misimbo inayotokana na ishara, mandhari na maana. Kulingana na mhimili huu, kitu chochote kinaweza kuwa ishara ikiwa watu wa jamii fulani watakifasiri kama kirejelea kinachosimama kwa niaba ya kitu kingine. Kwa ujumla, nadharia hii inaelekeza namna ya kufahamu matumizi ya lugha, ishara na mandhari kwa kutumia utamaduni wa jamii mahsusi.

Katika utafiti huu, tumeitumia mihimili ya nadharia ya Simiotiki ya kijamii kama iliyopendekezwa na mhakiki wa kifasihi, Roland Barthes. Kwa mujibu wa Barthes (1964), lengo la nadharia hii ni kuchunguza uhusiano baina ya maana ya kazi ya kifasihi na vijenzi vya kimtindo vilivyozua maana hizo. Nadharia hii imetumika kufafanua maana mbalimbali zinazowakilishwa na ishara zinazotumika katika uimbaji na uchezaji wa nyimbo za tiba asili. Pia, imetumika kuchambua aina mbalimbali za misimbo inayopatikana katika uimbaji na uchezaji wa nyimbo za tiba asili.

Kulingana na Barthes (1964), misimbo ya Kisimiotiki inayojadiliwa katika kazi za kifasihi na inaakisi mtindo katika kazi za fasihi. Kwa hiyo, uhakiki wa Kisimiotiki unamhitaji mhakiki kuivunja kazi ya kifasihi katika sehemu zake ndogo ndogo (leksia). Kila leksia hudhihirisha misimbo na kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri mtindo wa kazi ya kifasihi. Aidha, kutokana na Barthes, uhakiki wa kifasihi unaoongozwa na nadharia ya Simiotiki hauna budi kubainisha, kuchanganua na kufafanua misimbo mikuu ya Kisimiotiki inayojitokeza katika kazi ya kifasihi. Misimbo hiyo imejumuisha matukio, anwani, maneno ya lugha na utamaduni.

Aina ya kwanza ni msimbo wa matukio. Msimbo huu unahusu jinsi ishara zinazojengwa kutokana na mpangilio wa matukio au visa katika hadithi au simulizi fulani. Kwa kutumia msimbo huu, mtunzi anajenga visa na matukio kwa njia ya ishara. Msimbo wa pili ni ule wa kihemenitiki. Huu ni msimbo unaojengwa katika kazi ya kifasihi kupitia anwani ya kazi inayohusika. Anwani hiyo inaweza kuwa jina la kitabu, shairi, igizo au jina la mhusika. Kutokana na anwani hiyo mtunzi hujenga taharuki akilini mwa hadhira. Aidha, kwa kutumia msimbo wa kihemenitiki tunaweza kufahamu maana na kusudio la mtunzi kwa kudadisi kile kinachorejelewa na mtunzi katika kazi yake ya fasihi.

Aina ya tatu ni msimbo wa kiseme. Huu ni msimbo ambao unajengwa kwa kutumia maneno yenye kutoa maana ya kisemantiki. Maana ya kisemantiki hupatikana kwa kurejelea vipengele nasibishi vya kiisimu kama vile nahau, methali na sitiari zinazotumika katika kazi ya kifasihi. Aina ya nne ni msimbo wa kiutamaduni. Msimbo huu unajengwa kutokana na matumizi ya viashiria vya utamaduni katika

kazi ya kifasihi. Viashiria mbalimbali vya kiutamaduni vinavyotumika katika kazi ya kifasihi huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu vinavyoeleweka miongoni mwa wasomaji au watazamaji, hivyo kuipa kazi ya kifasihi nguzo za kiutamaduni. Msomaji/mtazamaji anaposema anaelewa akisemacho mtunzi huwa anasema hivi kutokana na viashiria vya msimbo huu.

Baadhi ya watafiti walioitua nadharia ya Simiotiki katika uchunguzi wa kazi za kifasihi ni Mturo (2011) aliyechunguza kipengele cha dhamira katika semi zilizoandikwa katika daladala zilizoko katika jiji la Dar es Salaam. Kimsingi, anaeleza Mturo kwamba, uchambuzi na uhakiki wa Kisimiotiki hudhibitiwa na miundo na miindo ya kifani iliyopo katika kazi iliyohusika. Hali hiyo huwafanya wachambuzi na wahakiki kuamini kuwa hadhira huathiriwa na mazingira ya kiwakati na kimahali katika upokezi wa kazi fulani. Maelezo haya yalimpa mtafiti fursa pana ya kuzichunguza nyimbo za tiba asili kama zao mahsusi la jamii iliyochunguzwa. Mtafiti alichunguza uhusiano uliopo baina ya nyimbo za tiba asili kuptia shughuli za uganga na tiba kulingana na utamaduni na mienendo katika jamii iliyochunguzwa katika utafiti huu.

Aidha, Nzobe (2012) aliyetumia kuchunguza uhusiano uliopo kati ya wanajamii na kupitia nyimbo za ngoma ya Wigashe ya jamii ya Wasukuma nchini Tanzania. Utafiti huu kama wa Nzobe ulimfanya mchunguzi kuwa na uhusiano wa karibu na jamii ya jamii za mkoani Ruvuma ili kujua tabia, mienendo na shughuli zao katika nyanja zote zinazohusiana na masuala ya uganga na tiba za asili kwa kurejelea nyimbo za tiba asili katika maeneo teule. Jambo hili linatokana na ukweli kwamba,

mtafiti hawezi kujitenga na matukio ya jamii anayoichunguza kwa sababu kazi yake ni kiungo chake. Mchunguzi hana budi kuliangaza suala hili kwa umakini katika uhakiki wake. Utafiti huu ulizichunguza nyimbo za tiba asili kwa umakini ili kupata data kulingana na mada ya utafiti uliofanyika.

Rajabu (2012) alitumia nadharia ya Semiotiki katika uhakiki wa misemo ya Kiswahili katika vazi la fulana. Kulingana na Rajabu, hadhira hutengeneza maana ya kazi fulani ya fasihi kupitia ubunifu na tafsiri zao kuhusu ya ishara zilizotengenezwa na msanii. Utengenezaji wa maana hutegemea sana muktadha wa mnyambulishaji wa ishara zilizotumika katika kazi inayohusika. Mtafiti alitumia nadharia hii kuzichunguza ishara, picha na taswira zilizomo katika nyimbo za tiba asili ili kubaini dhamira zilizomo katika nyimbo hizo. Kitu chochote kitakuwa alama kama watu watakifasiri kwa niaba ya kitu kingine. Huu ndio msingi wa uteuzi wa nadharia hii iliyochunguza kipengele cha mtindo katika nyimbo za tiba asili zilizolengwa katika utafiti huu.

Mgogo (2017) alitumia nadharia ya Simiotiki katika utafiti wa hadithi za jamii ya Wanyiha wanaoishi mkoa wa Songwe nchini Tanzania. Mgogo alizitazama hadithi za Wanyiha kama chombo thabiti kisichoweza kujitenga na maisha ya jamii iliyolengwa. Aidha, alichunguza na kuhakiki kwa undani uhusiano uliopo baina ya hadithi na jamii kama vitu viwili vinavyotegemeana na kuathiriana; na kwamba, haviwezi kutenganishwa kwa namna yoyote. Jambo hilo linatazamwa kuwa uhusiano wake ni sawa na pande mbili za sarafu ambazo haziwezi kuachanishwa. Fasihi haina budi kuchukuliwa kama ilivyo na uhusiano usiotatanika katika maisha ya jamii.

Nyimbo za tiba asili zilichunguzwa kwa kuzingatia muktadha mpana wa jamii iliyolengwa ili kuyaelewa masuala ya uganga na tiba kupitia nyimbo zake.

Katika uchambuzi, uhakiki na mjadala wa data, mtafiti aliwaweka waganga na waimbbaji wa nyimbo za tiba asili katika ulimwengu wao wa kawaida, kweli na halisi. Wasanii walitazamwa kwa undani jinsi walivyoyachunguza masuala ya uganga na tiba na kuyaweka kama yalivyo, yanavyoaminika na kukubalika kupitia nyimbo zao. Nyimbo za tiba asili zilichunguzwa kwa uwazi bila chuku ili kufanya uchambuzi na uhakiki unaokubalika na kuaminika. Nadharia hii iliteuliwa na kuwekewa misingi katika uchunguzi wa kipengele cha mtindo katika nyimbo za tiba asili. Eneo la utafiti lilipewa uzito ili kuonesha hali iliyopo katika nyimbo za tiba asili zinazoimbwa na waganga.

2.5.3 Uhusiano wa Nadharia Zilizotumika

Uchambuzi, uhakiki na mjadala wa data zilizowasilishwa katika utafiti huu uliongozwa na nadharia za Mitindo na Simiotiki. Nadharia hizi ziliteuliwa na kutumiwa ili kukidhi mada na malengo mahsusi yaliwekewa mkazo katika uchunguzi wa vipengele vya mtindo katika nyimbo za tiba asili za jamii za mkoa wa Ruvuma zilizoshughukiwa katika utafiti huu. Nadharia hizo ziliteuliwa kama msingi wa mjadala na uhakiki wa vipengele vilivyobainishwa. Nadharia hizo zilitegemeana na kukamilishana ili kukidhi malengo ya mada na mjadala wa data zilizolengwa na kuwasilishwa katika tasnifu hii.

2.6 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia mapitio ya maandiko na kiunzi cha Nadharia. Maandiko hayo yamewezesha kujenga hoja mbalimbali za kiutafiti ambazo zimejenga kazi hii. Baadhi ya vipengele vilivyopitiwa ni historia ya nyimbo, historia ya tiba asili, nyimbo zake na mtindo wa nyimbo za tiba asili. Katika sehemu inayofuata mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu zimefafanuliwa.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii imejadili mbinu za utafiti zilizotumika katika tasnifu hii. Sura hii imegawanyika katika vipengele anuwai vinavyofafanua eneo la utafiti, wango, sampuli na usampulishaji. Vipengele vingine ni mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za uchambuzi wa data na ukweli na uhalali wa data za utafiti. Mwisho, linatolewa hitimisho kuhusiana na sura ya mbinu za utafiti.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika Mkoa wa Ruvuma. Mkoa wa Ruvuma upo Kusini mwa Tanzania. Mkoa huo umeenea kati ya latitudo 90 35' hadi 110 45' Kusini mwa Ikweta na longitudo 340 35' hadi 380 10' Meridiani. Mkoa wa Ruvuma upande wa Kusini umepakana na nchi ya Msumbiji, upande wa Magharibi kuna Ziwa Nyasa na upande wa Kaskazini na Mashariki umepakana na mkoa wa Njombe. Pia, upande wa Kaskazini-Magharibi umepakana na mkoa wa Mtwara. Mkoa huo una eneo la kilometa za mraba 64,493. Kiutawala, mkoa huu una wilaya 6 ambazo ni Songea Mjini, Songea Vijijini, Namtumbo, Tunduru, Nyasa na Mbinga. Jamii zinazopatikana mkoani Ruvuma ni Wamatengo, Wangoni, Wayao, Wanyasa, Wandendeule, Wamakua, Wampoto, Wamanda, Wanindi, Wamatambwe na Wabena.

Kwa kawaida, uteuzi wa eneo la utafiti unafanyika katika mawanda mapana na mawanda finyu (Yin, 2011). Utafiti huu umefanyika katika mkoa wa mkoa wa Ruvumamahsusi. Maeneo mahsusi yaliyoteuliwa katika mkoa wa Ruvuma ni wilaya

ya Songea Mjini na Songea Vijijini. Maeneo hayo yaliteuliwa kwa sababu takwimu zimeonesha kuwa na waganga wengi wa tiba asili ukilinganisha na maeneo mengine ya mkoa wa Ruvuma. Data hizo zimepatikana kutoka Chama cha Waganga wa Jadi, Wakunga na Mangaliba wa Tiba Asili wa Mkoa wa Ruvuma (CHAWATASO). Taarifa kutoka chama cha waganga wa tiba asili kinaonesha Songea Mjini ina waganga 211, Songea Vijijini 71, Natumbo 33, Tunduru 20, Nyasa 17 na Mbinga 16.

3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpango maalumu unaobainisha mtiririko wa upatikanaji wa data zinazohitajika. Usanifu wa utafiti ni mpangilio unaoonesha sura nzima ya utafiti unavyopaswa kufanyika kuanzia katika hatua ya ukusanyaji wa data mpaka hatua za uandishi wa ripoti (Cooper, 1989 na William, 2008). Pia, hutoa picha kamili inayoonesha jinsi utafiti utakavyofanyika tangu unapoanza mpaka hatua za uandishi wa ripoti. Usanifu wa utafiti huonesha vipengele muhimu vitakavyoshughulikiwa katika utafiti unaohusika.

Katika tasnifu hii mbinu ya uchunguzi kifani imetumika. Uchunguzi kifani ni utaratibu maalumu unaomwezesha mtafiti kuteua jambo mahsusi ambalo atalishughulikia katika utafiti wake (Troachim, 2006 na Charkrabarthy, 2012). Uchunguzi kifani katika tasnifu hii ni mtindo wa nyimbo za tiba asili za jamii za mkoa wa Ruvuma. Mbinu hii ilimruhusu na kumpa uhuru mtafiti kuteua na kuvichunguza vipengele vya mtindo, vilivyomwongoza kupata data za msingi katika nyimbo na vipengele vilivyolengwa. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata data za kutosha zilizowezesha kukamilisha utafiti wake.

3.4 Wango, Sampuli na Usampulishaji

Katika sehemu ndogo ndogo kuanzia 3.3.1 hadi 3.3.3 unatolewa ufafanuzi kuhusu wango unaohusihwa na utafiti huu. Kisha sampuli inayotokana na wango huo imeoneshwa na kuthibitishwa uwakilishi wake. Hatua za usampulishaji zinaelezwa hatua kwa hatua ili kuonesha bayana jinsi sampuli ilivyopatikana.

3.4.1 Wango

Wango kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018) ni jumla ya watu au vitu vinavyoweza kutumiwa kama sampuli ya utafiti. Hii ina maana kuwa utafiti lazima uwe unaihusu jamii ya aina fulani katika mazingira halisi. Wango linaweza kuwa watu katika jiji au vitu vyenye sifa sawa vinavyopatikana kwenye eneo mahsusi la kijiografia(Kothari, 2009). Katika utafiti huu wango linajumuisha nyimbo, waganga na wagonjwa katika wilaya za Songea Mjini na Songea Vijijini katika mkoa wa Ruvuma.

3.4.2 Sampuli

Babbie (1992) anafasili sampuli kuwa ni sehemu ndogo ambayo mtafiti anaitumia katika ukusanyaji wa taarifa zinazomsaidia kufikia malengo ya utafiti. Sampuli ni seti ya vitu ambavyo mtafiti anachagua kutoka kwenye kapu kuu na inayoweza kujumuishwa sifa zake kwenye wango (Neuman, 2014). Wango ni jumla ya vitu, watu au dhana zilizopo kwenye ulimwengu halisi ambao utafiti umekusudiwa kufanyika (Polit na Hungler, 1997). Kwa mujibu wa Baker (2010), kinadharia, sampuli inapaswa kuwa na sifa ya ulinganifu na uwakilishi wa wango unaohusika.

Kwa jumla, sampuli ni kundi dogo la watafitiwa ambalo hutoa taarifa muhimu zinazohitajika katika utafiti ambazo humwezesha mtafiti kupata data za utafiti wake.

Katika utafiti huu sampuli imegawanya katika makundi mawili. Ugawanywaji ulifanyika ili kukidhi mahitaji ya malengo yaliyowekwa. Jumla ya watafitiwa 50 walishirikishwa katika ukusanyaji data. Sampuli ya kwanza ilijumuisha waganga 19 kwa uwiano sawa kutoka katika wilaya za Songea Mjini na Songea Vijijini. Mtafiti alifanya mahojiano na kundi hili kwa lengo la kupata data zinazohusu mtindo wa nyimbo za tiba asili, hasa katika kuonesha sababu ya kutumia nyimbo hizo katika tiba na matokeo yake. Mahojiano na kundi hili yalisaidia kupata data kuhusu uainishaji wa nyimbo za tiba asili.

Sampuli nyingine iliwahusu wagonjwa. Katika kundi hili, wagonjwa 30 walijumuishwa kutoa data kuhusu mtindo unaotumika katika nyimbo za tiba asili. Sampuli ya utafiti huu ilitumika katika kukusanya data kwa njia ya kushuhudia na mahojiano. Idadi ya sampuli hii ilitumika kwa kuwa ilitosha kukidhi mahitaji wa utafiti.

3.4.3 Usampulishaji

Usampulishaji ni mchakato wa kupata sampuli kutoka katika wango iliyokusudiwa (Kothari, 2008). Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua vitu mahsusi maalumukwa ajili ya kuchunguzwa kwenye utafiti. Mchakato wa usampulishaji unahitaji kufafanua ni kitu gani kitakuwa sampuli na kwa idadi ipi. Baker (2010 na Yin, 2011) wanaweka wazi kwamba, ulinganifu na uwakilishi ni masuala makuu ya kinadharia katika mchakato wa usampulishaji. Kuna mbinu mbalimbali za

usampulishaji kama vile usampulishaji tabakishi, usampulishaji nasibu taratibishi na sampuli mtajo. Mbinu ya usampulishaji hutegemea fursa na usampulishaji unaoshughulikiwa.. Katika utafiti huu, usampulishaji nasibu taratibishi umetumika kupata sampuli ya watafitiwa kutoka katika wilaya mbili zilizoteuliwa.

3.3.3.1 Usampulishaji Nasibu Taratibishi

Usampulishaji nasibu taratibishi, hii ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ambapo sampuli huteuliwa kutoka katika chanzo cha data kinasibu, lakini kwa kufuata utaratibu uliowekwa na mtafiti wa kuruka idadi maalumu ya vitu au watu (Bryman, 2004). Katika mbinu hii ya usampulishaji nasibu taratibishi, mtafiti huwagawa watafitiwa katika makundi kutegemea sifa zao na aina ya utafiti anaoufanya; na kisha, kuteua idadi fulani ya sampuli kutoka katika kila kundi kulingana na mahitaji ama malengo ya utafiti. Utafiti huu umefanyika katika wilaya za Songea Mjini na Songea Vijijini. Mtafiti aliteua waganga 19 kwa uwiano sawa katika wilaya mbili zilizobainishwa. Orodha ya CHAWATASO ilitusaidia kupata waganga 144 kati ya 282 wanatumia nyimbo. Mtafiti aliyapanga majina kwa alfabeti kwa kila eneo. Kisha, aliamua kuchukua jina moja kila baada ya majina 8 kwa kila upande. Hivyo, alipata majina ya waganga 14 kutoka Songea Mjini na majina 5 kutoka Songea Vijijini.

3.3.3.2 Usampulishaji Nujumu

Usampulishaji nujumu ni mchakato usio wa bahati nasibu ambapo mtafiti humchagua mtu yeyote anayetokea na kukutana naye bila mapangilio rasmi kutegemeana na upatikanaji. Maelezo ya Buchstaller na Khattab (2013) ni kwamba, mbinu hii ni ya haraka na rahisi; na inaweza kutekelezeka pale ambapo sifa

inayochunguzwa inaelekea kuwa jumuishi katika wango unaohusika. Mbinu hii imetumika kuteua wagonjwa, ambapo jumla ya wagonjwa 30 waliteuliwa. Hivyo, mbinu hii ilisaidia kupata data zilizohusu uainishaji wa nyimbo za tiba asili na kubaini mtindo wa nyimbo za waganga mkoani Ruvuma.

3.4 Aina ya Utafiti

Utafiti huu ni wa uwandani. Data za msingi zilikusanywa mkoani Ruvuma katika Wilaya ya Songea Mjini na Songea Vijijini. Maeneo hayo yaliteuliwa kwa kuwa yalikuwa na mawanda ya kutosha kupata data zilizolengwa kukidhi mahitaji ya utafiti huu. Pia, mtafiti alidurusu nyaraka mbalimbali kutoka katika maktaba ya mkoa wa Ruvuma, makumbusho ya Majimaji mkoani Ruvuma na katika tovuti na wavuti mbalimbali kwa ajili ya urejelezi na ufafanuzi wa data za msingi za utafiti uliofanyika. Maktaba na tovuti hizi ziliteuliwa kwa kuwa zina machapisho ya kutosha yaliyohusiana na mada ya tasnifu hii.

3.5 Vyanzo vya Data

Katika tasnifu hii tumekusanya data za msingi ambazo zimetumika katika kukamilisha utafiti huu. Data za msingi ni nyimbo zinazohusu tiba za asili kutoka katika wilaya mbili zilizobainishwa. Data za msingi ni zile zilizokusanywa kwa mara ya kwanza kabisa katika utafiti fulani. Aidha, ni zile ambazo hazijawahi kukusanywa na mtu mwingine kwa ajili ya utafiti kama anaofanya mtafiti wakati huo (Yin, 1984 na Frankfort-Nachmias na Nachmias, 2000). Katika tasnifu hii, tumekusanya data za msingi mkoani Ruvuma katika wilaya ya Songea Mjini na Songea Vijijini. Maeneo hayo yalitupatia data zilizokidhi mahitaji ya utafiti huu. Kama ilivyokwishaelezwa,

mtafiti alidurusu nyaraka mbalimbali kutoka katika maktaba ya mkoa wa Ruvuma na makumbusho ya Majimaji mkoani Ruvuma kwa ajili ya urejelezi na ufafanuzi wa data za msingi za utafiti uliofanyika. Maktaba hizi ziliteuliwa kwa kuwa zina machapisho ya kutosha yaliyohusiana na mada iliyochunguzwa.

3.6 Ukusanyaji wa Data

Katika utafiti huu data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za uwandani. Data zilikusanywa kwa mbinu za ushuhudiaji na mahojiano.

3.6.1 Ushuhudiaji

Kwa mujibu wa Kaahwa (2008), ushuhudiaji ni mchakato wa kufuatilia tukio au mwenendo wa jambo katika mazingira halisi na kuweka kumbukumbu ya mwenendo unaohusika kwa utaratibu maalumu. Ushuhudiaji ni mbinu ya ukusanyaji data ambapo mtafiti anachunguza kwa kuangalia watafitiwa moja kwa moja uwandani bila kumuuliza mtu mwingine (Kothari, 1990). Mbinu hii humsaidia mtafiti kukwepa vizingiti vya kukumbana na wasailiwa wanaodanganya ama wanaokataa kutoa data kutokana na sababu zinazolenga kuhitaji fedha kwa kuwa mtafiti hujionea mwenyewe. Mbinu hii hutazamwa kuwa ni moja ya njia za kisayansi za ukusanyaji wa taarifa za utafiti (Dawson, 2002). Mbinu hii husaidia kuondoa upendeleo, kwani kwayo mtafiti hulazimika kwenda eneo la tukio na kukusanya data kwa kushuhudia kinachofanyika. Kwa kutumia mbinu hii, tulifanikiwa kukusanya nyimbo na kushuhudia matendo mbalimbali yanayofanyika wakati wa uimbaji na utendaji katika nyimbo za tiba asili. Ushuhudiaji huu ulifanyika uwandani katika jukwaa la kuimbia nyimbo ambapo huambatana na tiba. Matendo yote hayo yamechanganuliwa na kubainisha mtindo wa nyimbo za tiba asili.

3.6.2 Mahojiano

Kombo na Tromp (2006) wanafasili mahojiano kuwa ni majibizano ya ana kwa ana au kwa simu au barua-pepe kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa. Katika utafiti huu, mahojiano ya ana kwa ana yamefanyika baina ya mtafiti, waganga na wagonjwa. Maswali baina ya waganga na wagonjwa yalitofautiana kwa kuwa data zilizohitajika kwa waganga ni tofauti na zilizohitajika toka kwa wagonjwa. Waganga walihojiwa kuhusu sababu za kutumia nyimbo katika tiba, uteuzi wa mandhari maalumu na matumizi ya maleba yenye rangi mbalimbali pamoja na vifaa vingine. . Wagonjwa walihojiwa kuhusu wanavyojisikia wakati na baada ya kuimba nyimbo. Mahojiano yalikuwa huria kwa kuzingatia maswali ya muongozo.

3.7 Ukweli na Uhalali wa Data

Utafiti wowote ule unapaswa kuwa thabiti na wenye kuaminika kwa kuhakikisha kuwa data zilizokusanywa ni sahihi na ya kweli. Vilevile, utafiti unakuwa thabiti na wenye kuaminika kama matokeo yake yatakuwa si yenye kubadililabadilika. Katika utafiti wa kitakwimu na ule usio wa kitakwimu huwa inazingatiwa kama matokeo yake yana ushikamani. Pia, kuaminika hujitokeza pale ambapo kuna uhusiano wa taarifa zilizotolewa na watu wale wale kwa muda tofauti (Furlong na Lovelace, 2000). Kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kuzalisha matokeo yale yale pale utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu hizo.

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa mbinu za ushuhudiaji na mahojiano. Uchambuzi na uhakiki wa data uliongozwa na nadharia za Mitindo na Simiotiki,

pamoja na mbinu ya kitaamuli. Upungufu wa mbinu ya moja hukamilishwa na ubora wa mbinu nyingine (Best na Khan, 2006). Mjadala kuhusu uhalali wa mbinu zilizotumika ulifanyika baina ya mtafiti na wasimamizi wake, pamoja na wanataaluma wa fasihi ya Kiswahili katika ngazi ya uzamivu. Hivyo, usahihi wa data katika utafiti huu, umehakikiwa kwa kutumia nadharia zilizoongoza mjadala wa data, mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data zilizotoa majibu yanayolingana.

3.8 Uchambuzi wa Data

Sehemu hii inahusu uchakataji na uchambuzi wa data za utafiti huu kama zilivyokusanywa kutoka uwandani. Uchakataji wa data ulifanyika baada ya kukusanya data zilizokusudiwa kulingana na malengo mahsusi ya utafiti. Maandalizi yalijumuisha hatua kadhaa za uchakataji wa data, yaani kunukuu, kutafsiri na kuweka katika misimbo. Katika hatua ya awali, mtafiti alichakata data kwa kunukuu nyimbo za tiba asili. Kutokana na mchakato huu, mtafiti alifanikiwa kutengeneza data iliyo katika maandishi. Data hiyo ni ya nyimbo 44 kati ya nyimbo 55 zilizokusanywa.

Hatua ya pili ni ya uhariri wa data zilizochakatwa ulifanyika kwa njia ya kulinganisha data zilizoandikwa kwa upande mmoja na data zilizorekodiwa za nyimbo toka kwenye kinasasauti. Nia ya hatua hii ni kuhakiki kuwa kilichorekodiwa na kilichoandikwa vinawiana.

Hatua ya tatu iliyofuata baada ya kunukuu na kuhariri ilikuwa ni kutafsiri baadhi ya data zilizokuwa katika lugha za Kingoni, Kiyao, Kindendeule, Kinyasa na Kibena ambazo zilitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Uzalishaji wa data katika tafsiri

ulitilia maanani ishara na misimbo ya kiutamaduni zilizodhihirika katika nyimbo za tiba asili. Jambo hili lilizingatia kwa kutumia watafsiri kutoka kwa mganga anayehusika ili kutopoteza maana ya nyimbo kwa kuzingatia utamaduni wa jamii inayohusika.

Hatua ya nne, ilikuwa ni kuweka misimbo. Mchakato huu ulijumuisha ugawanyaji data katika makundi mbalimbali kutegemea maudhui ya data. Kwa kuzingatia hayo, uwekaji misimbo ulijumuisha data za aina tatu. Kwanza, kuainisha nyimbo za tiba asili za waganga. Pili, kuchambua mtindo wa nyimbo za tiba asili; na matu, kueleza sababu za matumizi ya nyimbo katika tiba asili za waganga Mkoani Ruvuma.

Baada ya uchakataji wa data kukamilika kwa kuweka misimbo kwenye data kulingana na malengo mahsusi, mtafiti aliandaa ripoti ya utafiti. Icha ya kuwa, data za utafiti zilikusanywa kwa lugha ya Kiswahili na Kingoni, Kiyao, Kindendeule, Kinyasa na Kibena. Uchambuzi na uandaaji wa ripoti ulitumia lugha ya Kiswahili.

3.9 Itikeli ya Utafiti

Utafiti wa kitaaluma una maadili yanayopaswa kufuatwa. Maadili ya utafiti huzingatia sheria na miongozo iliyowekwa katika utaalumu fulani (Fink, 1998 na Mligo, 2012). Hali hii hujitokeza kwa kuwa watafiti hawana mtazamo na fikra za aina moja katika utendaji wa kazi zao. Huu ndio msingi wa Braud (1998) na Dornye (2007) kuona umuhimu wa kuwapo kwa miongozo na kanuni ambazo zitatumika kuwaweka watafiti katika mfanano fulani ili kujaribu kueleza jambo ambalo ni sahihi na lisilo sahihi katika mchakato wa utafiti.

Katika utafiti huu, masuala ya kiitikeli yaliyozingatiwa kikamilifu. Kwa mfano, kwanza, mtafiti anapaswa kuwauliza watafitiwa maswali yale tu yanayohusiana na mada ya utafiti ya wake, pamoja na kupata ridhaa ya watafitiwa kabla ya kuanza kufanya utafiti anaokusudia kuufanya. Kwa mujibu wa Preston (2001) na Israel na Hay (2006), ni suala linalokubalika kiutafiti kuwaliza watafitiwa maswali yatakayosaidia kupata ukweli kuhusu jambo linaloshughulikiwa. Mtafiti anapaswa kuwauliza watafitiwa maswali yatakayosaidia kupata taarifa sahihi kuhusu jambo analolishughulikia. Katika utafiti huu, mtafiti alipata ridhaa kutoka kwa watafitiwa kabla ya kuanza kufanya utafiti, pamoja na kuwauliza maswali yaliyolingana na malengo mahsusi ya utafiti uliofanyika.

Pili, mtafiti anapaswa kutathmini umuhimu wa utafiti anaokusudia kuufanya kabla ya kuanza kukusanya data za utafiti aliokusudia. Mtafiti akishindwa kuthibitisha dhima za utafiti unaokusudiwa atakuwa hajajua vema maadili ya utafiti (Brand na Anderson, 1983; Bell, 1999 na Hakim, 2000). Kipengele hiki kilizingatiwa kikamilifu katika tasnifu hii. Kabla ya kuanza kukusanya data, mtafiti alitathmini umuhimu wa utafiti kama ulivyofafanuliwa katika sura ya kwanza ya tasnifu hii.

Tatu, ni uvunjaji wa maadili pale mtafiti anapokusanya habari kutoka kwa watafitiwa bila wao kujua kwamba taarifa zinazokusanywa ni kwa ajili ya utafiti (Bogdan na Biklen, 1992 na Iphofen, 2009). Mtafiti anapaswa kuwafahamisha watafitiwa kuhusu data zinazohitajika na malengo mahsusi ya utafiti. Katika taalimu ya utafiti, mtafiti hapaswi kuwalazimisha watafitiwa wake kushiriki katika utafiti bila ridhaa yao (Charles, 1995 na Sappford na Jupp, 2006). Kufanya hivyo ni kukiuka maadili ya

utafiti. Kipengele hiki kilizingatiwa katika tasnifu hii, ambapo watafitiwa walielezwa kuhusu umuhimu wa utafiti. Hali hii iliwapa watafitiwa fursa ya kutoa taarifa kwa uhuru au hiari bila kulazimishwa.

Pia, mtafiti anapaswa kuzingatia usiri wa taarifa zilizotolewa na mtafitiwa. Kwa kawaida, yale anayoyatoa mtafitiwa huwa ni siri; na mtafiti anatakiwa kutumia taarifa hizo kulingana na malengo ya utafiti yaliyokusudiwa (Kvale, 1996 na Berg, 2009). Mtafiti hatakiwi kuweka wazi majina halisi ya watafitiwa wake isipokuwa kama wametoa ridhaa. Mtafiti ahakikishe kuwa chanzo chake cha taarifa hakiwezi kujulikana na wasomaji wake (Kothari, 2005 na Nagata, 2006). Kipengele hiki kilizingatiwa kwa kuwa watafitiwa walikuwa radhi majina yao kuorodheshwa katika ripoti ya utafiti, pamoja na kupigwa picha wakati wa kutoa taarifa zao. Kwa kufanya hivyo, data za utafiti zimetumika kwa kuzingatia malengo mahsusi na maadili ya utafiti.

Aidha, mtafiti hapaswi kuegemea upande wowote katika mchakato wa utafiti. Kufanya hivyo ni kukiuka maadili ya kazi ya utafiti. Mtafiti ahakikishe kuwa anatoa ripoti kwa usahihi kwa kuzingatia taratibu za kisayansi (Denzin na Lincoln, 2000 na Dellinger, 2005). Mtafiti akitumia njia za kisayansi, lakini akatoa ripoti isiyo sahihi kwa kuegemea upande fulani ili kutimiza matakwa fulani atakuwa amekiuka maadili ya taalimu ya utafiti (Cryer, 2000 na Oliver, 2003). Taratibu za kisayansi zilifuatwa ili kudhitibiti ubora wa taarifa zilizotolewa na watafitiwa. Mtafiti hakuegemea upande wowote wakati wa uchambuzi wa data na uandishi wa ripoti ya utafiti.

Kwa muhtasari, maadili ya utafiti yalimhusu mtafiti na mahusiano yake na watafitiwa katika mchakato wa utafiti. Jambo la kuzingatiwa katika mchakato huo ni kuhakikisha kuwa, mtafiti na watafitiwa hawaathiriwi kwa namna yoyote kiakili, kisaikolojia na kimwili kutokana na kushiriki kwao. Kwa ujumla, itikeli ya utafiti ilizingatiwa kikamilifu ili kuhakikisha utafiti unafuata misingi ya kisayansi na taalimu ya utafiti.

3.10 Hitimisho

Sura ya tatu imejadili masuala yanayohusiana na mbinu za utafiti. Dhana ya mbinu za utafiti imegusiwa kwa kujiegemeza katika kueleza tofauti za msingi zilizopo baina ya dhana hiyo na njia au zana mahsusi za ukusanyaji wa data. Njia za ukusanyaji wa data za ushuhudiaji na mahojiano zimefafanuliwa. Ufafanuzi umejiegemeza katika kueleza jinsi zilivyotumika kukusanya data za utafiti huu. Pia, njia za uwasilishaji na uchanganuzi wa data zimeelezwa. Kutokana na aina za data tumeweka wazi jinsi mkabala wa kitaamuli ulivyotumika. Data za ushuhudiaji na mahojiano zote zimetumia mbinu ya maelezo ya kinathari. Sura inayofuatayo inahusu uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti uliofanyika.

SURA YA NNE

UAINISHAJI WA NYIMBO ZA TIBA ASILI ZA WAGANGA

4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uainishaji wa nyimbo za tiba asili zilizolengwa katika utafiti. Data zimewasilishwa kwa kufuata mpangilio wa malengo mahsusi na maswali ya utafiti. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mtindo katika nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma. Sura hii imeshughulikia lengo mahsusi la kwanza lililohusu uainishaji wa nyimbo za tiba asili.

4.2 Aina za Nyimbo za Tiba Asili

Katika sehemu hii tumechaunguza swali la kwanza lilohusunyimbo za tiba asili katika jamii mkoa wa Ruvuma. Katika kujibu swali hili tumejikita kwenye data tulizozikusanya kutoka uwandani kwa njia ya mahojiano na ushuhudiaji. Data zimebainisha kwamba, nyimbo za tiba asili ambazo zinazotumiwa na waganga mkoani Ruvuma zimeainishwa katika makundi saba kulingana na muktadha wa matumizi na mahitaji yake. Uainishaji uliofanyika umewekwa wazi katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na 4. 1: Aina za Nyimbo za Tiba Asili

Aina	Wimbo	Dhima
1. Nyimbo za Maombi	<ul style="list-style-type: none"> • Tuombe • Tuombe na Malaika 	Kuomba ulinzi wa Mungu
1.1 Maombi kabla ya Tiba	Andaa Njia	Kuomba kwa kushirikiana na malaika
1.2 Wakati wa Kuchimba Dawa	Hodi Hodi Mwalimu	Kuomba kwa mizimu ifanye wepesi katika tiba.
1.3 Wakati wa Kutumia Dawa	Mababu na Malaika Mtusaidie	Kuomba ruhusa ya kuingia sehemu ya kuchimba/ kutafuta dawa
		Kuomba kwa mizimu ili dawa zimtibu mgonjwa
2. Nyimbo za Kuomboleza	Mjukuu Analia	Kuelezea mateso na maumivu ya mgonjwa
3. Nyimbo za Kufurahisha Mizimu	Tucheze Ngoma	Kuhimiza kucheza ngoma
	Furaha	Kufurahi pamoja na mizimu
4. Nyimbo za Historia	Mgelengana	kuelezea jina la dawa maarufu inayotibu magonjwa mengi
5. Nyimbo za Shukrani	Teleza	Kuishukuru miungu
6. Nyimbo za Tiba	Nole nole	Kuondoa maradhi
7. Nyimbo za Kuaga	Naluta	Kuaga baada ya kumaliza kazi

Kama inavyonekana katika Jedwali Na. 1, nyimbo za tiba asili zinaweza kugawanya katika makundi saba. Nyimbo hizo huimbwa katika matukio mbalimbali yanayoambatana na tiba, ambapo wananadharia ya Mitindo wanalita tukio hili kuwa ni la kiutendaji linalofungamana na muktadha maalumu. Kwanza, kuna nyimbo ambazo huimbwa kabla ya tiba kuanza kutolewa. Nyimbo hizi huwa na dhima ya kuita mizimu ili isogee karibu na mgonjwa kwa ajili ya kufanikisha matibabu. Pili, ni

nyimbo zinazoimbwa pale tiba inapoanza kutolewa. Hapa, nyimbo hutumika kupandisha mizimu iliyoko kwa mganga na wazumi au wasaidizi wake ili itoe maelekezo ya namna ya kumtibu mgonjwa.

Tatu, ni zile ambazo huimbwa wakati wa kwenda kuchimba dawa ili kupata maelekezo ya dawa gani ichimbwe kwa matumizi ya mgonjwa na ugonjwa upi. Nne, ni nyimbo zitolewazo wakati mgonjwa anatumia dawa. Katika hatua hii, mizimu huombwa kuifanya dawa iliyochimbwa iweze kumtibu kwa mafanikio mgonjwa anayehusika. Hatua zote hizo tumezifanua kwa kina sehemu inayofuata. Kwa jumla, lengo la kuimba nyimbo hizi ni kuihusisha na kuikabidhi mizimu na miungu shughuli zote za tiba tangu mwanzo mpaka mwisho. Kwa hiyo, kuna vipera vitatu vya nyimbo za maombi katika nyimbo za tiba asili. Nyimbo za tiba asili zimeainishwa kama zilivyofafanuliwa katika sehemu inayofuata.

4.2.1 Nyimbo za Maombi

Maombi ni dhima mojawapo ya nyimbo za tiba asili iliyobainika uwandani. Kabla ya kuanza kufafanua vipera vya nyimbo za maombi, kwanza tuangalie baadhi ya nyimbo za maombi na dhamira zake. Wimbo ufuatao unaitwa ‘*Tuombe*’ ambao umenukuliwa kama ulivyoimbwa na wazumi katika eneo la kazi la mganga mmojawapo aliyeshiriki katika utafiti huu. Wimbo unaeleza:

Kiongozi: Wee tuombe daima.
Aee daima.
Na majini wa milimani tabu sana.
Aee daima.

Wazumi: Wee tuombe daima.
Aee daima,
Na majini wa milimani tabu sana,
Aee daima.

- Kiongozi: Tuimbe wote daima aee, baba,
na majini wa milimani tabu leo,
Aee daima.
- Wazumi: Tuimbe wote daima aee, baba,
na majini wa milimani tabu leo,
Aee daima.
- Kiongozi: Ena ena daima,
Aee daima,
Na majini ya milimani tabu sana.
- Wazumi: Tuimbe wote daima aee, baba,
Na majini wa milimani tabu leo,
Aee daima.
- Kiongozi: Tuombe na mababu,
Aee daima,
Na majini ya milimani tabu sana.
- Wazumi: Tuombe na mababu,
Aee daima,
Na majini ya milimani tabu sana.
- Chanzo:** Uwandani (2017).

Dhamira kuu ya wimbo huu ni maombi. Waimbaji wanasisitiza kuomba daima.

Katika wimbo huu, waimbaji wanasisitiza kuomba dhidi ya majini wa milimani. Wanasema:

Wee tuombe daima,
Aee daima,
Na majini wa milimani tabu sana.

Uombaji wa daima maana yake ni kuomba bila kukoma wakati wote. Sababu ya kuomba bila kukoma inaoneshwa katika mshororo wa mwisho unaosema, ‘Majini wa milimani tabu sana’. Hivyo, waimbaji wanaonesha kuwa majini wa milimani sio ‘viumbe’ wazuri. Hivyo, binadamu wanasisitizwa kuomba daima. Katika utafiti huu imebainika kwamba, kuna majini wazuri na mabaya, ingawa mara nyingi majini

yanafikiriwa kuwa ni viumbe wanaodhuru tu. Uzuri na ubaya wa majini unaoneshwa kupitia nyimbo zinavyowapambanua.

Dhamira nyingine inayooneshwa katika wimbo huo inahusu nguvu inayokana na kuimba. Katika utafiti huu, tumegundua kuwa, nyimbo zina nguvu mbalimbali na hutumika katika shughuli zote za tiba. Hivyo, kuimba kunawasogeza karibu mizimu na miungu ambayo waimbaji wanaamini inawasaidia katika mambo mbalimbali. Katika kuomba, binadamu wanaimba na kupitisha maombi yao kwa mababu waliotangulia ili wafikishe maombi kwa mizimu na miungu.

Katika falsafa ya Kiafrika Mungu yupo katika darajia zinazotokana na kufariki kwa watu. Aliyefariki zamani yupo karibu zaidi na miungu tofauti na aliyefariki siku za karibuni (Mbiti, 1969). Katika kuimba wanawataja baba na mababu. Wanasema:

...Tuimbe wote daima aee, baba ...
...Tuombe na mababu...

Hapo, waimbaji wanasisitiza katika nguvu ya kuimba, inaaminika kuwa baba na mababu huwasaidia katika maombi yanayofanyika. Ufuatao ni wimbo mwingine wa maombi unaoitwa '*Tuombe na Malaika*'. Katika wimbo huu, waimbaji wanasisitiza kuomba kwa kuwashirikisha malaika ambao kiimani wapo jirani zaidi na Mungu ili wawasaidie.

Mganga: Tuombe tuombe tuombe na malaika,
Mganga + Wazumi: Tuombe tuombe tuombe watusaidie,
Mganga + Wazumi: Tuombe tuombe tuombe na malaika,
Mganga + Wazumi: Tuombe tuombe tuombe majini yote.

Chanzo: Uwandani (2017).

Dhamira kuu ya wimbo huu ni maombi. Waimbaji wanaomba malaika wawasaidie katika maombi yao. Malaika ni kiumbe asiyeonekana ambaye ameumbwa na Mungu.

Pia, majini yametajwa katika maombi haya. Katika wimbo huu, majini wanaombwa yasaide katika maombi. Hapa inaonesha majini si mabaya, bali wanasaidia katika maombi. Kwa ujumla, tunaona kwamba, maombi yanayofanyika kwa njia ya kuimba yanasawiri imani ya jamii inayohusika. Maombi kwa miungu na mizimu huwasilishwa kwa kutumia wawakilishi kama vile mababu, malaika na hata viumbe vingine visivyoonekana. Katika utafiti huu, tumebaini kwamba, nyimbo za maombi zina vipera mbalimbali kama ilivyoelezwa katika sehemu hii.

4.2.1.1 Nyimbo za Maombi kabla ya Tiba

Mganga pamoja na wagonjwa wake huimba kabla tendo la tiba halijaanza. Uimbaji kabla ya kutibu hufanyika kwa lengo la kuiomba mizimu iweze kusaidia ili tendo la kutibu liweze kufanyika na litekelezeke kwa ufanisi kwa kutumia nguvu za mizimu. Kuna wakati ambapo miungu na mizimu huombwa kwa kutajwa majina. Mganga na waimbaji hutegemea nguvu, ulinzi na uwezo wa miungu katika kukamilisha tiba. Moja ya wimbo ambao huimbwa kabla ya kuanza tiba ni huu uitwao '*Andaa njia*' kama ulivyoimbwa:

Mganga: Babu tengeneza njia,
Tupite salama x3.

Wazumi: Babu tengeneza njia,
Tupite salama x3.

Mganga: Babu tengeneza njia,
Tupite salama x3.

Wazumi: Babu tengeneza njia,
Tupite salama x3.

Chanzo: Uwandani (2017).

Dhamira kuu ni maombi kwa mizimu kabla ya kuanza tiba. Katika dhamira hiyo, waimbaji wakiongozwa na mganga wanaomba babu atengeneze njia ili wapite salama. Kwa kwa mujibu wa msimbo wa kiseme katika nadharia ya Simiotiki, neno ‘Babu’ ni taswira iliyobeba maana. ‘Babu’ ni taswira inayowakilisha mizimu iliyo karibu na miungu. Mfano, katika matambiko mbalimbali ya kijadi waombaji hutoa maombi yao kwa mizimu na miungu yao kupitia kwa mababu kama wimbo unavyoonesha katika mshororo wa kwanza na wa pili:

Babu tengeneza njia...
Tupite salama...

Hapa, babu anaombwa atengeneze njia ili wapite salama. Utengenezaji wa njia unaozungumziwa na waimbaji ni wa kitaswira. Njia inamaanisha kuwa, mizimu ioneshe kila kinachotakiwa kuoneshwa katika tiba. Kwa mfano, mizimu ionesho dawa na aina za magonjwa na kitu chochote kitakachojitokeza katika tiba. Linaweza kutokea tatizo ambalo litakwamisha tiba isikamilike. Hivyo, mizimu inaombwa ifanye mambo yaende vizuri.

Maombi ya tiba asili kwa kuimba hayana tofauti na maombi ya dini za kisasa, kwani maombi mbalimbali hufanyika kabla ya shughuli fulani kuanza. Maombi katika dini za kisasa hufanyika kabla ya kuamka asubuhi, kabla ya kuanza kula chakula na kabla ya kufanya matendo kadha wa kadha. Hivyo, uimbaji kabla ya kuanza tiba hauna tofauti na maombi yanayofanywa na dini za kisasa kabla ya kuanza shughuli yoyote muhimu.

4.2.1.2 Nyimbo za Wakati wa Kuchimba Dawa

Kabla ya kwenda kuchimba dawa, kuna maombi hufanyika ambayo yanamsaidia mganga kuweza kupata dawa zitamsaidia katika kutibu wagonjwa. Mizimu hupenda nyimbo. Hivyo, kabla ya uchimbaji dawa haujafanyika, nyimbo huimbwa. Huimbwa kabla ya kwenda porini kuchimba dawa. Zipo ambazo huimbwa wakati wa tendo la kuchimba dawa. Si dawa zote hupatikana kwa urahisi. Kuna dawa ambazo huchimbwa katika mapango. Kabla mchimbaji hajaingia katika pango, huimba nyimbo na kupiga hodi katika pango ili kuomba mizimu ioneshe dawa. Inaaminika kuwa, bila hufanya hivyo, unaweza kuingia katika pango na ukashindwa kuziona dawa kwani mizimu inaweza ikazificha. Wakati mwingine mhusika anaweza kupotelea ndani ya pango. Huu ndio msingi wa nadharia ya Mitindo kuangalia tukio la kiutendaji kulingana na muktadha unaonesha jinsi mtindo ulivyosaidia kuibua aina ya nyimbo.

Edrtsieck (2001) baada ya kufanya utafiti mkoani Songwe kwa mganga mmojawapo wa katika sehemu aliyoilengaalibaini kuwa, ili akachimbe dawa shurti aimbiwe nyimbo, ndipo hupandwa na pepo. Pepo huyo humuongoza aende porini akiwa amepagawa. Akiwa porini, huchimba dawa akiwa katika hali ya kupagawa na kurejea kwenye hali yake ya kawaida baada ya kumaliza kazi hiyo. Ufuatao ni wimbo unaoitwa '*Hodi Hodi Mwalimu*' wa kuingilia katika eneo la kuchimba dawa kama ulivyoimbwa:

Kiongozi:	Hodi hodi mwalimu ee, Hodi hodi mwalimu, Tumetoka Kilimanjaro x3.
Wazumi:	Hodi hodi mwalimu ee, Hodi hodi mwalimu, Tumetoka Kilimanjaro x3.

Kiongozi: Naingia mwalimu x3,
Nimetoka Kilimanjaro,
Hodi mwalimu.
Wazumi: Hodi hodi mwalimu ee,
Hodi hodi mwalimu,
Tumetoka Kilimanjaro x3.
Chanzo: Uwandani (2017).

Dhamira kuu ya wimbo huu ni kubisha hodi. Waimbaji wanaimba wakiwa na lengo la kukaribishwa na ‘Mwalimu’. Katika Simiotiki ya kiseme neno ‘Mwalimu’ ni taswira, ikimaanisha mwenye mamlaka zaidi. Hivyo, wanaomba ili mwenye mamlaka awakaribishe na kuwapokea. Vilevile, jina ‘Kilimanjaro’ ni lugha ya picha linalotumika mwalimu ametoka mbali. Haimaanishi mkoani Kilimanjaro au katika mlima Kilimanjaro. Halikadhalika, waimbaji wanaonesha kuingia; wanasema: ‘... Naingia mwalimu ...’. Hapa ndipo mchimba dawa anapoingia katika pango au sehemu ya kuchimba dawa. Lugha ya picha ni moja ya mtindo katika matumizi ya lugha katika kazi za kifasihi.

4.2.1.3 Nyimbo za Wakati wa Kutumia Dawa

Nyimbo zina nguvu yake katika tiba na dawa zina nafasi yake katika tiba. Hivyo, katika tiba asili, nyimbo hutumika pia wakati wa kutumia dawa. Dawa hizi hutolewa na mganga kwa nguvu na maono ya mizimu. Katika kuzifanya dawa zifanye kazi vizuri, kuna nyimbo maalumu ambazo huimbwa zikilenga kukaribisha mizimu iweze kuzipa baraka na nguvu dawa hizi ili ziweze kuwaponya wagonjwa. Moja ya nyimbo hizo ni huu unaoitwa ‘*Mababu na Malaika Mtusaidie*’. Unaeleza:

Mganga:	Mababu na Malaika kwa uwezo wenu baba mtusaidie,	} × 5
Wazumi:	Mababu na malaika kwa uwezo wenu baba mtusaidie,	
Mganga:	Maombi kwa malaika x 3, Maombi yetu wote x2,	
Wazumi:	Maombi kwa malaika x 3, Maombi yetu wote x 2,	
Mganga:	Maombi eee maombi eee x2,	
Wazumi:	Maombi eee maombi eee x2,	
Mganga:	Maombi yetu wote, Maombi eee x2,	
Wazumi:	Maombi yetu wote, Maombi eee x 2.	

Chanzo: Uwandani (2017).

Dhamira zinazojipambanua katika wimbo huu ni maombi kwa mababu na malaika ili dawa zimfae mgonjwa. Wimbo huu huimbwa pale wagonjwa wanapotumia dawa baada ya matatizo yao kugunduliwa. Waimbaji wanaamini kuwa, mababu na malaika watawasaidia baada ya kutumia dawa hizo kwa njia ya maombi na kuimba.

4.2.2 Nyimbo za Kuomboleza

Tukio la kiutendaji kama linavyobainishwa katika nadharia ya Mitindo lina nafasi kubwa katika uainishaji wa nyimbo za tiba asili. Kazi za nyimbo zinaambatana na muktadha maalumu. Hii inatubainishia aina nyingine ya nyimbo za tiba asili zinazohusu kuomboleza. Kuomboleza ni kulia kwa kusema maneno au kuimba nyimbo za masikitiko au uchungu (TUKI, 2010). Mulokozi (2017) anaeleza kuwa nyimbo hizi zinaitwa mbolezi au maombolezo. Anaeleza kuwa, hizi ni nyimbo za kilio na hutumika kutumbuiza kwa dhima yake. Utafiti huu umegundua kuwa, nyimbo hizo pia hutumika katika tiba asili. Katika tiba asili, nyimbo hizi huimbwa wakati ambao mgonjwa anakuwa katika mateso makali kutokana na magonjwa.

Hivyo, wimbo wa kuomboleza huimbwa ili kuiomba mizimu iweze kuondoa maumivu na mateso hayo kwa mgonjwa. Wimbo wa ‘*Mjukuu Analia*’ ni mfano wa wimbo wa kuomboleza:

Mganga:	Mjukuu aee, Mjukuu analia aee,
Wazumi:	Mjukuu aee, Mjukuu analia aee.
Mganga:	Mjukuu aeee, Baba mjukuu analia aee,
Wazumi:	Mjukuu aeee, Baba mjukuu analia aee.
Mganga:	Tukachimbie dawa, Mjukuu aee, Mjukuu analia aee.
Wazumi:	Mjukuu aee. Mjukuu analia aee. Chanzo: Uwandani (2017).

Dhamira ya wimbo huu ni kuonesha kilio cha mjukuu. Unabainisha mateso na maumivu ya mgonjwa yanayomfanya alie. Mganga na wazumi wanaimba wimbo huu wakiwa katika hali ya majonzi na baadhi yao machozi huwatoka. Wimbo huu unatoa taarifa kwa mizimu kuwa mgonjwa kazidiwa; na wanaomba mizimu isaidie kuonesha dawa zitakazomponya mgonjwa. Baadhi ya mishororo inasema, ‘Baba mjukuu analia... Tukachimbie dawa...’

4.2.3 Nyimbo za Kufurahisha Mizimu

Hizi huwa ni nyimbo za furaha ambapo waimbaji huimba baada ya kukamilisha shughuli ya tiba. Nyimbo hizi huambatana na furaha ya kufurahisha mizimu, kwa kuwa, tendo la tiba asili hutendeka kwa kushirikisha mizimu. Utafiti huu umebaini

jinsi muktadha wa kiutendaji ulivyoweka bayana aina ya nyimbo ziznzohusika. Katika uwekaji bayana, imebainika kwamba, katika ukamilishaji wa tiba asili hakuna hatua itakayofanyika bila kushirikisha mizimu, vinginevyo mganga hawezi kufanikiwa. Bila maombi mgonjwa hawezi kupona; na maombi hufanywa katika hatua zote za kutoa tiba, kuanzia kumpokea mgonjwa. Hata hatua ya utafutaji dawa na utumiaji huhusisha pia maombi na kuimba. Hivyo, yote hayo yakikamilika kwa ufasaha, nyimbo za kuifurahisha mizimu huimbwa. Mmojawapo wa wimbo wa kuifurahisha mizimu ni huu wa *'Tucheze Ngoma'*:

Kiongozi: Twendeni jamani eee x2,
Twendeni jamani tucheze ngoma eee x 2.

Wazumi: Twendeni jamani eee x2,
Twendeni jamani tucheze ngoma eee x 2.
Chanzo: Uwandani (2017).

Muktadha wa kiutendaji wa wimbo huu kama unavyobainishwa na nadharia ya Mitindo umeambatana na furaha, kwani watu hucheza ngoma na kufurahi kwa tiba iliyopatikana baada ya wagonjwa kupona. Huu ni ushindi kwa mgonjwa, mganga na ndugu wa mgonjwa ambao wanakuwa wamehangaika na mgonjwa kwa muda mrefu, hatimaye amepona. Hivyo, mizimu hupewa sifa kwa kushangiliwa. Wimbo mwingine wa kuifurahisha mizimu unaitwa *'Furaha'*:

Kiongozi: Furaha furaha furaha ee,
Furaha furaha furaha leo x 2.

Wazumi: Furaha furaha furaha ee,
Furaha furaha furaha leo x 2.

Kiongozi: Furaha furaha furaha eeh,
Furaha furaha furaha ya majini.

Wazumi: Furaha furaha furaha eee,
Furaha furaha furaha eee.

Kiongozi: Ushindi ushindi ushindi ee,
Ushindi, ushindi, ushindi ee.

Wazumi: Furaha, furaha, furaha ee,
Furaha, furaha, furaha ee.
Chanzo: Uwandani (2017).

4.2.4 Nyimbo za Historia

Jamii yoyote haikosi kuwa na historia ya maendeleo yake katika nyanja zoe za kijamii. Mambo yanayotambulisha katika jamii mbalimbali yana historia yake. Jamii ina historia yake, utamaduni wake, falsafa zake, uchumi na siasa zake. Pia, kila ukoo una historia na mambo yake. Tiba asili nayo ina historia na maendeleo yake. Nyimbo za historia zipo katika jamii mbalimbali na hubeba mambo mbalimbali. Kwa mfano, kuna nyimbo za historia ya nchi. Hivyo, nyimbo za historia ni muhimu katika jamii yoyote duniani. Katika nyimbo za tiba asili wimbo mmojawapo uliobeba historia ni huu wa *'Mgelengana'*. Wimbo huu unazungumzia dawa ya tiba asili inayoitwa *mgelengana*. Hii ni dawa nzuri na yenye uwezo wa kutibu magonjwa mengi ya binadamu na hata ya wanyama.

Hivyo, jamii imetunga wimbo wa kuhifadhi mmea huo. Kwa mujibu wa nadharia ya Mitindo kitu jambo hilo linabainishwa kuwa mfanyiko wa kimawasiliano kulingana na utamaduni. Hivyo, nadharia hii inaonesha umuhimu wa kulithishana historia kwa njia mbalimbali kulingana na utamaduni wa jamii inayohusika. Baadhi ya maneno katika wimbo huo huimbwa *'Mgelengana' dawa toka zamani dawa*". Kwa kutumia wimbo huo, dawa hiyo itaendelea kukumbukwa toka kizazi kimoja hadi kingine. Wimbo huo huimbwa kama ifuatavyo:

Kiongozi: *Mgelengana* aae dawa x2,
Toka zamani aee dawa x1,
Tukachimbe dawa,
Sisi ni wagonjwa,
Mgelengana x 2.

Wazumi: *Mgelengana* aae dawa x2,
Toka zamani aee dawa x1,
Tukachimbe dawa,
Sisi ni wagonjwa,
Mgelengana x2.

Kiongozi: Baba wote dawa,
Mgelengana baba,
Mama eee dawa x3.

Wazumi: Baba wote dawa,
Mgelengana baba,
Mama eee dawa x3,
Chanzo: Uwandani (2017).

4.2.5 Nyimbo za Shukrani

Katika jamii za Kiafrika kushukuru ni jambo ambalo jamii zimerithwa kutoka kwa wahenga. Kutoa shukrani ni jambo jema na la kawaida tunalofanyiwa na mtu au watu wengine. Shukrani pia hutolewa kwa Mungu na miungu kulingana na imani ya mtu anayehusika. Katika fasihi kuna nyimbo za shukrani ambazo jamii huimba kwa kushukuru au kupongeza jambo lililotendwa na mtu au watu fulani.

Nadharia ya Mitindo inabainisha mfanyiko wa kimawasiliano kulingana na utamaduni wa jamii inayohusika. Kutoa shukrani ni njia mojawapo ya wanajamii kuwasiliana. Katika tiba asili kuna namna mbalimbali za kuwasiliana na miungu na kutoa shukrani. Moja ya njia hizo ni kutumia nyimbo. Katika nyimbo za tiba asili kuna nyimbo za shukrani. Nyimbo hizi hutumika kuishukuru mizimu kwa kila kitu ilichofanya katika tiba, kuanzia pale mgonjwa alipooneshwa mahali pa kazi pa

mganga, hadi namna mizimu ilivyotumika kumlinda mgonjwa, mganga na eneo zima la kufanyia uganga. Pia, shukrani hutolewa kwa mizimu kwa kuonesha dawa kwa mganga. Mmojawapo wa nyimbo za shukrani ni huu unaoitwa ‘Teleza’:

Mganga: Tuleza teleza wee,
Majini yote teleza wee,

Wazumi: Tuleza teleza wee,
Majini yote teleza wee.

Mganga: Teleze majini yote,
Teleza wa milima,
Teleza wa mabonde.

Wazumi: Teleze majini yote,
Teleza wa milima,
Teleza wa mabonde.

Mganga: Tunakuomba,
Teleza weee teleza.

Wazumi: Tunakuomba,
Teleza weee teleza.

Chanzo: Uwandani (2017).

Katika wimbo huu dhamira ni kuyashukuru majini ya sehemu mbalimbali kama baadhi ya mishororo ya wimbo inavyoonesha, ‘Majini yote teleza wa milima... teleza wa mabonde...’. Ikumbukwe kwamba, kuna majini mazuri na mabaya. Katika wimbo huu majini mazuri ndio yanayopewa shukrani kwa kazi nzuri yaliyoifanya kwa kuwawezesha waganga kutibu wagonjwa kwa mafanikio.

4.2.6 Nyimbo za Kutolea Tiba

Nyimbo za tiba ni jumla ya nyimbo zote ambazo zinatumiwa kukamilisha tendo la tiba. Nyimbo za hizi zinaimbwa wakati maalumu, hasa tiba inatolewa. Nyimbo hizi huimbwa kwa lengo la kusisitiza matumizi ya dawa na kuomba dawa. Katika uimbaji

wa nyimbo hizi, fanani na hadhira hushirikiana kwa namna mbalimbali. Katika nadharia ya Mitindo ushirikiano huo huitwa utengamano wa fanani na hadhira unaonesha jinsi ushirikiano wao unavyofanikisha kazi ya fasihi kukamilika. Nyimbo hizo ni nyingi, mfano mmoja wa nyimbo hizo ni wimbo huu unaoitwa ‘*Nole Nole*’:

Mganga: *Nole nole,*
Aee! Nole nole,
Nole nole aee,
 Jini wa milima,
 Fukuza homa.

Wazumi: *Nole nole,*
Aee! Nole nole,
Nole nole aee,
 Jini wa milima,
 Fukuza homa.

Mganga: *Nole nole,*
Aee! Nole nole,
Nole nole aee,
 Jini wa milima,
 Fukuza homa.

Wazumi: *Nole nole,*
Aee! Nole nole,
Nole nole aee,
 Jini wa milima,
 Fukuza homa.

Mganga: *Aee! Nole nole,*
Nole nole aee,
 Jini wa bahari,
 Punguza homa.

Wazumi: *Aee! Nole nole,*
Nole nole aee,
 Jini wa bahari,
 Punguza homa.

Chanzo: Uwandani (2017).

Wimbo huu umetumia lugha mbili yaani Kiswahili na Kimatengo. Neno ‘*nole*’ maana yake nione. Wimbo huu unaonesha dhamira ya kuondoa maradhi. Waimbaji

katika wimbo huu wanaomba jini asaidie kufukuza na kupunguza homa kwa wagonjwa. Wimbo huu huimbwa wakati tendo la tiba likiwa linafanyika. Baadhi ya mishororo inayoonesha dhamira hiyo ni, ‘jini wa milima, fukuza homa, jini wa bahari, punguza homa ...’

4.2.7 Nyimbo za Kuaga

Baada ya kuimba na kukamilika kwa tendo la tiba zilizoambatana na uimbaji wa nyimbo maalumu za tendo linalohusika katika tiba. Mwishoni, kuna nyimbo za kuaga. Nyimbo hizi hutumika kuaga mizimu na miungu yote iliyosaidia kutoa tiba na kuwalinda wagonjwa na waganga. Mfano ufuatao ni wimbo ulioimbwa kwa lugha ya Kindendeule unaojulikana kwa jina la ‘*Naluta*’:

Kiongozi: *Unene naluta* (Sasa ninaondoka),
 Wazumi: *Ndegelela* (Karibu tena).
Chanzo: Uwandani (2017)

Wimbo huu ni mfupi kwa kuangalia mishororo yake, lakini katika kuimba huchukua wakaa mrefu kwa kuwa kunakuwa na uradidi wa mishororo. Uradidi katika fasihi simulizi ni mtindo wa kawaida ambao hutumika sana katika nyimbo na hata katika ngano. Pia, nafsi iliyotumika ni nafsi ya kwanza. Nafsi hiyo imetumika kwa sababu anayeimba ni mganga, lakini anayeondoka ni mzimu ulikuwa upo ndani ya mganga. Hapo unakuwa umemaliza kazi yake, huaga na kuondoka.

4.3 Hitimisho

Katika sura hii ya nne tumechaunguza suala la uainishaji wa nyimbo za tiba asili katika jamii za mkoa wa Ruvuma. Uchunguzi umejikita kwenye data tulizozikusanya kutoka uwandani kwa njia ya mahojiano na ushuhudiaji. Data zinabainisha kwamba,

nyimbo za tiba asili ambazo zinazotumiwa na waganga wa mkoani Ruvuma zimeweza kuianishwa katika makundi saba ya nyimbo zinazoimbwa kutegemeana na muktadha wa uimbaji wake. Sura ya tano inayofuata inahusu mtindo katika Nyimbo za tiba asili za Waganga wa jamii za mkoani Ruvuma nchini Tanzania.

SURA YA TANO

MTINDO KATIKA NYIMBO ZA TIBA ASILI ZA WAGANGA

5.1 Utangulizi

Katika kuchunguza mtindo ambao nyimbo za tiba asili hutumia, utafiti huu ulichambua vipengele tofauti tofauti ili kubaini mtindo uliotumika katika nyimbo teule. Mitindo iliyotumika katika utafiti huu imebainishwa kaika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na 4. 2: Vipengele vya Mtindo

	Mtindo	Maelezo ya Mtindo	Wimbo
1	Mtindo wa Matumizi ya Lugha katika Nyimbo	Mtindo wa matumizi ya lugha ya kawaida Mtindo wa matumizi ya lugha ya kisanaa <ul style="list-style-type: none"> • Mtindo wa Uchanganya msimbo • Mtindo wa Lugha ya picha • Mtindo wa Uradidi 	i. Mababu na malaika ii. Tucheze ngoma <i>i. Ningalonga Ndauli</i> <i>ii. Gwala Maganza</i>
2	Mtindo wa Nyimbo Kutokana na Urefu	i. mtindo wa urefu kwa idadi ya maneno ii. mtindo wa urefu kwa kigezo cha wakaa iii. mtindo wa urefu kwa kigezo cha beti	i. Nipe dawa ii. Hodihodi mwalimu iii. <i>Naluta</i> iv. <i>Niyaule</i>
3	Mtindo wa Mishororo	i. Idadi ya mishororo na vipande	i. Kalima
4	Mtindo wa Fomula	i. Mpangilio wa ala za muziki na vionjo vingine ii. Kuimba kwa kupokezana	i. Nipe udi
7	Mtindo wa Daiolojia	i. Mganga na Wazumi ii. Msaidizi na Wazumi	i. Tunakuomba Baba ii. Kalima
9	Mtindo wa Viunganishi	i. Kukosa viunganishi ii. Viunganishi vichache	i. Mizimu ii. Nipe Dawa Nzuri
10	Mtindo wa Vina na Mizani	i. Vina vya mwisho ii. Vina vya kati na mwisho	i. Nipe Udi ii. Ningalonga Ndauli
11	Mtindo wa Uchezaji	i. Uchezaji unaombatana na	i. Mjukuu analia

	Mtindo	Maelezo ya Mtindo	Wimbo
		ishara ii. Uchezaji wa kujiviringisha iii. Uchezaji wa kuzungusha shingo iv. Uchezaji wa kutoa mikono v. Uchezaji wa kurukaruka kwa makalio vi. Kudondoka na kupoteza fahamu vii. Kucheza kwa kuweka mikono kichwani viii. Kucheza kasi na kupagawa	ii. <i>Nole nole</i> iii. Nipe udi iv. Furaha v. Tuombe daima vi. Ubaya vii. Mganga uko wapi? viii. Ningalonga Ndauli
12	Mtindo wa Utendaji wa Kimuziki	i. Mtindo wa Muziki wa ala ii. Mtindo wa muziki wa sauti za waimbaji iii. Sauti za waimbaji kama kipengele cha mtindo	i. Matumizi ya ala za muziki ii. Chonde, sina wema
13	Mtindo wa Maleba na Vifaa	i. Mtindo wa mavazi kulinga na makundi ii. Mtindo wa vifaa vya uimbaji	
14	Muktadha wa Mahali kama Kipengele cha Mtindo	i. Jukwaa ii. Muda wa tendo kutendwa	

Katika sehemu hii, lengo ni kujibu swali la pili la utafiti linalouliza, ni mtindo gani hutumika katika nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma? Katika kujibu swali hili data kutoka uwandani kwa njia ya ushuhudiaji na mahojiano zimewasilishwa na kujadiliwa.

5.2 Mtindo wa Lugha katika Nyimbo za Tiba Asili

Mjadala umekitwa kwa upana katika kuelezea dhana ya mtindo kwa namna tofauti na ilivyo zoeleka. Kimapokeo, mtindo ni upekee wa msanii katika kuiwasilisha kazi ya fasihi. Mtindo ni tabia ya pekee ya mtunzi au uandishi na huhitilafiana kati ya mtunzi na mtunzi (Kahigi na Mulokozi, 1979). Fasili hiyo ni sawa na ile ya Senkoro

(2011) anayefasili mtindo kuwa ni upekee katika kazi za fasihi. Mtindo hujidhihirisha katika matumizi ya lugha, akiwa na maana ya uteuzi wa maneno, upangaji, mpangilio wa sauti za lugha na matumizi ya tamathali (Mulokozi, 2017).

Kwa muktadha wa utafiti huu, msingi wa nadharia ya Mitindo umezingatiwa katika uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo. Mihimili wa uchambuzi wa lugha na ule wa uchambuzi wa vizaida lugha imetumika katika uchambuzi wa data katika sura hii. Nadharia ya Simiotiki imetumika katika kufafanua maana za ishara mbalimbali zilizotumika katika uchambuzi wa data zilizowasilishwa. Kwa hiyo, uchambuzi umejikita kwenye vipengele mbalimbali vya mtindo vinavyojitokeza katika nyimbo za tiba asili na kulifanya tendo la uimbaji kukamilika na kufikia malengo yaliyokusudiwa na watendaji. Matendo hayo yametumika kuonesha dhana ya mtindo kwa upana wake.

Hivyo, katika sehemu hii, mtindo unajadiliwa kama dhana pana kwa kuangalia mfumo mzima wa uimbaji wa nyimbo za tiba asili, uchezaji na matumizi ya vifaa na mbinu zote zinatumika katika kuwasilisha nyimbo za tiba asili za mkoani Ruvuma. Kwanza, tunaanza na uchambuzi wa mtindo wa lugha unavyojipambanua katika nyimbo za tiba asili mkoani Ruvuma. Katika kufafanua mtindo wa nyimbo, sehemu hii imewasilisha data zinazodhihirisha mitindo mikuu sita ya nyimbo za tiba asili. Kila aina kuu ya mtindo, inadhihirisha tofauti ndogo ndogo zinajadiliwa katika kila mtindo mkuu.

Katika utafiti huu, kuna matumizi ya lugha ya kawaida na lugha ya kisanaa katika nyimbo za tiba asili. Wataalamu mbalimbali wa fasihi (Abedi, 1953; Finnegan, 1977;

Mulokozi, 1986) wanaunga mkono kwa maelezo kwamba, ushairi simulizi hutumia lugha ya kisanaa na isiyo ya kisanaa. Huu ni mtazamo ambao umeendelezwa pia na wataalamu wa nyakati za karibuni kama vile Mayoka (1993) na Wamitila (2004). Katika utafiti huu, aina hizo mbili zinafafanuliwa katika vipengele vifuatavyo:

5.2.1 Matumizi ya Lugha ya Kawaida

Lugha ya kawaida katika utafiti huu hurejelea lugha isiyotumia mbinu za kisanaa. Matumizi ya lugha ya kawaida yamejidhihirika katika nyimbo mbalimbali. Matumizi ya lugha ya kawaida yanatokana na fanani ambaye hutunga wimbo unaohusika kwa kuiangalia hadhira yake pamoja na kusudio lake. Pia, matumizi ya lugha ya kawaida yanaangalia muktadha wa utendaji wa tendo lenyewe na hadhira inayoshiriki katika tendo hilo la uimbaji. Nadharia ya Mitindo inafafanua kwamba, matumizi ya lugha hufungwa na muktadha. Hali hiyo imebainika pia katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili zilizochunguzwa katika utafiti huu. Ikumbukwe kwamba, nyimbo hizi huhifadhiwa kichwani na huwasilishwa mbele ya hadhira kwa wakati na namna tofauti kulingana na mahitaji yanayofungamana na muktadha wa kiutendaji. Kwa hiyo, wimbo unaweza kubadilika kulingana na mahitaji. Hiyo ni sifa muhimu ya fasihi simulizi. Kwa mfano, wimbo wa *'Mababu na Malaika Mtusaidie'* unaonesha matumizi ya lugha ya kawaida:

Mganga:	Mababu na Malaika kwa uwezo wenu baba mtusaidie,	} × 5
Wasaidizi:	Mababu na malaika kwa uwezo wenu baba mtusaidie,	
Mganga:	Maombi kwa malaika x3, Maombi yetu wote x2,	
Wasaidizi:	Maombi kwa malaika x3, Maombi yetu wote x 2.	
Mganga:	Maombi eee maombi eee x2,	
Wasaidizi:	Maombi eee maombi eee x2.	

Mganga: Maombi yetu wote,
 Maombi eee x2,
 Wasaidizi: Maombi yetu wote,
 Maombi eee x 2.
Chanzo: Uwandani (2017).

Huu ni wimbo uliotumia lugha ya kawaida, ikiwa na maana kwamba, hakuna lugha ya picha, taswira wala tamathali za semi. Matumizi ya lugha ya kawaida yanajidhirisha kwenye jina la wimbo na katika maneno mengine yaliyomo katika wimbo wenyewe. Neno ‘Mababu’ limetokana na jina babu na ‘Malaika’ linabaki kama malaika. Katika imani za Kiafrika kuna miungu na miungu. Mgawanyiko unajidhirisha katika sehemu tatu. Kwanza, ni ya watu waliokufa siku za karibuni. Hao ndio mababu. Pili, waliokufa siku nyingi. Hao ndio malaika; na wapo waliokufa zamani zaidi hao ndio wapo karibu na Mungu. Hivyo, maneno ‘Mababu’ na ‘Malaika’ ni majina ya kawaida yanayotumika katika imani za kijadi, hasa katika shughuli za uganga na matambiko. Pia, katika mishororo ya wimbo huo lugha iliyotumika ni ya kawaida kama inavyodhihirika katika baadhi ya mishororo:

Mababu na malaika kwa uwezo wenu baba mtusaidie,
 Maombi kwa malaika,
 Maombi yetu wote.
Chanzo: Uwandani, (2017).

Kama tulivyoeleza awali kuwa, mishororo hii inawakilisha mishororo mingine katika kuonesha jinsi wimbo huo ulivyotumia lugha ya kawaida. Matumizi ya lugha ya kawaida huufanya wimbo kuimbika kwa urahisi, hasa kwa wazumi wageni na watoto ambao lugha ya kawaida inawafanya wajifunze namna ya kuimba wimbo huo kwa urahisi. Kwa mujibu wa nadharia ya Mitindo, matumizi haya ya lugha ni

sehemu ya mtindo ambao unatokana na utangamano wa fanani na hadhira inayohusika.

Lugha ya kawaida husababishwa na utunzi wa papo kwa papo wa nyimbo za tiba asili. Mganga au fanani wa kuimbisha anaweza kutongoa wimbo papo kwa papo. Utongoaji huo humfanya atumie lugha ya kawaida kutokana na hadhira waliomzunguka. Kama ilivyo fasihi simulizi, moja ya uhai wake ni kubadilika kulingana na mazingira. Hali hii hutokana na utashi wa mtunzi mwenyewe baada ya kuona mahitaji ya hadhira yake kwa wakati huo. Katika nyimbo za tiba asili fanani huweza kutunga kwa kuangalia mahitaji ya hadhira yake. Hivyo, katika utongoaji wa nyimbo hizi lugha ya kawaida hutumika. Ufuatao ni wimbo uliotungwa papo kwa papo uitwao *'Tucheze Ngoma'*:

Kiongozi: Twendeni jamani eee x 2,
Twendeni jamani tucheze ngoma eee x2.

Wazumi: Twendeni jamani eee x 2,
Twendeni jamani tucheze ngoma eee x2.
Chanzo: Uwandani (2017).

Wimbo huu ulitongolewa mbele ya mtafiti na wazumi walishiriki kuuimba kwa kufuata maneno ya fanani. Sababu ya kutongolewa wimbo huu, ilikuwa baada ya wagonjwa wengi kudondoka chini na kugalagala baada ya kupandwa na pepo. Mganga alianza kuimba wimbo ambao mwanzo waitikiaji walikuwa wanababaika kuitikia. Baada ya kumaliza tiba tulifanya mahojiano na mganga kuhusu hali hiyo. Alisema sababu ya waitikiaji kubabaika ni kwamba, wimbo huo ulitungwa pale pale jukwaani.

Sababu nyingine ya matumizi ya lugha ya kawaida katika nyimbo za tiba asili ni muktadha wa kihistoria. Katika utafiti huu, tumebaini kwamba, kuna nyimbo ambazo zinatumika kuelezea historia ya dawa ambazo hutibu maradhi mbalimbali. Matumizi ya lugha ya kawaida katika kipengele cha historia kinamfanya mwanajamii yeyote kuelewa historia ya jambo linalohusika; awe mtoto au mtu mzima katika jamii hiyo ataelewa kwa urahisi ujumbe uliopo katika wimbo wenye lugha ya kawaida. Lugha ya kisanaa wakati mwingine hueleweka kwa watu maalumu wenye uelewa wa kutafsiriwa lugha ya kisanaa.

Wimbo mwingine ambao umetumia lugha ya kawaida ni unaozungumzia aina ya mmea unaoitwa '*Mgelengana*'. Mmea huo, kwa mujibu ya waganga, hutumika kutibu maradhi mbalimbali kwa binadamu na wanyama. Hivyo, wazee wa zamani wakaona ni bora mti huo utungiwe wimbo ambao utahifadhi historia ya dawa hiyo. Waliamini kwamba, wimbo huweza kuishi muda mrefu kwa kurithishana toka kizazi kimoja hadi kizazi kingine tofauti na maisha ya binadamu ambayo ni mafupi. Ukweli ni kwamba, wimbo huo umedumu hadi wakati huu wakati wagunduzi wa mmea huo waliishafariki. Wimbo wenyewe unaitwa '*Mgelengana*' ukiwa umetumia lugha ya kawaida na huuimbwa kama ifuatavyo:

Kiongozi: *Mgelengana* aae dawa x2,
Toka zamani aee dawa x1,
Tukachimbe dawa,
Sisi ni wagonjwa,
Mgelengana x2.

Wazumi: *Mgelengana* aae dawa x2,
Toka zamani aee dawa x1,
Tukachimbe dawa,
Sisi ni wagonjwa,
Mgelengana x 2.

Kiongozi: Baba wote dawa,
Mgelengana baba,
 Mama eee dawa x 3.

Wazumi: Baba wote dawa,
Mgelengana baba,
 Mama eee dawa x3.
Chanzo: Uwandani (2017).

Kama tulivyoona katika wimbo huu, matumizi ya lugha ni ya kawaida ambayo mtu yeyote akiusikiliza wimbo huo, ataelewa kitu ambacho kinazungumzwa. Hivyo, matumizi ya lugha ya kawaida yanasaidia kufikisha ujumbe kwa urahisi kwa watu wenye uelewa mbalimbali, tofauti na lugha ya kisanaa ambayo wakati mwingine msanii hutunga kazi yake kwa kulilenga kundi maalumu. maalumu

Tendo la uimbaji wa nyimbo za tiba asili hujumuisha wagonjwa, wauguzi, wasaidizi wa mganga na mganga mwenyewe. Vilevile, huwa na waganga wanafunzi na mara chache huwa na watazamaji ambao hushiriki baada ya kusikia mdundo wa ngoma na kuvutiwa nao. Hivyo, lugha ya kawaida katika nyimbo za tiba asili hutumika ili kuvuta hisia za washirika wa tendo la uimbaji kwa kuwa huwa wanaelewa kwa urahisi kile kinachoimbwa. Mbinu hiyo huufanya wimbo uweze kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa walengwa bila kuwafikirisha sana. Lugha ya kawaida huwafanya washiriki ambao ni wageni kujifunza nyimbo kwa urahisi zaidi; kwa kuwa lugha inayotumika inakuwa inaeleweka kwa urahisi na humfanya mshiriki kujifunza kuimba kwa haraka.

5.2.2 Matumizi ya Lugha ya Kisanaa

Data za utafiti huu zinaonesha aina mbalimbali za matumizi ya lugha ya kisanaa. Suala la kuwapo kwa lugha ya kisanaa kwenye tanzu za fasihi simulizi kama ilivyo

nyimbo za tiba linaelezwa na kuungwa mkono na Biebyuck (1978), Mulokozi (1986) pamoja na Wamitila (2004). Katika kudhihiridha jinsi lugha ya kisanaa inavyotumika katika nyimbo za tiba asili, uchambuzi umefanyika kwa kuzingatia vipengele vya uchanganyaji msimbo, lugha ya picha na uradidi.

5.2.2.1 Uchanganyaji Msimbo

Wamitila (2010) anafafanua kuwa, kuchanganya msimbo ni kitendo cha kuingiza maneno, sentensi, virai au vishazi vya lugha moja kwenye lugha nyingine. Uingizaji huo unaweza kutokeza kwa maneno ya lugha mbili kuchanganywa katika kauli au sentensi moja au lugha moja kuachwa na msemaji kuhamia lugha nyingine. Katika utafiti huu, kuna nyimbo mbalimbali ambazo waimbaji wamechangaya lugha. Katika wimbo uitwao ‘*Ningalonga Ndauli*’ (Ntasema Nini?) kuna matumizi dhahiri ya uchanganyaji msimbo kama ulivyooneshwa:

Mganga: *Ningalonga ndauli x2,*
Wazumi: *Ningalonga ndauli x 2.*

Mganga: *Ningalonga ndauli x 2,*
Wazumi: *Ningalonga ndauli x 2.*

Mganga: *Ningalonga ndauli, pa **nyumba** pana lisoka,*
Wazumi: *Ningalonga ndauli, pa **nyumba** pana lisoka.*

Mganga: **Babu unange, babu unange,**
Washiriki: **Babu unange, babu unange.**

Mganga + Wazumi: *Pa **nyumba** pana lisoka,*
Mganga: *Pana lisoka, pana lisoka,*
Wazumi: *Pana lisoka, pana lisoka.*

Mganga + Wazumi: *Pana **nyumba** pana lisoka,*
Mganga: **Babu unange, babu unange, pa **nyumba** pana lisoka,**
Wazumi: **Babu unange, babu unange, pa **nyumba** pana lisoka.**

Tafsiri ya Kiswahili***Nitasema nini?***

Mganga: Nitaseme nini x2,

Wazumi: Nitaseme nini x2.

Mganga: Nitaseme nini x2,

Wazumi: Nitaseme nini x2.

Mganga: Nitaseme nini, ndani kuna nyoka,

Wazumi: Nitaseme nini, ndani kuna nyoka.

Mganga: Babu nisaidie, babu nisaidie,

Washiriki: Babu nisaidie, babu nisaidie.

Mganga + Wazumi: kwenye nyumba kuna nyoka,

Mganga: kuna nyoka, kuna nyoka,

Wazumi: kuna nyoka, kuna nyoka.

Mganga + Wazumi: kwenye nyumba kuna nyoka,

Mganga: Babu nisaidie, babu nisaidie, kwenye nyumba kuna nyoka,

Wazumi: Babu nisaidie, babu nisaidie, kwenye nyumba kuna nyoka.

Chanzo: Uwandani (2017).

Wimbo huu ni wa jamii ya Wabena na mzimu uliompana ni wa Wabena kwa sababu mganga huyu alienda kuongeza nguvu zake kwa Wabena. Katika wimbo huu wa Kibena kuna maneno ya lugha ya Kiswahili ambayo yamekozwa wino. Maneno hayo ni ‘babu’ na ‘nyumba’ ambayo kimsingi, yanguweza kuachwa kwa sababu kuna visawe vyake katika lugha ya Kibena. Kutumika katika wimbo ni kwa ajili ya mahitaji ya kisanaa kadiri fanani alivyoona ni rahisi kuufaya wimbo uimbike na kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Maelezo kuhusu wimbo huo yalitolewa na mganga:

“Wakati wa shughuli za tiba kuna jini mbaya alikuja na kuingia kwa mgonjwa. Hivyo, mzimu wa tiba uliona hatari hiyo na kwa kutumia wimbo huu taarifa ikanifikia kuwa kuna jini mbaya hivyo jitihada za kumuondoa zianze kufanyika. Hatimaye jini alitolewa kwa mgonjwa” (Mtafitiwa 4: Mahojiano yalifanyika, 18. 08. 2017).

Uchanganyaji msimbo unaweza kuchochewa na sababu kadhaa. Kwanza, inategemea jini au mzimu uliompana mwimbaji kwa wakati huo ni wa kabila gani? Jini au mzimu huo huimba wimbo uupendao. Ikumbukwe kuwa, wakati mgonjwa amepandwa na jini au mzimu, mambo anayoyafanya hayatokani na urazini wake, bali ni jini au mzimu uliompana. Maelezo haya yalielezwa na mmoja wa waganga aliyehojiwa wakati wa utafiti huu. Hivyo, mwimbaji huwa ni jini kupitia binadamu, hata sauti inayotoka kwa binadamu inakuwa si ile iliyozoeleka. Hali hii katika Nadharia ya Simiotiki tumeifanua kuwa ni kiashiria cha kiutamaduni ambacho hutumika kukamilisha kazi ya kifasihi. Nyimbo za tiba asili ni fasihi, hivyo pepo kumpanda mgonjwa ni sehemu ya kukamilisha tendo la kifasihi.

Sababu ya pili ya uchanganyaji msimbo katika nyimbo za tiba asili ni mahali ambako uganga ulipatikana. Hii ina maana kuwa, inategemea mganga amepatia wapi utaalamu wake wa uganga. Katika utafiti huu, ilibainika kuwa kuna mganga ambaye ni wa jamii ya Kimatengo, aliyekwenda kuongeza nguvu za uganga katika jamii ya Wabena. Hivyo, miongoni mwa nyimbo zake zipo za jamii ya Wabena ambazo anapoziimba mizimu ya Wabena humpanda na humsaidia katika kuifanikisha kazi yake ya utoaji tiba kwa wagonjwa wake. Kwa hiyo, uchanganyaji msimbo hapa ni matumizi ya lugha ya Kibena na Kimatengo. Sababu ya uchanganyaji msimbo huo ni kutokana na mganga kuwa na mizimu ya Kibena. Nadharia ya Simiotiki inajibainisha hapa kwa kuonesha msimbo wa kiutamaduni unavyofanyakazi katika nyimbo za tiba asili. Utangamano wa kiutamaduni ndio uliotumika kuchambua data hii. Ufuatao ni wimbo unaojulikana kwa jina la *'Gwala Maganza'* (Tengeneza Njia) ulioimbwa kwa lugha ya Kibena:

Mganga: **Ahoku** gwala maganza,
Ndevilima x3,

Wasaidizi: **Ahoku** gwala maganza,
Ndevilima x 3.

Mganga: **Ahoku** gwala maganza,
Ndevilima x3,

Wasaidizi: **Ahoku** gwala maganza,
Ndevilima x 3.

Tafsiri:

Tengeneza Njia

Mganga: Babu tengeneza njia,
Tupite x3,

Wasaidizi: Babu tengeneza njia,
Tupite x3.

Mganga: Babu tengeneza njia,
Tupite x3,

Wasaidizi: Babu tengeneza njia,
Tupite x3.

Chanzo: Uwandani (2017).

Wimbo huu kuna uchanganyaji msimbo wa Kibena na Kiswahili. Neno *Ahoku* la Kimatengo lina maana ya babu ambalo si la Kibena lugha ambayo kimsingi imetawala wimbo huo. Hata hivyo, inafaa kueleza hapa kwamba, jina ‘Ahoku’ lenye maana ya babu limebeba maana ya mizimu kisanaa. Sawa na maneno *gwala maganza* ya Kibena yenye maana ya ‘Tengeneza njia tupite’. Kisanaa, hii ina maana ya kuomba kurahisishiwa na kusaidiwa ili shughuli ya tiba ifanyike kwa mafanikio.

Wimbo mwingine unaodhihirisha uchanganyaji wa msimbo unaitwa ‘*Alalonga*’:

Mganga: **Nwane** alalonga lunoge,
Alonga lunoge,

Wazumi: **Nwane** alalonga lunoge,
Alonga lunoge.

Mganga: **Nwane** alalonga lunoge (**Ahoku**),
Alonga lunoge (**Ambuja**),

Wazumi: **Nwane** alalonga lunoge (**Ahoku**),
Alonga lunoge (**Ambuja**).

Tafsiri:**Amesema Utapona**

Mganga: Nani amesema utapona,
Amesema utapona,

Wazumi: Nani amesema utapona,
Amesema utapona.

Mganga: Nani amesema utapona (babu),
Amesema utapona (bibi),

Wazumi: Nani amesema utapona (babu),
Amesema utapona (bibi).

Chanzo: Uwandani (2017).

Katika wimbo huu pia kuna uchangayaji wa msimbo baina ya Kibena na Kimatengo. Maneno *ahoku naaAmbuja* yenye maana ya babu na bibi katika lugha ya Kimatengo yametumika kwenye wimbo ambao kimsingi ni wa Kibena.

Sababu ya tatu ya kuchanganya msimbo katika nyimbo za tiba asili ni kukosekana kwa msamiati. Taaluma ya tiba asili huambatana na utamaduni wa jamii inayohusika. Nadharia ya Simiotiki kwa kutumia mhimili wa msimbo wa kiutamaduni hubainisha viashiria mbalimbali vya kiutamaduni vinavyotumika katika kazi ya kifasihi ambavyo huunda uhalisi mahsusi katika fani inayohusika. Hivyo, imebainika kwamba, mwingiliano wa tamaduni na matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa katika jamii huifanya jamii kuongeza matumizi ya lugha ya Kiswahili. Matumizi ya lugha ya Kiswahili yamefanya hata nyimbo karibu zote za tiba asili katika mkoa wa Ruvuma ziimbwe kwa Kiswahili. Kuimbwa nyimbo hizi kwa lugha ya Kiswahili hakuwezi kubadili matumizi ya lugha kwa vifaa au vitu vyote kuwa katika lugha ya Kiswahili.

Kuna baadhi ya dawa zitabaki kuwa katika lugha ya asili hata kama nyimbo zitaimbwa kwa Kiswahili. Vilevile, baadhi ya vifaa vya tiba asili, majina yake

yatabaki katika lugha zinazoimbwa na kusababisha kuwa na mchanganyo wa msimbo. Mfano ufuatao ni wa wimbo wa ‘*Mgelengana*’ ambao unaimbwa kwa lugha ya Kiswahili, lakini jina la dawa inayoimbwa si la Kiswahili:

Kiongozi: *Mgelengana* aae dawa x2,
Toka zamani aae dawa x1,
Tukachimbe dawa,
Sisi ni wagonjwa,
Mgelengana x 2.

Wazumi: *Mgelengana* aae dawa x2,
Toka zamani aae dawa x1,
Tukachimbe dawa,
Sisi ni wagonjwa,
Mgelengana x 2.

Kiongozi: Baba wote dawa,
Mgelengana baba,
Mama eee dawa x 3.

Wazumi: Baba wote dawa,
Mgelengana baba,
Mama eee dawa x 3.
Chanzo: Uwandani (2017).

Katika wimbo huu, neno *Mgelengana* linatambulisha dawa katika utamaduni wa jamii za mkoa wa Ruvuma zinatumia neno hilo ambalo kwa hakika si la Kiswahili. Utafiti uligundua kuwa, katika nyimbo za tiba asili si dawa pekee ambazo zinatumia lugha ya asili, bali hata baadhi ya vifaa vinavyotumika katika tendo la uimbaji navyo vinatumia lugha za asili. Mfano wa baadhi ya vifaa hivyo ni kama vile *kinyenye* kwa maana ya kishoka, na *kibonga* kwa maana ya kirungu.

Uchanganyaji msimbo unajitokeza katika kiwango cha neno na hudhihirika kwa namna mbili. Kwanza, msamiati wa Kiswahili hudhirika kwenye lugha za asili. Hii ikiwa na maana kwamba, kimsingi, lugha inayotawala ni ya asili, lakini kuna

matumizi kiasi ya lugha ya Kiswahili. Katika wimbo uitwao *‘Ningalonga Ndauli’* uchanganyaji huo unadhihirika bayana:

Mganga: **Babu** *uunange*, **babu** *uunange*, *pa nyumba* pana *lisoka*,
Wazumi: **Babu** *uunange*, **babu** *uunange*, *pa nyumba* pana *lisoka*.

Katika wimbo huu tunaona maneno ‘babu’ na ‘nyumba’ yanajitokeza katika wimbo wa lugha ya Kibena. Lugha ya Kibena ina maneno yake yanayowakilisha maana za ‘babu’ na ‘nyumba’. Kwa lugha ya Kibena, ‘babu’ huitwa *‘huhuu’* na ‘nyumba’ huitwa *‘kaye’*. Lakini, kutokana na athari ya mwingiliano wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kibena, lugha ya Kibena imechukua maneno ya Kiswahili na kuyatumia katika nyimbo na matumizi mengine. Katika nadharia ya Mitindo msimbo huu wa uchanganyaji lugha unabainishwa kuwa unatokana na mfanyiko wa kimawasiliano kulingana na utamaduni, pamoja na utangamano wa fanani na hadhira.

Pili, kuna uchanganyaji wa msamiati wa lugha za asili katika nyimbo zinazoimbwa kwa Kiswahili. Kama tulivyoobainisha katika mfano wa kwanza na wa pili, katika sehemu hii, tumebainisha msamiati wa lugha za asili unavyojitokeza katika wimbo unaoimbwa kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo, mifano hii inayofuata, inaonesha uchanganyaji msimbo wa maneno ya lugha asili yanavyojitokeza katika lugha ya Kiswahili. Huu ni uchanganyaji msimbo wa aina ya pili kama tulivyoonesha hapo awali. Katika wimbo uitwao *‘Mgelengana’* unaoonesha uchanganyaji msimbo wa lugha asili katika wimbo wa lugha ya Kiswahili:

Kiongozi: **Mgelengana** aae dawa x2,
Wazumi: Toka zamani aee dawa x1.

Mgelengana ni jina la dawa kwa lugha ya Kingoni.

Jina hilo limeendelea kutumika hadi sasa na limetungiwa wimbo. Hivyo, kukosekana kwa jina la Kiswahili la dawa hiyo imelazimu jina hilo lizidi kutumia hata katika nyimbo na matumizi mengine ya lugha ya Kiswahili. Mfano mwingine wa maneno ya lugha ya asili kuchanganywa katika Kiswahili ni huu ufuatao uitwao ‘*Mizimu*’:

Mganga: Wee mizimu, wee mizimu,
Wazumi: Mizimu *kalili mwana* wee mzimu.

Mganga: Mababu wee mababu,
Wazumi: Mababu *kalili mwana* x4.

Katika wimbo huu ‘*Mizimu*’ kuna maneno *kalili* na *mwana* yamejitokeza. Maneno haya si ya Kiswahili, bali ni ya lugha za jamii ambayo yamejitokeza katika wimbo ulio katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, tumeona jinsi uchanganyaji msimbo wa maneno ulivyojitokeza kwa kutumia mifano hiyo. Uchambuzi huu umedhihirisha kuwa uchanganyaji msimbo hujitokeza kulingana na mahitaji ya jamii, kama yanavyoelezwa katika nadharia ya Simiotiki ya kiutamaduni.

5.2.2.2 Lugha ya Picha

Wimbo unaoitwa ‘*Ningalonga Ndauli*’ umetumia lugha ya picha kuwa ndani ya nyumba kuna nyoka. Lugha ya picha inachambuliwa vizuri kwa nadharia ya Mitindo kwa kutumia mhimili wa uchanganuzi lugha. Hivyo, maana inayoelezwa ya lugha za picha imefumbatwa na nadharia ya mitindo. Katika wimbo huo, neno ‘nyoka’ linamaanisha hatari iliyomwingia mmoja wa wagonjwa, yaani jini mbaya aliyemuvingia mgonjwa amefananishwa na nyoka. Hivyo, anaombwa babu (mzimu wa tiba) aweze kutoa tiba kwa mgonjwa aliyepatwa na tatizo hilo. Ufuatao ni mfano wa wimbo uliotumia lugha ya picha:

Mganga:	<i>Ningalonga ndauli x,2</i>
Wazumi:	<i>Ningalonga ndauli x 2.</i>
Mganga:	<i>Ningalonga ndauli x 2,</i>
Wazumi:	<i>Ningalonga ndauli x 2.</i>
Mganga:	<i>Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lizoka,</i>
Wazumi:	<i>Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lizoka.</i>
Mganga:	Babu <i>uunange</i> , babu <i>uunange</i> ,
Washiriki:	Babu <i>uunange</i> , babu <i>uunange</i> .
Mganga +	Wazumi: <i>Pa nyumba pana lisoka,</i>
Mganga:	<i>Pana lisoka, pana lisoka,</i>
Wazumi:	<i>Pana lisoka, pana lisoka.</i>
Mganga +	Wazumi: <i>Pa nyumba, pana lisoka,</i>
Mganga:	Babu <i>uunange</i> , babu <i>uunange, pa nyumba pana lisoka,</i>
Wazumi:	Babu <i>uunange</i> , babu <i>uunange, pa nyumba pana lisoka.</i>
	Chanzo: Uwandani (2017).

Katika wimbo huo neno *lisoka* lenye maana ya nyoka ni taswira ya hatari iliyopo ndani ya nyumba.

5.2.2.3 Uradidi

Katika ushairi-simulizi uradidi ni kitu cha kawaida kujitokeza. Wamitila (2004) anaeleza kuwa, moja ya mbinu ya kisanaa katika ushairi simulizi ni uradidi. Nadharia ya Mitindo katika mhimili wa uchanganuzi lugha inaelezea matumizi ya lugha kibalagha. Mbinu mojawapo inayotajwa katika matumizi ya lugha kuwa ni urudiaji na mbinu za urudiaji huo. Katika utafiti huu, tumebaini kwamba, kiwango cha uradidi katika nyimbo za tiba asili kimekuwa kikibadilika kutegemea idadi ya beti za wimbo. Beti zikiwa chache, uradidi hujitokeza zaidi kuliko beti zikiwa nyingi. Kuna nyimbo zenye kiwango kikubwa cha uradidi kama inavyoonekana kwenye wimbo uitwao 'Mjukuu Analia' ufuatao hapa chini:

Mganga: Mjuku aee,
Mjuku analia aee,
Wazumi: Mjuku aee,
Mjuku analia aee.

Mganga: Mjuku aeee,
Baba mjuku analia aee,
Wazumi: Mjuku aeee,
Baba mjuku analia aee.

Mganga: Tukachimbie dawa,
Mjuku aee,
Mjuku analia aee,
Wazumi: Mjuku aee,
Mjuku analia aee.,
Chanzo: Uwandani (2017).

Katika wimbo huu, uradidi neno mjuku limejitokeza katika kila mstari. Pia, kuna sauti za mwisho ‘aee’ karibu katika kila mshororo zinaradidiwa. Hivyo, kuna uradidi wa neno katika kila mshororo. Wakati mwingine, uradidi unaweza kufanyika ndani ya mshororo mmoja kama unavyohibitishwa na data ya wimbo wa ‘*Furaha*’ ufuatao:

Kiongozi: Furaha furaha furaha ee,
Furaha furaha furaha leo x2,
Wazumi: Furaha furaha furaha ee,
Furaha furaha furaha leo x2,.

Kiongozi: Furaha furaha furaha eeh,
Furaha furaha furaha ya majini,
Wazumi: Furaha furaha furaha eee,
Furaha furaha furaha eee.

Kiongozi: Ushindi ushindi ushindi ee,
Ushindi, ushindi, ushindi ee,
Wazumi: Furaha, furaha, furaha ee,
Furaha, furaha, furaha ee.

Kiongozi: Amani, amani, amani ee,
Amani, amani, amani ee,
Wazumi: Furaha, furaha, furaha ee,
Furaha, furaha, furaha ee.
Chanzo: Uwandani (2017).

Katika wimbo huu, kila mshororo umekuwa na uradidi wa maneno furaha, ushindi na amani pamoja na sauti za mwisho ‘ee’ zimeradidiwa ndani ya mshororo mmoja. Wimbo mzima umetawaliwa na maneno ‘furaha’, ‘ushindi’ na ‘amani’. Hivyo, huu ni mtindo wa uradidi unaojitokeza kwa kiasi kikubwa katika nyimbo za tiba asili. Katika kujadili umuhimu wa uradidi katika fasihi simulizi ya Kiafrika, Okpewho (1992) anasema kuwa, uradidi una dhima za kiujumi na kiuamilifu katika fasihi simulizi ya Kiafrika.

Nadharia ya Mitindo inafafanua kuwa, uradidi ni mbinu ambayo sio tu huathiri ujumi au kuzifanya tanzu za kifasihi simulizi zivutie zaidi; lakini huathiri utokeaji wa vipengele mbalimbali vinavyounda nyimbo za kifasihi simulizi. Kiujumi, kupendeza kwa nyimbo katika uimbaji huchangiwa na uradidi ambao huufanya wimbo uwe na vionjo vyenye kuwavutia waimbaji na wasikilizaji. Kiuamilifu, uradidi huwa na dhima ya kusisitiza dhamira iliyopo katika wimbo unaohusika. Katika wimbo huo wa ‘*Furaha*’, tumeona dhamira inayosisitizwa ni furaha, amani na ushindi.

5.2.3 Mtindo wa Nyimbo za Tiba Asili kutokana na Urefu

Nyimbo zinazotumika katika tiba asili zinatofautina kwa urefu. Katika utafiti huu, vigezo vilivyotumika kutofautisha urefu wa nyimbo ni idadi ya maneno, wakaa, beti, na mishororo kama inavyofafanuliwa katika sehemu inayofuata.

5.2.3.1 Urefu kwa Kigezo cha Idadi ya Maneno

Katika kuchunguza vipengele hivi, tumeonesha jinsi vinavyochangia kuibua dhamira mbalimbali na kukamilisha tendo zima la uimbaji wa nyimbo za tiba asili vikiwa sehemu muhimu ya mtindo wake. Katika utafiti huu, data zinaonesha kuwapo kwa

nyimbo fupi fupi ambazo licha ya kutokuwa na kigezo majumui kinachokubalika katika kupima urefu. Hata hivyo, hoja hii inaweza kuthibitishwa kwa kutumia idadi ya maneno. Tunachukulia kwamba ,wimbo wenye maneno mawili hadi matatu kuwa ni wimbo mfupi na wimbo wenye maneno manne na kuendelea kuwa ni mrefu. Wimbo uitwao ‘*Niyaule*’ unadhihirisha dhana ya ufupi wa wimbo katika muktadha wa utafiti huu na unaimbwa kama ulivyokaririwa:

Kiongozi: *Niyaule* (Naenda),
 Wazumi: *Kumikongo* (Kwenye miti).
Chanzo: Uwandani (2017).

Kinachofanya wimbo huu wa maneno mawili ukamilike ni urudiaje unaofanywa na waimbaji kwa kufuata mahadhi ya kimuziki. Wimbo huu ujulikanao kama ‘*Naluta*’ ni mfano wa wimbo wa maneno matatu ambao pia unaainishwa katika utafiti huu kuwa ni wimbo mfupi kama inavyoonekana katika data ifuatayo:

Kiongozi: *Unene naluta*,
 Wazumi: *Ndegelela*,
Chanzo: Uwandani (2017).

Wimbo huo una maneno matatu, na ukamilifu wake, unatokana na urudiaji wa maneno hayo wakati wa uimbaji. Kwa upande mwingine, kuna nyimbo zenye maneno kuanzia manne na kuendelea ambazo katika utafiti huu zinabainishwa kuwa ni nyimbo ndefu. Wimbo unaitwa ‘*Njoo Tuonane*’ ambao uliimbwa kwa lugha ya Kiswahili unadhihirisha mtindo wa nyimbo ndefu:

Mganga: Abubakari jini, njoo tuonane,
 Wazumi: Abubakari jini, njoo tuonane,
 Mganga: Panda milima jini, njoo tuonane,
 Wazumi: Panda milima jini, njoo tuonane.
Chanzo: Uwandani (2017).

Katika wimbo huu, kuna maneno 6 ambayo yanajirudia kuanzia mwanzo hadi mwisho wa wimbo. Maneno yanayojirudia ni Abubakari, jini, njoo, tuonane, panda na milima. Hivyo, idadi ya maneno imeufanya wimbo huo uwe mrefu kwa kuzingatia uainishaji unaofanywa katika utafiti huu. Uradidi ni sifa mojawapo katika fasihi simulizi ambayo pamoja na masuala mengine, unasaidia kukazia dhamira zinazoibuliwa na nyimbo unaohusika.

5.2.3.2 Urefu kwa Kigezo cha Beti

Katika utafiti huu,, data zinaonesha kwamba nyimbo zinafuata mtindo wa uimbaji wa pande mbili, ambapo kunakuwa na mwimbishaji na waitikiaji. Dhana ya beti kwa mujibu wa Wamitila (2003) ni kifungu cha mshororo mmoja mmoja au mishororo kadhaa katika shairi ambacho kimejitosheleza. Dhana ya ubeti katika utafiti huu inazingatia kukamilika kwa maneno ya mwimbishaji na waitikiaji. Katika wimbo uitwao ‘*Nipe Dawa Nzuri*’ una jumla ya beti mbili kama ulivyonukuliwa:

Mganga: Nilikwenda Kisimani,
Nikamkuta jini,
Jini wangu **mganga** huyo,
Nipe dawa jini x4.

Wazumi: Nilikwenda Kisimani,
Nikamkuta jini,
Jini wangu **mganga** huyo,
Nipe dawa jini x4.

Mganga: Nipe dawa nzuri,
Nipe dawa nzuri,
Nipe dawa nzuri,
Nipe dawa nzuri x4.

Wazumi: Nipe dawa nzuri,
Nipe dawa nzuri,
Nipe dawa nzuri,
Nipe dawa nzuri x 4.
Chanzo: Uwandani (2017).

Wimbo wa *'Nipe Dawa Nzuri'* una beti mbili ambapo kila beti inaanazishwa na mganga na kukamilishwa na sauti za wazumi kisha mganga huanza upya na katika beti mpya. Inafaa kuisitiza hapa kwamba, beti katika nyimbo haijitokezi waziwazi kwa kuwa ni ushairi-simulizi tofauti na ushairi-andishi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, nyimbo hubadilika kutegemena na uwasilishaji, hadhira pamoja na wakati. Katika kuelezea mhimili wa uchambuzi wa lugha kwa nadharia ya Mitindo, Wamitila (2008) anasema kuwa, maarifa yanayotokana na isimu hutumiwa ili kubaini sifa za kimtindo katika kazi za kifasihi.

Anazitaja baadhi ya sifa hizo kuwa ni za kifonolojia (ruwaza za sauti, vina, mizani) na kisintaksia (miundo ya sentensi, aina ya sentensi). Kwa hiyo, beti za nyimbo katika utafiti huu, tumeziangalia kwa kigezo cha namna fanani na hadhira wanavyopokezana kuimba. Pale ambapo wazumi wanamalizia kuitikia kutoka kwa fanani, ndio Kunakamilisha ubeti mmoja. Hivyo, idadi ya beti inaamua kiwango cha urefu wa nyimbo. Kadiri wimbo uanavyokuwa na beti nyingi, ndivyo unavyochukuliwa kuwa mrefu au mfupi zaidi ikilinganishwa. Wimbo ufuatao unaoitwa *'Nolenole'* una jumla ya beti tatu (3) kama unavyoonekana:

Mganga: *Nole nole,
Aee! Nole nole,
Nole nole aee,
Jini wa milima,
Kufukuza homa.*

Wazumi: *Nole nole,
Aee! Nole nole,
Nole nole aee,
Jini wa milima,
Fukuza homa.*

Mganga: *Nole nole,*
Aee! Nole nole,
Nole nole aee,
 Jini wa milima,
 Fukuza homa.

Wazumi: *Nole nole,*
Aee! Nole nole,
Nole nole aee,
 Jini wa milima,
 Fukuza homa.

Mganga: *Aee! Nole nole,*
Nole nole aee,
 Jini wa bahari,
 Punguza homa.

Wazumi: *Aee! Nole nole,*
Nole nole aee,
 Jini wa bahari,
 Punguza homa.

Wimbo huu unatofautiana na wimbo uitwao ‘Tuombe’ wenye jumla ya beti nne (4)

kama unavyoonekana hapa:

Kiongozi: Wee tuombe daima,
 Aee daima,
 Na majini wa milimani tabu sana,
 Aee daima.

Wazumi: Wee tuombe daima,
 Aee daima,
 Na majini wa milimani tabu sana,
 Aee daima.

Kiongozi: Tuimbe wote daima aee, baba,
 na majini wa milimani tabu leo,
 Aee daima.

Wazumi: Tuimbe wote daima aee, baba,
 na majini wa milimani tabu leo,
 Aee daima.

Kiongozi: Ena ena daima,
 Aee daima,
 Na majini ya milimani tabu sana.

Wazumi: Tuimbe wote daima aee, baba,
Na majini wa milimani tabu leo,
Aee daima.

Kiongozi: Tuombe na mababu,
Aee daima,
Na majini ya milimani tabu sana.

Wazumi: Tuombe na mababu,
Aee daima,
Na majini ya milimani tabu sana.
Chanzo: Uwandani (2017).

Nyimbo hizi mbili zinawakilisha nyimbo nyingi za tiba asili ambazo kwa kigezo cha idadi ya beti inaweza kuelezwa kwamba zinatofautiana kwa urefu ambapo wimbo uitwa ‘*Nolenole*’ ni mfupi kuliko wimbo uitwao ‘*Tuombe*’.

5.2.3.3 Urefu wa Nyimbo kwa Kigezo cha Wakaa

Dhana ya wakaa kama kipengele cha mtindo wa nyimbo za tiba asili, inarejelea muda unaotumika tangu kuanza kwa wimbo mpaka kumalizika. Hapo awali katika ufafanuzi wa urefu wa nyimbo kwa kigezo cha idadi ya maneno na beti imeelezwa kwamba ,nyimbo zenye maneno machache na beti chache ni fupi na kinyume chake ni kweli. Mantiki ya kawaida inaelekea kutueleza kwamba, wimbo wenye maneno machache utatumia muda mfupi kuliko ule wenye maneno mengi. Pia, maelezo haya yanaweza kuchukuliwa kwa mantiki sawa kinapotumika kigezo cha beti. Katika utafiti huu, ilishuhudiwa kwamba, wimbo uitwao ‘*Niyaule*’ wenye maneno mawili tu kama ulivyonukuliwa hapa chini:

Kiongozi: *Niyaule*,
Wazumi: *Kumikongo*.
Chanzo: Uwandani (2017).

Wimbo huu uliimbwa kwa muda mrefu kuliko wimbo wenye maneno zaidi ya manne uitwao 'Ndembekulugwa' kama ulivyonukuliwa hapa chini:

Mganga: *Ndembekulugwa, ndembekulugwa wewe?
Ndembekulugwa, ndembekulugwa eee,
Ndembekulugwa, kupalapala mikongo,*

Wazumi: *Ndembekulugwa, ndembekulugwa uweje?
Ndembekulugwa, ndembekulugwa eee,
Ndembekulugwa, kupalapala mikongo.*

Mganga: *Kupalapala mikongo, uweje,*
Wazumi: *Ndembekulugwa, kupalapala mikongo.*

Mganga: *Kupalapala mikongo, eee, uweje,*
Wazumi: *Ndembekulugwa, kupalapala mikongo.*

Tafsiri:

Mganga: Mungu mkubwa, mungu mkubwa, wewe,
Mungu mkubwa, Mungu mkubwa, eee,
Mungu mkubwa, tusaidie kupata dawa,

Wazumi: Mungu mkubwa, mungu mkubwa, wewe,
Mungu mkubwa, mungu mkubwa, eee,
Mungu mkubwa, tusaidie kupata dawa.

Mganga: Mungu mkubwa, wewe,
Wazumi: Mungu mkubwa, tusaidie kupata dawa.

Mganga: Mungu mkubwa, eee, wewe,
Wazumi: Mungu mkubwa, tusaidie kupata dawa.,

Chanzo: Uwandani (2017).

Kimsingi kinachoamua muda kiasi gani utumike kukamilisha uimbaji ni tukio lililohitajia uimbaji wa wimbo. Ilishuhudiwa katika utafiti huu kwamba, wimbo wenye maneno mawili katika tukio la kufaurahia kupona kwa mgonjwa uliimbwa kwa muda mrefu zaidi kuliko wimbo wenye maneno mengi zaidi katika tukio la kuaga wakati wa kuondoka kwa mganga. Nadharia ya Mitindo inatumika kuchambua data hii kwa kuonesha jinsi muundo wa tukio la kiutendaji kulingana na muktadha

linavyoukilia wakaa wa uimbaji hivyo kuwa kipengele muhimu cha mtindo katika nyimbo za tiba asili.

5.3 Mishororo

Mulokozi (2017) anaeleza mshororo kuwa ni mstari mzima wa shairi ambao katika shairi la kimapokeo hujitosheleza kimaana. Mshororo huweza kuwa na kipande kimoja, viwili au zaidi kutegemea aina ya shairi linalohusika. Anaendelea kufafanua kuwa ushairi wa mavue/ tungo huru, mshororo si lazima ujitosheleze kimaana. Wazo la mstari mmoja laweza kuendelezwa katika mstari au mistari inayofuatia. Katika utafiti huu, tunatumia istilahi mshororo kwa sababu ni nzuri zaidi kuliko mstari kwa kuwa inazingatia aina zote za tungo, zikiwemo tungo-simulizi ambazo hazina ambao ni bayana katika uwasilishaji. Katika uchambuzi tumetumia nadharia ya Mitindo kwa kuangalia matumizi lugha na tunaangalia ujitokezaji wa mishororo katika nyimbo za tiba asili. Wimbo uitwao *'Mababu na Malaika Mtusaidie'* umeundwa na mishororo kama ifuatavyo:

Mganga: Mababu na Malaika kwa uwezo wenu baba mtusaidie
Wasaidizi: Mababu na malaika kwa uwezo wenu baba mtusaidie

Mganga: Maombi kwa malaika x 3,
Maombi yetu wote x2,
Wasaidizi: Maombi kwa malaika x 3,
Maombi yetu wote x 2.

Mganga: Maombi eee maombi eee x2,
Wasaidizi: Maombi eee maombi eee x2.

Mganga: Maombi yetu wote,
Maombi eee x2,
Wasaidizi: Maombi yetu wote,
Maombi eee x 2.
Chanzo: Uwandani (2017).

Wimbo huu una mishororo 12. Mshororo wa ufunguzi ni mrefu, yaani una maneno sita, viunganishi viwili na mishororo inayofuata ina neno moja hadi maneno matatu. Katika muktadha mwingine, wimbo uitwao ‘*Furaha*’ una mishororo 12 kama unavyonukuliwa hapa chini:

Kiongozi:	Furaha furaha furaha ee, Furaha furaha furaha leo x2,
Wazumi:	Furaha furaha furaha ee, Furaha furaha furaha leo x2.
Kiongozi:	Furaha furaha furaha eeh, Furaha furaha furaha ya majini,
Wazumi:	Furaha furaha furaha eee, Furaha furaha furaha eee.
Kiongozi:	Ushindi ushindi ushindi ee, Ushindi, ushindi, ushindi ee,
Wazumi:	Furaha, furaha, furaha ee, Furaha, furaha, furaha ee.
Kiongozi:	Amani, amani, amani ee, Amani, amani, amani ee.
Wazumi:	Furaha, furaha, furaha ee, Furaha, furaha, furaha ee.

Chanzo: Uwandani (2017).

Nyimbo hizi mbili zinapolinganishwa kwa urefu, wimbo wa ‘*Mababu na Malaika Mtuombe*’ unachukuliwa kuwa ni mfupi wakati wimbo wa ‘*Furaha*’ unachukuliwa kuwa ni mrefu. Katika mazingira mengine, wimbo unaweza kuwa na mishororo miwili tu kama data ya wimbo wa ‘*Liyaule*’ inavyoonesha hapa chini:

Kiongozi: *Liyaule*,
Wazumi: *Kumagongo*.
Chanzo: Uwandani (2017).

Mulokozi (2007) anasema mshororo katika shairi la kimapokeo hujitosheleza kimaana. Mshororo huweza kuwa na kipande kimoja, viwili au zaidi kutegemea aina

ya shairi linalohusika. Anaendelea kufafanua kuwa, katika ushairi wa mavue/ tungo huru, mshororo si lazima ujitosheleze kimaana; wazo la mstari mmoja linaweza kuendelezwa katika mstari au mistari inayofuatia. Katika utafiti huu, tumebaini kuwa, sifa za mashairi ya kimapokeo na ya kisasa zinajitokeza katika nyimbo za tiba asili, hasa katika kipengele cha mshororo kujitosheleza na kutojitosheleza kimaana.

Kwa jumla, hakuna idadi inayoweka ukomo wa idadi ya mishororo katika nyimbo za tiba asilia. Idadi ya mishororo kama ilivyo kwa idadi ya maneno na beti hutegemea muktadha na kiini cha uimbaji wa wimbo husika. Kuhusu mishororo, mantiki inaelekea kueleza kwamba, kuna nyimbo zinazoanzia na mshororo mmoja hadi mishororo mingi kulingana na mahitaji na muktadha wa uimbaji. Kwa hiyo, kulingana na kigezo hiki, katika utafiti huu kuna nyimbo zenye beti za mshororo mmoja hadi mishororo 30. Tumebaini kwamba, idadi ya mishororo inaweza kuongezeka kulingana na wakaa wa uimbaji.

5.3.1 Fomula

Wamitila (2004) anasema kuwa tungo nyingi zinazohusishwa na ushairi-simulizi huwa na fomula. Fomula ni maneno na vifungu fulani vinavyorudiwa. Fomula hizi huwapo kwa vijalizo vya aina na mizani au kaida za ushairi wenyewe. Katika utafiti huu fomula inahusisha urari wa matumizi ya ala katika uimbaji kama ilivyo manyanga na ngoma. Katika utafiti huu, imebainika kuwa, matumizi makubwa ya fomula za namna mbalimbali kabla ya kuanza kuimba, wakati wa uimbaji (wimbo ukiendelea) na wakati wa kuhitimisha uimbaji. Katika kuthibitisha hili tunatumia wimbo uitwao '*Nipe Udi*' unaonesha fomula:

Mganga: Nipe udi na ubani mwalimu,
Nipe udi wana ubani.

Wazumi: Nipe udi na ubani mwalimu,
Nipe udi na ubani.

Mganga: Wee! Nipe udi na ubani mwalimu,
Nipe udi na ubani tuombe.

Wazumi: Nipe udi na ubani mwalimu,
Nipe udi na ubani.

Chanzo: Uwandani (2017).

Kwa kutumia wimbo wa ‘*Nipe Udi*’ utafiti huu unaonesha hatua mbalimbali zinazoambatana na tendo la uimbaji.

Mganga: Nipe udi na ubani mwalimu } bila vifaa,
 Nipe udi wana ubani. }

Huu ni ubeti wa kwanza wa wimbo wa tiba asili. Ubeti huu unapoanza kuimbwa mwimbishaji huimba bila kutumia ala yoyote ya muziki. Utaratibu huu umejitokeza katika nyimbo zote. Ubeti unaofuata unaonesha fomula nyingine:

Wazumi: Nipe udi na ubani mwalimu, } Manyanga
 Nipe udi na ubani. }

Ubeti wa pili unapokelewa na wazumi ala za muziki huanza kwa kutumia manyanga ndio ala ya kwanza kuanza kupigwa:

Mganga: Wee! Nipe udi na ubani mwalimu, } Manyanga na ngoma
 Nipe udi na ubani tuombe. }

Wazumi: Nipe udi na ubani mwalimu,
 Nipe udi na ubani.

Katika ubeti wa tatu na kuendelea ndipo vifaa vyote huanza kutumia. Hii inajitokeza kwa nyimbo nyingi zinazoimbwa katika tiba asili mkoani Ruvuma. Kama tulivyoona, fomula ya kwanza katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili ni matumizi ya udi, kisha manyanga na ngoma. Pia, katika uimbaji kuna uchezaji na matumizi ya vifaa vingine na mavazi maalumu. Vyote hivi hukamilisha tendo la uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili kuna mavazi maalumu. Mavazi hayo huvaliwa na mganga pamoja na hadhira yake. Mavazi hutegemeana na aina ya shughuli inayofanyika. Kuna mavazi maalumu kwa watu wote; hapa vazi la kaniki hutumika.

Kuna mavazi kwa ajili ya mgonjwa maalumu au mavazi maalumu kwa mganga husika. Rangi za mavazi hutegemea mahitaji ya mizimu kwa wakati unaohusika. Kuimba kwa kupokezana ni mtindo ambao upo katika nyimbo zote za tiba asili. Hakuna wimbo utakaoimbwa na mtu mmoja peke yake. Wimbo ukianza kuimbwa wazumi hufuata maneno ya kiongozi au mganga huku wakicheza katika duara. Uchezaji hutofautiana baina ya mzumi mmoja na mwingine. Kipengele cha uchezaji kimedadavuliwa katika kipengele cha miondoko ya waimbaji. Sehemu ya mwisho ya nyimbo za maombi aghalabu huishia kwa mgonjwa kupandisha pepo. Hapo mganga huanza kuzungumza na pepo wa mgonjwa, na ndipo maradhi mengi hutibiwa. Baada ya tendo la tiba kukamilika ambalo huenda pamoja na uimbaji, wimbo maalumu kwa ajili ya kuaga mizimu huimbwa. Hivyo, tendo la uimbaji na uchezaji hukamilishwa na wimbo wa shukrani na kuiaga mizimu.

Wachezaji wa wimbo huu hucheza kwa kurudi kinyumenyume hadi kutoka katika jukwaa la kuimba nyimbo za tiba asili. wimbbo wa ‘*Kwa Herini*’ ni mmoja kati ya nyimbo hizo za kuaga:

Mganga: Kwa herini, aee,
Wazumi: Kwa herini, aee .

Mganga: Tutaonana, aee,
Wazumi: Tutaonana, aee.

Mganga: Mungu akipenda, aee,
Wazumi: Mungu akipenda, aee.

Mganga: Bai bai tutaonana, aee,
Wazumi: Bai bai tutaonana, aee.

Mganga: Tuombe mungu, aee,
Wazumi: Tutaonana, aee.
Chanzo: Uwandani (2017)

Nadharia ya Mitindo unafafanua kwamba muundo wa tukio la kiutendaji hulingana na muktadha. Tumbani kwamba, kabla ya kuanza kuimba kitu cha kwanza ni lazima udi uwashwe na kila mshiriki lazima awe na udi. Utaratibu huu ni maalumu kwa nyimbo za maombi. Udi huwasaidia waimbaji na wenye pepo kuimba nyimbo zitakazowafurahisha pepo; na mgonjwa mwenye ugonjwa uliosababishwa na pepo wabaya hupona haraka au atapona kwa haraka udi ukitumika.

5.3.2 Daiolojia

Uwasilishaji wa nyimbo za tiba asili huwashirikisha fanani (mganga au kiongozi) na hadhira (wazumi) katika kuimba, kucheza na kupiga ala mbalimbali za muziki. Ushirikishwaji huo pia tumeuita mtindo wa mwitiko kwa sababu ndani ya mtindo huo kuna majibizano na kuimba kwa kupokezana baina ya mganga au kiongozi na

wazumi. Katika nadharia ya Mitindo, daiolojia tumeiweka katika mhimili wa utengamano wa fanani na hadhira. Kupokezana katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili hufanyika ili kukamilisha tendo la tiba.

Kupokezana huko si kwa namna moja bali hubadilikabadilika kutoka aina moja au wimbo mmoja hadi nyingine. Upokezanaji huu hutokea kwa namna tofauti tofauti. Zifuatazo ni aina mbalimbali za upokezanaji. Aina hizo tunaziangalia kwa kutumia mifano ifuatayo: Mfano wa kwanza ni pale ambapo mwimbishaji ni mganga na waitikiaji ni wazumi. Hivyo, daiolojia hapa ni baina ya mganga na wazumi. Mfano wa wimbo unaoshirikisha mganga na wazumi ni huu uitwao *'Tunakuomba Baba'*:

Mganga: Tunakuomba baba,
Majini yote mwana,
Tufungulie mwanga,
Tuonee huruma.

Wazumi: Tunakuomba baba,
Majini yote mwana,
Tufungulie mwanga,
Tuonee huruma.

Mganga: Tunaomba majini yote,
Mtufungulie mwanga,
Mtuonee huruma.

Wazumi: Tunaomba majini yote,
Mtufungulie mwanga,
Mtuonee huruma.

Chanzo: Uwandani (2017).

Mfano wa pili ni wimbo ulioimbishwa na msadizi wa mganga. Hivyo, hapa daiolojia ni kati ya msaidizi wa mganga ambaye katika wimbo uitwao *'Kalima'* anajulikana kuwa kiongozi:

Kiongozi: Kalima kale kadogo, wee nashindwa kupanda,
Wazumi: Kalima kale kadogo, wee nashindwa kupanda.

Kiongozi: Kale kadogo, nashindwa kupanda,
Wazumi: Kale kadogo, nashindwa kupanda.

Kiongozi: Ukamweleze mwalimu akapande,
Wazumi: Ukamweleze mwalimu akapande.
Chanzo: Uwandani (2017).

Katika mfano wa tatu data inatuonesha daiolojia inayofanywa baina ya mganga kwa upande mmoja na baadaye wote. Hapa, ganga na wazumi wanaimba kwa pamoja kwa kushirikiana. Jambo hilo limeoneshwa pia katika wimbo wa *'Tuombe na Malaika'*:

Mganga: Tuombe tuombe tuombe na malaika,
Mganga + Wazumi: Tuombe tuombe tuombe watusaidie,
Mganga + Wazumi: Tuombe tuombe tuombe na malaika,
Mganga + Wazumi: Tuombe tuombe tuombe majini yote.

5.3.3 Viunganishi

Sifa mojawapo ya mtindo wa nyimbo ni kuwa na viunganishi vichache. Katika wimbo uitwao *'Mizimu'* katika data inayofuata hapa chini kuna kiunganishi kimoja pekee:

Mganga: Wee mizimu, wee mizimu,
Wazumi: Mizimu kalili mwana wee mizimu.

Mganga: Mababu wee mababu,
Wazumi: Mababu kalili mwana x4.

Mganga: Mumsaidie,
Wazumi: Mababu kalili mwana mababu.

Mganga: Mumsaidie,
Wazumi: Mababu kalili mwana mababu.

Mganga: Anahangaika,
Afanye nini mwana?
Wazumi: Wanaitikia vivyo hivyo.

Mganga: **Mumsaidie na maombi yake,**
Wazumi: Anahangaika,
Mumhurumie.
Chanzo: Uwandani (2017).

Katika wimbo huo, kuna mshororo unaosema **mumsaidie na maombi yake** ambao umetumia kiunganishi ‘na’. Suala la nyimbo za tiba asili kuwa na viunganishi vichache limelezwa pia na Wamitila (2004) anapozungumzia ushairi-simulizi kwa jumla, kwamba, huhusishwa na uchache wa viunganishi. Maneno mbalimbali hayaungwi pamoja kwa matumizi ya “na” na viunganishi vingine. Nadharia ya Mitindo kwa kutumia mhimili wa uchanganuzi lugha inaonesha namna uteuzi wa maneno unavyofanyika kulingana na mahitaji ya matini inayohusika.

Hivyo, matumizi ya viunganishi vichache katika katika nyimbo za tiba asili yanaibua mtindo muhimu katika nyimbo hizo. Aidha, kuna nyimbo nyingine hazina viunganishi kabisa. Baadhi ya mifano ya nyimbo zisizo na viunganishi ni huu wa ‘*Nipe Dawa Nzuri*’:

Mganga: Nilikwenda Kisimani,
Nikamkuta jini,
Jini wangu **mganga** huyo,
Nipe dawa jini.

Wazumi: Nilikwenda Kisimani,
Nikamkuta jini,
Jini wangu **mganga** huyo,
Nipe dawa jini x4.

Mganga: Nipe dawa nzuri,
Nipe dawa nzuri,
Nipe dawa nzuri,
Nipe dawa nzuri x4.

Wazumi: Nipe dawa nzuri,
 Nipe dawa nzuri,
 Nipe dawa nzuri,
 Nipe dawa nzuri x4.
Chanzo: Uwandani (2017).

Wimbo huu hauna kiunganishi hata kimoja suala ambalo linashadadia maelezo ya wanafasihi wengine, akiwamo Wamitila (2004) kwamba, ni kawaida kwa nyimbo na ushairi simulizi kutokuwa na viunganishi vingi.

5.3.4 Vina na Mizani

Katika ushairi wa kimapokeo vina na mizani hukuchuliwa kama uti wa ushairi (Abed, 1952). Dhana hiyo ni tofauti na nyimbo za tiba asili ambazo kanuni zake za utunzi ni tofauti na mashairi ya kimapokeo. Mashairi ya kimapokeo ni fasihi andishi na nyimbo ni fasihi simulizi. Katika nyimbo kuna ubadilikaji au ugeukaji wa tungo. Utungo unawasilishwa jukwaani au mbele ya hadhira unaweza kubadilika kutegemea mwasilishaji, hadhira pamoja na wakati.

Vilevile, uwasilishwaji unaweza kuachwa au kubadilishwa. Hali hii hufanya mpangilio wa vina na mizani kutokuwa imara. Katika utafiti wetu, tumegundua kwamba, uradidi hufanya uwepo wa vina katika nyimbo. Vina hivi mara nyingi huwa vina vya mwisho. Kwa kuwa mishororo mingi ya nyimbo huwa ni kipande kimoja, hata zile nyimbo zenye vipande viwili haziwi na vina vya kati. Ufuatao ni wimbo wa '*Nipe Udi*' ni mfano mmojawapo wa nyimbo hizo:

Mganga: Nipe udi na ubani mwalimu,
 Nipe udi na ubani.

Wazumi: Nipe udi na ubani mwalimu,
 Nipe udi na ubani.

Mganga: Wee! Nipe udi na ubani mwalimu,
Nipe udi na ubani tuombe.

Wazumi: Nipe udi na ubani mwalimu,
Nipe udi na ubani tuombe.
Chanzo: Uwandani (2017).

Katika wimbo huu, uradidi katika uimbaji ndio ulifanya kuwapo kwa vina. Vina vinajitokeza kila baada ya kupokezana katika uimbaji, kwa kuwa wazumi huitikia maneno yale yale yaliyoimbishwa na fanani (mganga). Vina vilivyojipambanua ni -**mu** kila baada ya mstari mmoja, na **-ni**; kisha **-mbe**. Baadhi ya nyimbo zilizochunguzwa uwandani zilibainika kuwa na mchanganyiko wa vina. Hii ina maana kwamba, vina vya kati na mwishoni vinaweza kubainishwa katika wimbo mmoja kama inavyoonekana kwenye wimbo uitwao ‘*Ningalonga Ndauli*’ kama ifuatavyo.:

Mganga: *Ningalonga ndauli* x2,
Wazumi: *Ningalonga ndauli* x2.

Mganga: *Ningalonga ndauli* x2,
Wazumi: *Ningalonga ndauli* x2.

Mganga: *Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lisoka,*
Wazumi: *Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lisoka.*

Mganga: Babu *uunange*, babu *uunange*,
Washiriki: Babu *uunange*, babu *uunange*,
Mganga + Wazumi: *Pa nyumba pana lisoka.*

Mganga: Pana *lisoka*, pana *lisoka*,
Wazumi: Pana *lisoka*, pana *lisoka*,
Mganga + Wazumi: Pana nyumba pana *lisoka*.

Mganga: Babu *uunange*, babu *uunange*, *pa nyumba pana lisoka*,
Wazumi: Babu *uunange*, babu *uunange*, *pa nyumba pana lisoka*.

Chanzo: Uwandani (2017).

Kwa kawaida, vina hutokea mwishoni mwa kipande. Hivyo, kama shairi la kimapokeo lina vipande vitatu, basi na vina hutokea mwishoni mwa kila kipande. Katika wimbo huu, tumeona kuna mchanganyiko wa utokeaji vipande katika mishororo. Kuna kipande kimoja, kuna vipande viwili na vipande vitatu. Uradidi unavyojitokeza katika wimbo ndivyo na vina vinavyojitokeza katika mishororo.

Kwa kutumia wimbo huu wa ‘*Ningalonga Ndauli*’ tunaonesha jinsi vina vilivyojipambanua katika kipande kimoja, vipande viwili na vipande vitatu. Tukianza na kipande kimoja katika mshororo, vina vilivyojitokeza ni kama vifuatavyo:

Mganga: Ningalonga ndauli x2,
Wazumi: Ningalonga ndauli x2.

Mganga: Ningalonga ndauli x2,
Wazumi: Ningalonga ndauli x2.

Mganga + Wazumi: Pa nyumba pana lisoka,
Mganga + Wazumi: Pana nyumba pana lisoka.
Chanzo: Uwandani (2017).

Hii ni mshororo ya kipande kimoja na vina vya **-li** na **-ka** vimejitokeza katika mishororo hiyo. Pili, tunaangalia vina vilivyojitokeza katika mishororo ya vipande viwili kutoka katika wimbo huu.

Mganga: *Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lizoka,*
Wazumi: *Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lizoka.*

Mganga: Babu *uunange*, babu *uunange*,
Washiriki: Babu *uunange*, babu *uunange*.

Mganga: Pana *lisoka*, pana *lisoka*,
Wazumi: Pana *lisoka*, pana *lisoka*.

Kama tunavyoona katika mfano huu vina vilivyojitokeza ni **-li** na **-ka** katika mishororo miwili ya mwanzo. Vilevile, kuna vina **-ka** na **-ka** katika mishororo miwili inayofuata. Mwisho, tunaonesha vina katika mishororo ya vipande vitatu. Kuna ni nyimbo chache sana zenye vipande vitatu vya mishororo. Hivyo, hapa tunaangalia jinsi vina hivyo vinavyojipambanua katika mishororo ifuatayo:

Mganga: Babu *uunange*, babu *uunange*, pa nyumba pana lisoka,
Wazumi: Babu *uunange*, babu *uunange*, pa nyumba pana lisoka.

Katika mishororo hii miwili ya mwisho katika wimbo huu tunaona jinsi vipande vitatu vinavyojitokeza katika mstari mmoja. Katika vipande hivyo vina pia vimejitokeza kutokana na uradidi ulijitokeza katika uimbaji wa wimbo huo. Vina vilivyojitokeza tumevikoleza kwa wino; vina hivyo ni **-nge** na **-ka**. Kwa jumla matokeo ya data yanadhihirisha kukosekana kwa urari vina na mizani katika nyimbo za tiba asili. Matokeo ya utafiti huu yanaafikiana na ya Babalola (1966) aliyechunguza nyimbo za Wayoruba na kubaini kuwa nyimbo zina mtindo wa kishairi unaotumia mizani tofauti tofauti kuibua hisia na mapigo ya ridhimu za kimuziki.

5.3.5 Uchezaji

Miondoko ya uchezaji hujumuisha tabia za kuigiza mwendo au mijongoe ya mwili. Mitindo hii hujidhihirisha kwa fanani pamoja na hadhira kwa kutumia uso, kichwa, mikono au kiungo kingine chochote cha mwili. Katika utafiti huu, mtafiti alishuhudia mitindo mbalimbali ya uchezaji wa nyimbo za tiba asili. Kwanza, mtafiti alishuhudia uchezaji wa Kujiviringisha. Midundo ya ngoma inapokolea na uimbaji kuchangamka wagonjwa na watu wenye pepo hupandisha pepo na kuanza kugaragara kwa

kujivingilisha bila kujali vumbi linalotimka wakati huo. Hali hii ya kujivingirisha huashiria mtu kapandwa na pepo. Hivyo, mgonjwa kupandwa na pepo katika muktadha wa kiuganga hali hiyo hufumbatwa na viashiria vya kiutamaduni. Mganga na wasaidizi wake huanza kutoa tiba kwa watu hao.

Pili, mtafiti alishuhudia mtindo wa uchezaji wa kuzungusha shingo. Uimbaji wa nyimbo za tiba asili huambatana na uchezaji wa kuzungusha shingo kwa nguvu. Katika hali ya kawaida, mtu hawezi kuzungusha shingo kwa nguvu kama inavyoshuhudiwa katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Wachezaji hawa hufanya hayo wakati wamepagawa na pepo. Kutokana na hilo imebanika kwamba, matendo wanayofanya wachezaji hao hayatokani na urazini wao bali ni pepo huyafanya hayo wakati ya nyimbo za tiba asili zinaimbwa. Uzungushaji wa shingo huenda na midundo na miondoko ya wimbo ambao unakuwa unaimbwa.

Tatu, mtafiti alishuhudia mtindo wa uchezaji unaambatanao na kutoa mkono wa shukrani. Katika fasihi simulizi pongezi hutolewa kwa njia mbalimbali. Hii ni moja ya sifa ya fasihi simulizi katika kuipa uhai fasihi husika. Katika ngano msimulizi hupongezwa kwa kupigiwa makofi. Halikadhalika, katika vitendawili, mtegaji kitendawili kisichopatiwa jibu hupongezwa kwa kupendekezewa mji mzuri anaoupenda. Ndivyo ilivyoshuhudiwa katika nyimbo za tiba asili, mmoja kati ya wagonjwa waliopandwa na pepo hutoa mkono wa shukrani kwa washiriki. Kama tulivyofafanua hapo juu kuwa pepo huweza kufurahi kwa midundo ya ngoma na wimbo wa tiba. Furaha yao huikamilisha kwa aina nyingine ya uchezaji. Uchezaji huo ni wa kuzunguka kwa wazumi wote na kuwapa mkono wa pongezi na

kuwashukuru wote walioshiriki katika uimbaji wa nyimbo za tiba. Hii ni ishara kuwa wimbo ulioimbwa na ngoma zinazopigwa zimewafurahisha pepo.

Nne, mtafiti alishuhudia mtindo wa uchezaji wa kuruka kwa kutumia makalio. Uchezaji huu ni wa kipekee na huvutia mtazamaji. Wakati wa uimbaji wa wimbo baadhi ya wagonjwa walianza kucheza kwa kutumia makalio. Huu ndio msingi wa nadharia ya Simiotiki kusisitiza kwamba, utamaduni unaviashiria vya aina mbalimbali vinafungamana na ishara mbalimbali. Kucheza kwa kutumia makalio nako kuna maana yake. Uchezaji wa kurukaruka kwa kutumia makalio hufanyika wakati midundo ya ngoma na uimbaji umekuwa ni wa hali ya juu. Hapo baadhi ya wazumi huanza kucheza kwa kufuata midundo ya ngoma. Mtindo huo kwa macho ya kawaida lazima uone mchezaji anaumia lakini kwa kuwa mchezaji hutumii urazini wake huwa hapati maumivu yoyote, lakini baada ya pepo kutolewa ndipo mchezaji huyo huwa na maumivu ya viungo.

Tano, mtafiti alishuhudia pia mtindo wa kucheza hadi kudondoka na kupoteza fahamu. Wakati wa kuimba na kucheza nyimbo za tiba asili kuna kitu cha tofauti na cha kushangaza kilishuhudiwa ambacho hutokea kwa baadhi ya wazumi. Wazumi hao hucheza wimbo unaoimbwa kwa muda na baada hapo hudondoka chini na kupoteza fahamu. Katika mazingira ya kawaida, mtu akidondoka na kupoteza fahamu, ingekuwa ni jambo la kutisha sana, lakini katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili kitu hicho kinachukuliwa ni cha kawaida.maalumu. Huchukuliwa kwamba, aliyedondoka amedondoka na kulala, na kuwa, haitamletea athari kiafya, kama kukosa hewa au kuanguka sehemu ambayo ni hatari. Wazumi hao huanguka na

baada ya muda huamka na kuendelea kushiriki matendo ambayo yatakuwa yanaendelea.

Sita, mtafiti alishuhudia mtindo wa kucheza kwa kuweka mikono kichwani Mitindo ya uchezaji hutofautiana toka aina moja ya wimbo na nyingine katika jamii za Kiafrika. Katika nyimbo za tiba asili kuna uchezaji wa kuweka mikono kichwani huku mchezaji akiwa amekaa chini au hutembea kutoka sehemu mmoja hadi nyingine kwa kutumia makalio na mkono ikiwa kichwani. Mchezaji hutoka upande mmoja kwenda upande mwingine huku akiwa na lengo la kukamilisha duara. Mchezaji huyu hufanya hivi kutokana na kupandwa na hisia ambazo atakuwa amezipata kutokana na wimbo unaoimbwa. Nadharia ya Simiotiki inabanisha ishara hiyo inakuwa imefumbatwa na maana ambapo mganga mmoja aliyehojiwa alisema mgonjwa akicheza hivyo inaonesha kuwa ana mzigo ameubeba; yaani, ana matatizo hivyo anaomba msaada wa kuyaondoa. Mganga akiona hivyo huanza kumpa tiba kulingana na ugonjwa au tatizo atakalokuwa ameligundua.

Saba, mtafiti alishuhudia mtindo wa kucheza kwa kuongeza kasi kadiri kupagawa kunavyoongezeka. Miondoko ya uchezaji katika nyimbo za tiba asili kwa kawaida hufuata midundo ya ngoma na wachezaji hucheza kwa kufuata midundo hiyo bila kuwa na aina moja ya uchezaji. Hata hivyo, kadiri uimbaji na uchezaji unavyoendelea ndivyo kasi ya uchezaji isiyo ya kawaida kwa wazumi waliopandwa na mzuka huongezeka.

5.3.6 Utendaji wa Kimuziki

Mitindo ya utendaji wa kimuziki ina nafasi kubwa katika uwasilishaji wa ujumbe na maana katika nyimbo za fasihi simulizi ya Kiafrika. Niane (1995) anasema, muziki ndio uti wa mgongo wa waimbaji katika fasihi simulizi. Umuhimu wa muziki katika fasihi simulizi ya Kiafrika upo katika kuchochea hamasa za ushiriki wa watendaji pamoja na kukoleza ujumbe unaowasilishwa katika fasihi hiyo. Hivyo, mfungamano wa muziki na nyimbo za Kiafrika unapatikana katika utendaji wake. Mapigo ya kimuziki yana dhima kubwa katika kusisitiza ujumbe wa nyimbo. Muziki huufanya ujumbe ueleweke vyema na kuufanya utendaji mzima uvutie.

Okpewho (1992) anasema, kulingana na mfungamano baina ya maana na sauti zinazojitokeza katika nyimbo, ni dhahiri kuwa, matini simulizi inaathiriwa na mitindo ya utendaji wa kimuziki. Hivyo, ili utendaji wa fasihi simulizi ufanikiwe, muziki na maneno yanayotamkwa katika nyimbo vinahitajika viwe na muwala maalumu.

Katika uwasilishaji wa tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kwa kiwango kikubwa hadhira pamoja washirika wengine huupata ujumi wa fasihi hiyo kutokana na kiwango cha ubora wa sauti za kimuziki zinazosikika wakati wa kuimba na wakati wa kutumia ala za kimuziki. Mubina (1997) anaeleza kuwa, utendaji wa nyimbo za fasihi simulizi ya jamii nyingi za Kiafrika unaambatana na matumizi ya aina mbili za muziki. Kuna muziki utokanao na ala za kimuziki na pia kuna muziki utokanao na sauti mbalimbali za mitindo ya uimbaji. Katika sehemu ifuatayo tumejadili aina za utendaji wa kimuziki kwa kurejelea utendaji wa nyimbo za tiba asili za mkoa wa Ruvuma.

5.3.6.1 Muziki wa Ala

Kuna ala mbalimbali za muziki hutumika katika utendaji wa nyimbo za tiba asili. Nadharia ya Simiotiki inafafanua kuhusu matumizi ya viashiria vya utamaduni katika kazi za fasihi, viashiria hivyo vya kitamaduni ni pamoja na ala za muziki. Katika nyimbo za tiba asili ala maarufu ni nyanga, ngoma na vipande vya vyuma. Waganga ambao tumefanya nao mahojiano walisema:

“Bila nyanga uimbaji wa nyimbo za tiba asili unakuwa haujakalika. Vilevile, wanasisitiza kuwa, ngoma ni kifaa muhimu; bila ngoma utashindwa kufanya ibada kwa mizimu” (Mtafitiwa 5: Mahojiano yalifanyika, 22. 08. 2017).

Dhana ya ngoma katika tiba asili ipo ya aina mbili. Kwanza, ngoma ni kifaa kitumikacho kutoa sauti baada ya kupigwa na huandaliwa/hutengenezwa kwa kuwambwa ngozi katika kifaa kama ndoo, debe, pipa hata kipande cha mti (gogo) ambacho kimeandaliwa maalumu kwa ajili ya kuunda ngoma. Dhana ya pili ya ngoma kwa muktadha wa uganga wa tiba asili ni tendo la kualika watu katika tendo la kupiga ngoma inayoambatana na uimbaji, uchezaji na utoaji wa sadaka kwa mizimu. Tendo hili kila mganga hulifanya lakini hutofautiana. Wapo ambao hufanya mara moja kwa mwaka na wapo wafanyao mara kwa mara.

Dhana hii ya pili hufungamana na matendo mengine ya upigaji ngoma (uimbaji) kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali. Hivyo, katika sehemu hii tunaangalia ngoma kama kifaa kinachotumika katika kutoa ala ya sauti katika nyimbo za tiba asili. Katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili ngoma ni kifaa muhimu katika kutoa midundo ambayo hutia hamasa zaidi ya kucheza. Mganga tuliyehojiana naye alielezea kuwa ngoma ni kifaa muhimu katika uimbaji wa nyimbo zinazotumika

katika kutoa tiba, nyimbo za kufurahisha mizimu, nyimbo za shukrani na nyimbo za kuomboleza. Anasema:

“Mdundo na ngoma hutumika kuamsha na kusogeza mizimu ya mgonjwa”. “Mizimu inapenda sana ngoma kiasi kwamba, mgonjwa anaweza akawa amefikishwa akiwa hajiwezi, lakini anaweza kupigiwa ngoma akapona kabisa bila kutumia dawa yoyote” (Mtafitiwa 6: Mahojiano yalifanyika, 27. 08. 2017).

Ala nyingine ni manyanga. Hiki ni kifaa ambacho hutengenezwa kwa kutumia kopo la bati na kuwekewa mshikio wa mti. Ndani yake huwekwa kokoto au mbegu za mimea ili iweze kutoa sauti pindi kopo hilo litakapotikiswa. Katika utafiti huu ilishuhudiwa manyanga kutumika katika aina zote za nyimbo. Mara nyingi, nyimbo za tiba asili zipo ambazo hazitumii ngoma, lakini hakuna nyimbo ambazo zinakosa kutumia manyanga. Katika mahojiano, mmoja wa waganga alieleza:

“Manyanga ni kifaa muhimu kwa kuwa kinatumika kutoa ala katika nyimbo za aina zote. Manyanga pia ni ala ya aina ya kwanza kuanza kupigwa kabla ya ngoma; na ala ya kwanza kuanza kupigwa kabla ya ngoma na kabla ya ala nyingine kuanza kupigwa. Hivyo, manyanga hujulikana kama ala tangulizi” (Mtafitiwa 7: Mahojiano yalifanyika, 22. 08. 2017).

Manyanga hutumika katika ngoma zote kama ilivyoelzwa hapo awali lakini huwa tegemeo zaidi katika nyimbo hizo kwa sababu katika nyimbo za maombi ala inayotumika ni manyanga tu na hadhira hutumika kupiga makofi. Vipande vya vyuma hutumika kunogesha ala nyingine za muziki katika nyimbo za tiba asili. Vipande vilivyoshuhudiwa uwandani ni kipande cha jembe bovu na kipande cha nondo ambavyo kwa pamoja hutumika kwa kugongesha kipande kimoja na kingine. Mahojiano yetu na waganga kuhusu matumizi ya ala hizi wengi walieleza kwamba:

“Ala hii huvutia watu. Ugongaji wa kipande hicho hufanyika kwa utaratibu maalumu ili kunogesha tendo la uimbaji” (Mtafitiwa 8: Mahojiano yalifanyika, 03. 08. 2017).

Ala hizi zote ni vigumu kuweka milio yake hapa hutumika kunogesha uimbaji wa nyimbo za tiba kwa kushirikiana na vionjo vingine vya mwili kama vile kupiga makofi na mijongeo kama kucheza kwa kukanyaga ardhi kwa kishindo. Katika upigaji wa ala hizi za muziki wapigaji wa ngoma huwa watu maalumu ambao wapo kwa shughuli hiyo. Wapo wapigaji ambao hukodiwa na wapo wale ambao ni maalumu. Hao huishi kwa mganga au wagonjwa ambao wamepata ujuzi wa kupiga ngoma hapo kwa mganga. Kwa upigaji wa manyanga, mtu yoyote hupiga manyanga kwa kuwa hayahitaji utaalumu kama ilivyo ngoma. Matumizi ya ala hizi za muziki yameanza miaka mingi katika mkoa wa Ruvuma. Aidha, ala hizi bado ni kiasili. Hii inaonesha jinsi ambavyo nyimbo hizi za tiba asili hazijapata athari za matumizi ya ala za kisasa kama tarumbeta.

5.3.6.2 Muziki wa Sauti za Uimbaji

Sauti za uimbaji zina nafasi kubwa katika utendaji wa nyimbo za tiba asili. Mojawapo ya dhima zake ni kusaidia kutoa mapigo ya kimuziki wakati wa uwasilishaji wa nyimbo. Sauti za waimbaji ni moja ya ishara, ambayo nadharia ya Simiotiki inaaita ni ishara katika mpangilio wa matukio. Sauti hizo huwa na kazi mbalimbali mojawapo ni kuvuta umakini wa hadhira pamoja na kusisitiza ujumbe unawasilishwa kwa hadhira. Kadhalika, muziki wa sauti una dhima ya kuutambulisha muktadha wa utendaji baina ya fanani na hadhira. Kwa ujumla, ujumi wa utendaji wa nyimbo za tiba asili unaimarishwa kwa kutumia vipashio mbalimbali vya muziki wa sauti za waimbaji kama vile mifumo ya uimbaji wa nyimbo, ubora wa sauti, mawimbi ya sauti na toni. Vipashio vyote hivi husaidia kukoleza na kunogesha

fani na maudhui ya nyimbo za tiba asili. Uimbaji wa nyimbo za tiba unafanywa kwa kufuata mfumo wa mwitikio.

Kulingana na mfumo huu suala la uimbaji linategemea ushirikiano baina ya mwimbishaji na waitikiaji wake. Wimbo mmoja unakuwa na mwimbishaji mmoja tofauti na baadhi ya nyimbo toka katika fani nyingine zinaweza kuwa na waimbishaji zaidi ya mmoja. Mwimbishaji atakayeimbisha aina fulani ya wimbo inategemea dhima ya wimbo, kwani wimbo utakaoimbishwa na mganga utakuwa tofauti na wimbo utakaoimbishwa na mgonjwa. Mganga huimbisha nyimbo wakati wa tiba na wagonjwa mara nyingi huimbisha zile za kupeana faraja na kuliwazana hasa katika maombolezo. Ifuatayo ni mifano wa nyimbo zilizoimbishwa na mganga na mgonjwa. Wimbo wa ‘*Sina Wema*’ ulioimbishwa na mganga akiuhoji mzimu kuwa umekuja kufanya nini? Dhima hii ya wimbo haiwezi kutumika kwa mgonjwa kwa kuwa hawezi kujua hata aina ya mzimu kama ulivyooneshwa:

Mganga: Sina wema umekuja kufanya nini,
Wazumi: Kuokoa kuoa.

Mganga: Kuokoa binadamu,
Wazumi: Kuokoa kuoa.

Mganga: Kuokoa wenye homa,
Wazumi: Kuokoa kuoa.

Mganga: Sina wema,
Wazumi: Kuokoa kuokoa.

Mganga: Chonde chonde,
Wazumi: Kuokoa kuokoa.
Chanzo: Uwandani (2017).

Wimbo ufuatao umeimbwa na wagonjwa ukiwa na dhima ya kuelezea tabu wanazozipata kutokana na majini. Hivyo, wanasisitiza kuomba zaidi kama wimbo wa ‘Tuombe’ unavyoeleza:

- Kiongozi: Wee tuombe daima,
Aee daima,
Na majini wa milimani tabu sana,
Aee daima.
- Wazumi: Wee tuombe daima,
Aee daima,
Na majini wa milimani tabu sana,
Aee daima.
- Kiongozi: Tuimbe wote daima aee, baba,
na majini wa milimani tabu leo,
Aee daima.
- Wazumi: Tuimbe wote daima aee, baba,
na majini wa milimani tabu leo,
Aee daima.
- Kiongozi: Ena ena daima,
Aee daima,
Na majini ya milimani tabu sana.
- Wazumi: Tuimbe wote daima aee, baba,
Na majini wa milimani tabu leo,
Aee daima.
- Kiongozi: Tuombe na mababu,
Aee daima,
Na majini ya milimani tabu sana.
- Wazumi: Tuombe na mababu,
Aee daima,
Na majini ya milimani tabu sana.
Chanzo: Uwandani (2017).

Mwimbishaji ndiye mwenye mamlaka ya kutoa aina ya wimbo kulingana na aina ya tukio. Pia, ndiye mwenye mamlaka ya kuchagua mfumo wa uimbaji. Anaweza kuanzisha uimbaji kwa kutumia mawimbi ya juu, kati au chini kutegemeana ujumbe

anaotaka kuuwasilisha wakati huo. Wimbo wa ‘*Ubaya*’ ulishuhudiwa ukianzishwa kwa sauti ya chini kutokana na ujumbe wa masikitiko ulioubeba:

Kiongozi: Ubaya wee, ubaya wee,
Binadamu ubaya, uache ubaya,
Wazumi: Ubaya wee, ubaya wee,
Binadamu ubaya, uache ubaya.

Kiongozi: Uache ubaya,
Wazumi: Ubaya, mwanadamu, ubaya,
Kiongozi: Uache ubaya,
Washiriki: ubaya, mwanadamu, ubaya.
Chanzo: Uwandani (2017).

Kwa upande mwingine, mapigo ya kimuziki katika nyimbo za tiba asili yanapata uhai wake kutokana na ushiriki wa hadhira. Hadhira inaweza kuitikia kwa kukaririwa maneno yaliyotamkwa na fanani bila kubadili chochote au kukariri baadhi ya maneno ya fanani. Wimbo wa ‘*Chonde*’ unaonesha kaida ya kupokezana katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili kama ilivyoshuhudiwa

Mganga: Aaee, eee, aaee, eee, aaee,
Wazumi: Aaee, eee, aaee, eee, aaee.

Mganga: Chonde, eee, chonde, eee,
Chonde, eee, chonde, eee, malaika, aaee,
Wazumi: Aaee.

Mganga: Tusaidie tupate dawa, dawa za majini,
Dawa za mti mkubwa, dawa za pangoni,
Dawa za milimani.

Wazumi: Aaee,
Chanzo: Uwandani (2017).

Uteuzi wa mfumo wa uimbaji haufanyiki kiholela bali unatokea kulingana na mikakati ya kiuwasilishaji katika muktadha mahsusi wa kiutendaji. Fanani wa nyimbo za tiba asili huamua kutumia mfumo wa aina fulani ya sauti kulingana na mahitaji ya wakati huo. Kuna sauti ya wakati wa kuimba wimbo wa kuomboleza au

wimbo wa tiba. Sauti hizo hutofautiana kulingana na tendo linalohusika. Katika kuomboleza sauti zinakuwa chini na zenye kutia huruma kwa wazumi.

5.3.7 Sauti za Waimbaji

Uimbaji wowote unakuwa na sauti za mahadhi ya kupanda na kushuka katika mpangilio maalumu ulioandaliwa au uliozoeleka. Hapa tunakusudia kuonesha sauti zinazoashiria maumivu, furaha na mazungumzo ya wazumi kutokana na kupagawa baada ya kupandwa na mizimu.

Kwanza, kuna sauti za Maumivu za waimbaji. Nyimbo za tiba zinapoimbwa, sauti huwavuta watu mbalimbali. Wagonjwa walioko nyumbani huvutwa na kwenda kushiriki. Watu wenye matatizo mbalimbali huanza kupaza sauti za kupagawa kuelezea matatizo yao. Uelezaji wa matatizo kwa wagonjwa hasa waliopagawa na pepo hufanyika kwa kutoa sauti za maumivu au kuonesha kwa ishara sehemu zenye maumivu makali zinazowasumbua. Mtafiti alishuhudia baadhi ya wagonjwa wakiwa wanatambaa huku wakigugumia kwa maumivu. Sauti za viguno, malalamiko, vilio na yowe ziliashiria hali ya maumivu. Mganga mmoja wapo wakati anahojiwa kuhusu hali hiyo alisema:

“Hao wanaolalamika maumivu wanakuwa wamerushiwa pepo wabaya ambao wanawatesa wagonjwa. Sauti za nyimbo na mdundo wa ngoma ndio zinawafanya wagonjwa wasogee karibu huku wakigumia kwa maumivu” (Mtafitiwa 9: Mahojiano yalifanyika, 22. 08. 2017).

Dondoo ya hapo juu inaonesha kuwapo kwa sauti zinazojirudia ambazo zinaashiria maumivu hivyo kufanya kipengele muhimu cha mtindo.

Pia, nyimbo hizo zinapoimbwa pepo huwapanda baadhi ya watu wenye pepo na kuanza kuwaadhibu kwa makosa mbalimbali waliyoyafanya. Adhabu huwa za aina tofauti tofauti. Pepo huweza kuwafinya na kuwapiga wagonjwa hao ambao wanakuwa hawajatimiza baadhi ya maelekezo toka kwa pepo hao. Yote haya yanatokea wakati wimbo unaimbwa hadi wimbo unapomalizika, ambapo mazungumzo na sauti za maumivu huendelea kwa baadhi ya wagonjwa. Mganga ndiye mwenye jukumu la kutuliza ama kutibu tatizo linalomsibu mgonjwa. Tiba mojawapo ni kuuliza pepo hao wanahitaji nini ili wasiendeele kumtesa mgonjwa. Pepo hubainisha mahitaji yake kwa wakati huo. Yanayoweza kutimizwa hutizwa na yanayohitaji maandalizi zaidi hufanyika baada ya maandalizi kukamilika. Moja ya mahitaji yanaweza kuwa udi au vazi lenye rangi maalumu ambayo pepo atakuwa anaihitaji.

Pili, kuna Sauti za Furaha. Sauti za furaha ni kipengele kingine cha kimtindo kinachojitokeza katika nyimbo za tiba asili. Sauti hizi zinachochewa na hali mbalimbali. Mtafiti alishuhudia sauti za furaha zikiwa zinajitokeza kutoka kwa wagonjwa waliopagawa na miongoni mwa wazumi baada ya tiba kukamilika. Uimbaji na uchezaji wa nyimbo za tiba asili huambatana sauti za furaha zinazojirudia, kwa mfano vigelegele, nderemo, vifijo, mbinja, ushangiliaji na vicheko hujitokeza wakati wa uimbaji. Sauti za furaha pia hujitokeza. Tunasema za pekee kwa kuwa ni tofauti na sauti za furaha zinazopatikana katika uimbaji wa nyimbo nyingine. Sauti hizi huwa na vicheko toka kwa wagonjwa waliopandwa na kupagawa na pepo wakati wa uimbaji na baada ya wimbo kuisha vicheko hutokea pale ambapo wimbo unakuwa umefurahisha pepo. Pia, vicheko na sauti nyingine za

furaha hutokea pale ambapo pepo anakuwa ametimiziwa mahitaji yake aliyokuwa anayahitaji, kama kumechomewa ubani au kupewa nguo aliyokuwa anaihitaji. Pepo hutoa shukrani na kuomba aimbiwe wimbo wa kumuomba aondoke.

Zaidi ya hayo, kuna matumizi ya Sauti za Kuzungumza. Kuna wakati wimbo unaweza kukatishwa na baadhi ya waimbaji wanaweza kuanzisha mazungumzo. Mtafiti alishuhudia wimbo ukikatishwa ghafla na mgonjwa aliyepandwa na pepo akaanza kuzungumza na mganga. Mazungumzo yalikuwa hivi:

(Sauti ya kupandwa na pepo inasika toka kwa mgonjwa)

Mgonjwa: Tunaomba udi *(Kicheko kinasikika toka kwa mgonjwa)*.

Mganga: *(Anatoa maagizo)* Mpe udi.

Mgonjwa: *(Anaimba wimbo)*,
Twendeni jamani eee,
Twendeni tucheze ngoma *(Hakuna anaaitikia.*
Anatoa sauti ya kupandwa na pepo),

Mganga: *Anawaambia pepo)* Haya mpunguzieni adhabu
Mwenyewe huyo mambo mnayofanyia sio mazuri. Kama mjukuu amekosea ndio mmtandike adhabu kiasihiki?

Mgonjwa: (Sauti ya pepo) Tumemfinya, tumemfinya...
(Mtafitiwa 10: Mahojiano yalifanyika, 25. 08. 2017).

Dondoo hii inaonesha dhahiri kuwa mtindo wa mazungumzo unajitokeza ghafla wakati utendekeji wa wimbo unaendelea. Baada ya mazungumzo kama hayo, mtafiti alishuhudia wazumi wakiwa wanaendelea kuimba tena.

5.3.8 Maleba na Vifaa

Kuna maleba na vifaa anuwai vitumikavyo katika nyimbo za tiba asili za mkoa wa Ruvuma. Maleba ni aina ya mavazi maalumu yanayovaliwa na fanani na hadhira katika utendaji wao wa fani inayohusika. Mara nyingi maleba yanahusishwa na

uigizaji wa sanaa za maonesho na tamthilia. Maleba na vifaa hivyo ni viziadalugha. Hivyo, kwa kutumia mhimili wa uchambuzi wa viziadalugha na nadharia ya Simiotiki tumechambua data na kuonesha matokeo yake. Katika utafiti wetu, tumegundua kuwa, waimbaji wa nyimbo za tiba asili huvaa maleba na pia hutumia vifaa mbalimbali katika kukamilisha utendaji wa tendo hili. Matumizi ya maleba na vifaa ni njia ya kufikisha ujumbe kwa ishara maalumu.

Fanani na hadhira katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili ndio ambao huvaa maleba na kutumia vifaa maalumu. Fanani wa nyimbo za tiba asili ni mganga ambaye kwa kiasi kikubwa ndiye ambaye anaimbisha na kutenda/kuongoza matendo mengi katika fani hiyo. Hadhira ya nyimbo za tiba asili ni waganga wasaidizi, wagonjwa, wapiga vifaa (ngoma na vifaa vingine), watazamaji na wauguzi. Hadhira hii nayo ina nafasi ya kuimbisha nyimbo. Kuna wakati fanani atakuwa mmoja wa wasaidizi wa mganga au mgonjwa mmoja.

Hii inategemea na tendo linaloambatana na nyimbo zinazohusika. Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki tunachambua kipengele hiki cha maleba na vifaa vitumiavyo katika kuimba nyimbo za tiba asili ni kipengele kinachotoa ujumbe kwa njia ya lugha ishara ni mavazi pamoja na vifaa vingine. Mavazi yanayotumika ni kaniki, nguo za rangi mbalimbali, mfano nyekundu na njano.

Vingine ni kanzu na barakashia. Vifaa vilivyoshuhidiwa uwandani vinavyoambatana na upigaji ngoma ni mkuki, *kinyenge* (kishoka), *kibonga* (kirungu), nyanga, shanga, mkia wa nyumbu na fimbo maalumu. Vitu vyote hivi, kutumika katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili wakati wa tendo la kutoa tiba likiwa linaendelea. Kila kifaa kina

mchango wake katika tendo la uimbaji linalofungamana na utoaji tiba kama nadharia ya Simiotiki inavyoeleza katika msimbo wa kiutamaduni kuwa kuna viashiria vya utamaduni ambavyo huunda uhalisi mahsusi katika jamii.

5.3.8.1 Mavazi Kulingana na Makundi

Nyimbo ni sehemu ya ushairi simulizi. Katika ushairi simulizi mavazi ni sehemu ya mtindo kwasababu yanateuliwa kuendana na wimbo husika. Katika utafiti huu dhana ya mtindo imepanuliwa kutoka kwenye mawanda finyu ya kimapokeo hadi kuhusisha matendo, mavazi kwa jumla viziada lugha kuwa sehemu ya mtindo katika fasihi simulizi. Kutokana na matumizi ya mitindo ya mavazi pamoja na aina za mavazi tumefanikiwa kubainisha makundi mbalimbali ya washiriki wa nyimbo za tiba. Nadharia ya Simiotiki kwa kutumia msimbo wa matukio na muktadha imetumika kuchambua makundi mbalimbali kulingana utendaji kazi wake. Kwa kuanza tumeanza na fanani ambao wamegawanyika kulingana na aina za nyimbo kama tulivyoeleza hapo awali kuwa kuna aina saba za nyimbo ambazo zimegawanywa katika sehemu mbalimbali. Hivyo, hata fanani pia wamegawanyika, ingawa mganga ndiye anayejitokeza zaidi katika nafasi ya kuwa fanani. Wapiga ngoma, ni muhimu sana katika nyimbo za tiba asili kwa kuwa bila wao ladha ya nyimbo hupungua. Hata hivyo, si nyimbo zote zinazotumia ngoma; nyimbo nyingine hutumia manyanga peke yake.

Wagonjwa ni kundi jingine ambalo nalo hushiriki katika nyimbo za tiba asili. Hili ndilo kundi ambalo nyimbo hizi zimelilenga. Bila wagonjwa kusingekuwa na nyimbo za tiba asili. Wasaidizi wa mganga ni kundi jingine ambalo nalo linajitokeza

katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Kundi jingine ni wauguzi wa wagonjwa. Hao ni kundi jingine ambalo nalo linajitokeza katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Makundi haya tumeyabainisha kwa namna yanavyojipambanua katika uchezaji kutokana na mitindo ya mavazi katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Makundi haya yanatofautiana katika mitindo ya mavazi.

Kwanza kuna mavazi ya Mganga. Mganga hapa tunamuita fanani mkuu. Tumemuita hivyo kwa kuwa amejitokeza katika aina nyingi za nyimbo za tiba asili kama kiongozi, ingawa kuna baadhi ya nyimbo hawi fanani, bali anakuwa msikilizaji au hutokea endapo tatizo linakuwa limetokea. Mavazi ya mganga yanatofautiana na wagonjwa. Tofauti hii ni kutokana na ukweli kwamba mganga ndiye kiongozi katika shughuli nzima ya uimbaji. Katika mahojiano tuliyofanya na waganga wanasema kuwa:

“Mavazi wanayovaa hutofautiana rangi kutokana na shughuli anayoifanya pia mahitaji ya mzimu aliyempanda. Mavazi hayo huwa na rangi tofauti, mfano rangi ya njano, nyeusi au nyekundu” (Mtafitiwa 11: Mahojiano yalifanyika, 17. 08. 2017).

Utofauti wa rangi ni ishara ambayo katika nadharia ya Simiotiki ichambua kuwa rangi hutofautiana kwasababu ya mhusika, tukio na mandhari. Mavazi haya huvaliwa kutokana na mahitaji ya mizimu iliyompanda mganga hapa mhusika ni mganga. Mganga mmoja anaweza kuwa na mzimu zaidi ya mmoja na kila mzimu unakuwa na mahitaji ya rangi yake ili uweze kutoa tiba kwa mgonjwa husika.

Pili, kuna mavazi ya wapiga ngoma. Katika utafiti huu, tumeshuhudia wapiga ngoma wakiwa katika mavazi mchanganyiko. Lakini, pia wapo ambao huvaa mavazi

maalumu yenye rangi kulingana na mahitaji ya mzimu au huvaa nguo nyeusi. Wakati mwingine huvaa nguo za kawaida. Wapiga ngoma kuna wakati huwa ni kikundi kilichokodiwa kwa ajili ya kupiga ngoma. Kuna kikundi chenye mavazi maalumu na kingine huwa hakina mavazi maalumu. Pia, kuna kikundi ambacho huwa kinaishi kwa mganga. Kikundi hiki huwa na mavazi maalumu. Mavazi katika vikundi vya sanaa huwakilisha utamaduni wa jamii husika. Hivyo, mavazi katika nyimbo za tiba asili hubeba ujumbe maalumu kulingana na mahitaji.

Tatu, kuna mavazi ya wagonjwa. Katika utafiti huu, tumeshuhudia wagonjwa wakiwa wamevaa nguo maalumu. Uvaji huu wa mavazi maalumu kwa maelezo ya waganga baada ya kuhojiana nao ni kutokana na mahitaji ya mizimu, kwani kila mgonjwa anatimiza hitaji la mzimu wake. Mizimu ya wagonjwa hutofautiana kutokana na mila ya mgonjwa husika au mzimu uliompenda. Mizimu huwa na mahitaji tofauti ya aina za nguo hasa rangi. Kuna mizimu inayopenda rangi ya njano, pia rangi nyeusi. Rangi ni kiSimiotiki ni ishara zina maana kulingana na mizimu husika. Mavazi kwa wagonjwa hutofautiana kutokana na aina ya nyimbo zinazoimbwa na tukio linalotendeka. Endapo kutakuwa kunaimbwa nyimbo za tiba basi mgonjwa atavaa kwa ajili ya nyimbo husika. Pia, endapo atakuwa katika nyimbo za maombolezo, basi atavaa nguo za maombolezo. Mavazi ni maleba katika fasihi ambayo yanabeba ujumbe katika kazi ya kifasihi.

Nne, kuna mavazi ya wasaidizi wa mganga. Hao ni watu muhimu ambao tuliwashuhudia katika utafiti huu. Hawa pia huwa na mavazi maalumu katika uimbaji, wasaidizi hawa huvaa nguo nyeusi (kaniki). Nguo hizi huzivaa wakati wa

kuimba nyimbo za aina mbalimbali ili mizimu iweze kupoa maombi yanayofanyika kwa njia ya nyimbo. Katika mahojiano na waganga wengi walieleza kwamba:

Kaniki ni vazi ambalo mizimu hulipenda zaidi. Vazi hili limekuwa na historia ndefu katika tiba asili. Pia, hutumika katika shughuli nyingi za masuala ya mila na desturi. Vilevile, vazi hili la kaniki limekuwa likihusishwa na masuala ya uchawi na ushirikina lakini watu wasilichukulie kwa mtazamo hasi vazi hili, bali walipe heshima na kulithamini kama vazi la asili, na si vinginevyo (Mtafitiwa 12: Mahojiano yalifanyika, 28. 08. 2017).

Hivyo, utafiti huu umebaini umuhimu wa mavazi (maleba) haya kama sehemu ya mtindo katika nyimbo za tiba asili.

Tano, kuna mavazi ya wauguzi. Katika ushuhudiaji tumeshuhudia wauguzi ni moja ya washiriki muhimu katika nyimbo za tiba asili. Ushiriki wao unakwenda sambamba na uvaaji wa maleba ya kifasihi. Mara chache wauguzi huvaa nguo zinazofanana na wagonjwa wao au vilemba vyenye rangi inayofanana na nguo za wagonjwa. Mara nyingi hawana sare au nguo maalumu. Baadhi ya waganga huwa na sare maalumu wakati wa uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Vazi hilo maalumu huweza kuvaliwa na ndugu wa wagonjwa. Vazi maarufu ni kaniki. Uvaaji wa vazi hili maalumu huwa tofauti kati ya wanaume na wanawake. Mara nyingi sare katika vikundi zinawahususha wanawake kwa kuwa wanaume huvaa nguo za kawaida. Katika uvaaji wa vazi hili huwa kuna mtindo wa ufungaji kibwebwe. Ufungaji kibwebwe huwa ni maalumu katika unogeshaji wa uchezaji. Mchezaji aliyevaa kibwebwe huvutia zaidi kuliko asiyefunga kibwebwe. Kibwebwe huonesha unenguaji zaidi kuliko yule asiyefunga kibwebwe. Hivyo kibwebwe ni moja ya mtindo unaoatana na nyimbo za tiba asili.

Kwa hiyo, katika utendaji wa nyimbo za tiba asili kuna mavazi maalumu yanayo valiwa na fanani na wazumi. Mavazi haya yamegawanyika kulingana na jinsi yaani yapo ya wanawake na pia ya wanaume. Wanawake huvaa zaidi mavazi maalumu tofauti na wanaume. Vilevile, umaalumu wa mavazi hutegemea tendo linalotendeka katika uimbaji wa nyimbo hizo. Umaalumu wa mavazi hutokana na aina ya mizimu na mahitaji ya mzimu husika. Pia, tumbaini kwamba, si wazumi/washiriki wote huwa na mavazi maalumu. Wauguzi wa wagonjwa si lazima kuwa na mavazi maalumu.

Kwa ujumla, mitindo ya uvaaji katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili kiishara unaakisi mfumo wa maisha ya jamii husika. Huwa hairuhusiwi kuvaa mavazi yasiyo na heshima kama vile nguo zenye kuonesha sehemu za siri au nusu uchi. Mavazi ya waimbaji wa nyimbo za tiba asili na nyimbo nyingine za tiba asili hayajapata athari toka nje ya jamii hii. Hivyo, mila na desturi zimeshikiliwa. Katika mahojiano tuliyo fanya na mganga mmojawapo wa tiba asili alikuwa na haya ya kueleza:

“Tunaendelea kuvaa mavazi yetu ya asili wakati wa kuimba nyimbo za tiba asili kulingana na mila ili mizimu iendelee kutoa tiba na endapo utakiuka mila hizo mizimu hutoa adhabu mbalimbali kama vile kukupiga, kukupa homa kali ambayo itakufanya ushindwe kutoa huduma na hata kushindwa kufanya shughuli za kukuingizia kipato. Pia nguvu za kutibu zinaweze kupungua au kutoweka kabisa” (Mtafitiwa 13: Mahojiano yalifanyika, 18. 08. 2017).

Katika dondoo ya hapo juu ni dhahiri kwamba kunakuwa na uteuzi wa mahsusni wa mavazi yanayoendana na wimbo wa tiba asili unaoimbwa kwa wakati unaohusika. Katika muktadha huo ni maantiki kuchukulia kwamba, mavazi ni sehemu ya mtindo katika nyimbo za tiba asili.

5.3.8.2 Vifaa vya Uimbaji

Kipengele kingine cha mtindo kilichobainishwa katika utafiti huu kuwa kiziada lugha ni vifaa vya uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Katika kuipa uhai fasihi simulizi vifaa ni vitu muhimu. Vifaa vitumikavyo katika fasihi simulizi huendana na mazingira halisi na mahitaji ya jamii husika. Vifaa pia huonesha asili ya jamii inayovitumia. Vifaa hubeba taswira na ishara nzito ya tendo husika. Vifaa hivi tunaviita viziada lugha kwa kuwa vinabeba ujumbe katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Hapo ndipo mhimili wa uchambuzi wa viziada lugha unapotumika katika uchanganuzi wa data. Vifaa vinavyotumika katika utendaji wa nyimbo za tiba asili katika mkoa Ruvuma ni pamoja na ngoma, mkuki, *kinyenye*, *kibonga*, nyanga, shanga, mkia wa nyumbu na fimbo maalumu ya mpingo.

Ngoma ni moja kati ya vifaa muhimu katika utendaji wa nyimbo za tiba asili, ingawa si nyimbo zote hutumia ngoma. Zipo ngoma za aina mbalimbali kulingana na maumbo yake. Kuna ngoma kubwa na kuna ngoma ndogo. Pia kuna ngoma ndefu na kuna ngoma fupi. Maumbo ya ngoma hufanya milio yake kutofautiana. Kuna zinazotoa sauti/mdudo mzito na zipo zinazotoa sauti/mdundo mwepesi. Upigaji wa ngoma hutegemea mahadhi ya wimbo. Wimbo ukiwa na mahadhi ya taratibu basi na midundo huwa ya taratibu, bali wimbo ukiwa na mahadhi ya haraka basi na mapigo yatakuwa ya haraka. Wakati mwingine, dhamira ya wimbo huamua upigaji wa ngoma. Mfano, wimbo wa kuomboleza huwa na mapigo tofauti na wimbo wa shukrani kwa mizimu. Wimbo wa kuomboleza huwa na mapigo ya taratibu ilhali wimbo wa shukrani huwa na mapigo ya haraka na waimbaji huimba kwa furaha.

Vifaa vingine ni silaha za jadi kama vile mkuki, kishoka na kirungu. Silaha hizi za hutumika kama ishara maalumu wakati wa uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Kama inavyofahamika tiba asili ni tiba ya jadi hivyo matumizi ya vifaa hivi katika tendo la uimbaji ni moja ya udumishaji wa mila na desturi. Mkuki katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili huchomekwa katikati ya duara linalotengenezwa wakati wa uimbaji. Hivyo, waimbaji huimba na kucheza huku wakiwa wanauzunguka mkuki. Kitendo cha kuuchomeka mkuki ardhini ni ishara ya ulinzi wa mizimu katika utendaji wa tendo hilo.

KiSimiotiki kishoka na kirungu huwa ni ishara ya mapambano na ushindi katika nyimbo za tiba. Mganga au wasaidizi wake hushika vifaa hivyo wakati wa uimbaji na huonesha ishara ya kukata hewani au kupiga hewani kwa kutumia kirungu na kishoka. Kirungu kinachotumika huwa na umbo dogo tofauti na mashoka makubwa au virungu vikubwa. Matumizi yake huwa ya kiishara zaidi. Lakini, ishara hizi hukamilisha tendo thabiti la kuyashinda majini mabaya ambayo yanakuwa yakiwatesa wagonjwa.

Katika utafiti wetu, ishara hizi tumezimithilisha na matumizi ya taswira na ishara katika maombi ya wagonjwa kwa dini za Kikristo ambapo muombaji huita moto (ndimi za moto) au huita Roho Mtakatifu. Moto huo huwa hauonekani, lakini mgonjwa au mtu mwenye mapepo (majini) huhangaika na kupiga kelele kuwa anaungua kwa moto huo. Hivyo, matumizi ya vifaa kama ishara ya mapambano na majini katika tiba asili hufanana na ishara hiyo katika imani ya Kikristo.

Shanga hutumika kama kifaa ambacho huvaliwa wakati wa kuimba nyimbo za tiba asili na wakati wa kuimba nyimbo za tiba asili. Wakati mwingine, huvaliwa kama tiba kwa wagonjwa. Matumizi ya shanga hutofautiana kutokana kwa mganga mmoja na mganga mwingine. Kuna baadhi ya waganga hutunga shanga zikiwa mpya na kuwapa wagonjwa wavae au wao wenyewe wazivaa wakati wa tiba na uimbaji. Lakini, kuna waganga ambao wenyewe huvaa shanga kuanzia shingoni hadi kifuni. Shanga ambazo huvaliwa wakati wa tendo la uimbaji na utoaji tiba si shanga mpya, bali ni shanga ambazo tayari zimevaliwa na mtu. Mtu huyo ni mke halali wa mganga endapo mganga ni mwanamume. Mmojawapo wa waganga tuliyehojiana nae anasema:

“Sababu za kutumia shanga ambazo zimetumika na mkewe kwa kuzivaa kiunoni kisha mganga azitumie katika tiba na kama maleba katika uimbaji ni kwamba kuna nguvu ya asili ambayo ipo katika shanga zinazovaliwa na mwanamke. Nguvu hiyo imetoka katika mizimu ya mwanamke” (Mtafitiwa 14: Mahojiano yalifanyika, 13. 08. 2017).

Manyanga ni kifaa kingine kinachotumika katika tendo la uimbaji. Waganga waliohojiwa wamesema:

“Manyanga ni kifaa muhimu katika uimbaji wa nyimbo za tiba kwa kuwa mlio wake huivuta na kuifurahisha mizimu kwa haraka zaidi” (Mtafitiwa 14: Mahojiano yalifanyika, 13. 08. 2017).

Upigajii wa manyanga hauhitaji ufundi sana bali mpiga manyanga humlazimu kufuata mapigo/mahadhi ya wimbo. Katika utafiti huu, umebaini kwamba, katika nyimbo za tiba asili hakuna wimbo utakaokosa manyanga. Nyimbo zote ni lazima manyanga yapigwe. Kuna nyimbo zinazotendeka bila ngoma, lakini hakuna wimbo unaoimbwa bila manyanga. Kwa ujumla mlio wa manyanga hunogesha zaidi wimbo

kuliko vifaa au ala nyingine. Mpiga manyanga huwa mtu wa jinsi yoyote tofauti na wapiga ngoma, ambazo aghalabu ni wanaume.

Mkia wa nyumbu ni moja ya vifaa vitumikavyo katika tendo la uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Mkia huu una manyoya ambayo hutawanyikatawanyika pindi uinuliwapo. Katika kushuhudia uimbaji wa nyimbo za tiba asili tumebaini kwamba matumizi ya mkia huu ni ya kiishara zaidi wakati wa kuimba na kucheza nyimbo za tiba asili. Mganga mmojawapo alisema ishara hizo tunazoziona ni kitu halisi ambapo majini mabaya ambayo yapo kwa wagonjwa au hata ambayo yamenuia kufika katika uwanja wa mganga na kufanya matendo maovu. Mganga hufanya ishara hiyo ya kufukuza pepo hao wabaya kwa pande zote, mbele, nyuma, kushoto na kulia. Kitendo hii hakifanyiki kwa nyimbo zote, bali hufanyika kwa nyimbo ambazo hutumika kukaribisha tendo la tiba kuanza.

Fimbo nyeusi ya mpingo ni kifaa kingine kiendacho pamoja na tendo la uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Fimbo hii hushikwa na mganga, kiSimiotiki fimbo hii ni ishara ya nguvu na utawala wa mganga. Mganga hushika fimbo hii kuonesha nguvu na uwezo wa mizimu yake. Mganga mmojawapo alieleza kuwa fimbo hii hutumika kama kifaa cha tiba kwani wakati tendo la uimbaji wa nyimbo za tiba likiendelea. Ikitokea mgonjwa anapandisha pepo mbaya mwenye kusababisha maradhi, humuonesha fimbo hiyo; na mapepo yakaanza kutoa sauti ya woga na kuanza kutoka mwilini na kumfanya mgonjwa apone maradhi yaliyokuwa yakimsumbua.

Hivyo, mavazi na vifaa vitumikavyo katika nyimbo za tiba asili hutumika kama ishara maalumu ambazo hutumika katika kutibu wakati tendo uimbaji likiwa

linaendelea. Hivyo, vitendo na ishara mbalimbali ambazo hufanyika kwa kutumia maleva na vifaa ni muhimu katika tendo la uimbaji wa nyimbo za tiba asili.

5.3.9 Muktradha

Kutokana na upanuzi wa dhana ya mtindo katika utendekaji wa nyimbo kama utanzu wa fasihi simulizi muktadha wa mahali ni kipengele mojawapo cha mtindo wa nyimbo za tiba asili. Matendo yanayotendeka katika fasihi simulizi ni ya dhati. Hivyo, ni lazima kuwe na muktadha wa mahali pa kutendea jambo. Katika utafiti huu, tunachukulia kwamba, mahali ni kipengele cha mtindo wa nyimbo za tiba asili. Mtazamo huu unatokana na msingi wa nadharia ya mitindo ambayo imepanua wigo wa vipengele vya mtindo katika uimbaji hivyo kufumbata viziadalugha. Sehemu inayofuata inafafanua jukwaa kama muktadha wa mahali ambao kwa mujibu wa utafiti huu ni kipengele cha mtindo.

Jukwaa ni mahali ambapo kazi ya fasihi simulizi hutendeka. Utendekaji huo hufanyika katika mahali rasmi. Wakati wa uimbaji na utendaji huo, kunakuwa na uigizaji wa matendo mbalimbali yanayofanywa na mganga, wagonjwa au wasaidizi wa mganga. Katika utafiti huu jukwaa ni mahali popote ambapo nyimbo za tiba asili zinaimbwa. Inawezakuwa porini, kwenye eneo la kutibia wagonjwa au makazi ya wagonjwa.

Uhusiano wa mitindo ya utendaji na uimbaji wa nyimbo za tiba asili huukiliwa na jukwaa. Muundo wa jukwaa unaweza kubadilika kutegemeana na mahali pa uimbaji wa nyimbo za tiba asili. Katika utafiti huu, mtafiti alishuhudia jukwaa la nyumbani likiwa na nafasi ndogo na kuruhusu wazumi wachache ikilinganishwa na jukwaa la

porini wakati kutambika likiwa na nafasi kubwa hivyo kuruhusu wazumi wengi zaidi. Tofauti hizi zinaibua mitindo anuwai ya majukwaa ya uimbaji wa tiba asili. Muundo wa jukwaa kama kipengele cha mtindo ni muhimu katika kudokeza dhamira ya uimbaji uliokusudiwa.

Katika Wilaya ya Songea Mjini na Vijijini, mtafiti aliwashuhudia baadhi ya waganga wakitumia msitu wa Matogoro na Chabruma kuchimba dawa, kutibu na kufanya matambiko. Misitu hiyo inaunda aina mahsusi ya majukwaa ya nyimbo za tiba asili ambayo kimsingi ni rahisi kudokeza dhamira ya shughuli hizo kupitia mandhari kama kipengele cha mtindo. Hata hivyo, uchambuzi wa data haujabaini uwezekano wa kutofautisha nyimbo za tiba asili kwa kigezo cha muktadha wa kiwakati. Kwa maneno mengine hakuna nyimbo maalumu za zinazoimbwa au usiku pekee. Wimbo mmoja unaweza kuimbwa wakati wowote wa shughuli za matibabu.

5.4 Hitimisho

Sehemu ya tano katiika tasinifu hii imeshughulikia na uchambuzi wa data umebainisha mitindo mbalimbali iliyotumika katika nyimbo za tiba asili, ikiwa ni pamoja na mitindo mikuu ya matumizi ya lugha, mtindo wa nyimbo unaotokana na kigezo cha urefu, mtindo wa mishororo, mtindo wa fomula, dailojia, viunganishi, vina na mizani, utendaji wa kimuziki, mtindo wa maleba na vifaa vinginevyo. Vipengeele hivyo hutumiwa kwa madhumuni mahsusi kwa kuzingatia muktadha wa uimbaji unaorejelea shughuli za uganga na tiba katika nyimbo za tiba asili katika jamii za mkoa wa Ruvuma hapa nchini.

SURA YA SITA

TATHIMINI YA MATOKEO YA MTINDO WA NYIMBO ZA TIBA ASILI

KWA WAGONJWA

6.1 Utangulizi

Sehemu hii inahusu mtindo wa nyimbo za tiba asili kwa wagonjwa. Sehemu hii inatokana na uwasilishaji na uchambuzi wa data zinazohusiana na lengo la tatu la utafiti huu. Lengo hilo lilihusu kubainisha matokeo ya mtindo wa nyimbo za tiba asili kwa wagonjwa. Sehemu hii inaweka bayana kwamba, mtindo unaotumika katika nyimbo za tiba asili zinakulia matokeo ya aina moja au nyingine kwa wagonjwa. Matokeo ya vipengele vya mtindo kama vilivyobainishwa katika sehemu hii vimewasilishwa katika vipengele mbalimbali ili kuonesha matokeo ya kila mtindo uliotumika katika nyimbo zinazowahusu wagonjwa wanaotibiwa kwa tiba asili.

6.2 Mtindo wa Nyimbo za Tiba Asili

Katika uchunguzi wa kipengele cha mtindo wa nyimbo za tiba asili, utafiti huu ulichambua na kushughulikia maeneo yafuatayo ili kubaini mtindo uliotumika katika nyimbo za tiba asili za jamii za mkoani Ruvuma.

6.2.1 Matumizi ya Lugha ya Kawaida

Matumizi ya lugha ya kawaida yanatokana na fanani ambaye hutunga wimbo unaohusika kwa kuiangalia hadhira yake pamoja na kusudio lake. Hivyo, hutunga nyimbo za papo kwa papo kulingana na mahitaji ya hadhira yake. Matokeo yake, nyimbo za aina hiyo zinamwezesha mgonjwa kujifunza kwa haraka na kushiriki mchakato wa tiba kikamilifu. Wimbo unaoeleweka kwa urahisi unasaidia kuelewa

maelekezo ya matumizi ya dawa na hutolewa kwa njia ya nyimbo. mfano, kwa le kurejea wimbo wa ‘*Mababu na Malaika Mtusaidie*’ kama ulivyonukuliwa katika sura ya nne umetumia lugha ya kawaida kama ulivyobainishwa katika sehemu hii:

Mganga: Mababu na Malaika kwa uwezo wenu baba mtusaidie,
Wasaidizi: Mababu na malaika kwa uwezo wenu baba mtusaidie,

Mganga: Maombi kwa malaika x3,
Maombi yetu wote x2.
Wasaidizi: Maombi kwa malaika x3,
Maombi yetu wote x 2.

Mganga: Maombi eee maombi eee x2,
Wasaidizi: Maombi eee maombi eee x2.

Mganga: Maombi yetu wote,
Maombi eee x2.
Wasaidizi: Maombi yetu wote,
Maombi eee x 2.

Chanzo: Uwandani (2017)

Wimbo wa hapo juu unaonesha matumizi ya lugha ya kawaida ambayo matokeo yake kwa mgonjwa ni kuelewa maelekezo na kushiriki kikamilifu katika mchakato wa matibabu.

6.2.2 Matumizi ya Lugha ya Kisanaa

Data za utafiti huu zinaonesha aina mbalimbali za matumizi ya lugha ya kisanaa. Kila aina ya lugha ya kisanaa huukilia matokeo ya aina moja au nyingine kwa mgonjwa. Katika kudhihiridha matokeo ya lugha ya kisanaa kwa wagonjwa vipengele anuwai kama vile uchanganyaji msimbo, lugha ya picha na uradidi vimefafafnuliwa.

6.2.2.1 Uchanganyaji Msimbo

Katika utafiti huu, kuna nyimbo mbalimbali ambazo waimbaji wamechangaya lugha. Katika wimbo uitwao ‘*Ningalonga Ndauli*’ kuna matumizi dhahiri ya uchanganyaji msimbo kama ulivyokaririwa hapa:

Mganga:	<i>Ningalonga ndauli x2,</i>
Wazumi:	<i>Ningalonga ndauli x 2.</i>
Mganga:	<i>Ningalonga ndauli x 2,</i>
Wazumi:	<i>Ningalonga ndauli x 2.</i>
Mganga:	<i>Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lisoka,</i>
Wazumi:	<i>Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lisoka.</i>
Mganga:	Babu unange, babu unange,
Washiriki:	Babu unange, babu unange.
Mganga + Wazumi:	<i>Pa nyumba pana lisoka,</i>
Mganga:	<i>Pana lisoka, pana lisoka.</i>
Wazumi:	<i>Pana lisoka, pana lisoka,</i>
Mganga + Wazumi:	<i>Pana nyumba pana lisoka.</i>
Mganga:	Babu unange, babu unange, pa nyumba pana lisoka,
Wazumi:	Babu unange, babu unange, pa nyumba pana lisoka.

Tafsiri ya Kiswahili

Nitasema nini?

Mganga:	Nitaseme nini x2,
Wazumi:	Nitaseme nini x2.
Mganga:	Nitaseme nini x2,
Wazumi:	Nitaseme nini x2.
Mganga:	Nitaseme nini, ndani kuna nyoka,
Wazumi:	Nitaseme nini, ndani kuna nyoka.
Mganga:	Babu nisaidie, babu nisaidie,
Washiriki:	Babu nisaidie, babu nisaidie.

Mganga + Wazumi:	kwenye nyumba kuna nyoka,
Mganga:	kuna nyoka, kuna nyoka.
Wazumi:	kuna nyoka, kuna nyoka,
Mganga + Wazumi:	kwenye nyumba kuna nyoka.
Mganga:	Babu nisaidie, babu nisaidie, kwenye nyumba kuna nyoka,
Wazumi:	Babu nisaidie, babu nisaidie, kwenye nyumba kuna nyoka.

Chanzo: Uwandani (2017).

Wimbo huu ni wa jamii ya Wabena na mzimu uliompanda ni wa Wabena kwa sababu mganga huyu alienda kuongeza nguvu zake kwa Wabena. Katika sura ya nne tulifafanua sababu anuwai za uchanganyaji msimbo. Pia, tulibainisha kwamba, uchanganyaji msimbo unaojitokeza katika nyimbo za tiba asilia ni wa kiwango cha neno. Waganga wa tiba asili wanapochanganya msimbo unaongeza imani kwa wagonjwa kwamba, mganga wao anaongea na mizimu kwa lugha wasioijua. Hivyo, watapata msaada zaidi. Mgonjwa mmojawapo alipohojiwa kuhusu matumizi ya lugha zaidi ya moja kwenye nyimbo za tiba asili alikuwa na haya ya kueleza:

“... unajua waganga wanapoimba au kuongea kwa lugha isiyoeleweka vizuri kwetu haongei wao, bali ni mizimu ambayo inasaidia sisi tupone. Lugha ya mizimu si rahisi kuelewa, lakini mizimu wanajua lugha zetu....”
(Mtafitiwa 1: Mahojiano yalifanyika, 03. 09. 2017).

Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba, mtindo wa uchanganyaji msimbo matokeo yake kwa wagonjwa ni kuwa na matumini zaidi ya kupona.

6.2.2.2 Lugha ya Picha

Wimbo unaoitwa *‘Ningalonga Ndauli’* umetumia lugha ya picha kuwa ndani ya nyumba kuna nyoka. Matumizi ya lugha ya picha katika nyimbo yanasaidia

kupunguza hofu kwa wagonjwa. Jambo ambalo linaweza kuwa gumu au zito kulieleza kwa lugha ya kawaida linaweza kuelezwa kwa lugha ya picha.

Mganga: *Ningalonga ndauli x2,*
Wazumi: *Ningalonga ndauli x2.*

Mganga: *Ningalonga ndauli x2,*
Wazumi: *Ningalonga ndauli x2.*

Mganga: *Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lizoka,*
Wazumi: *Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lizoka.*

Mganga: Babu *uunange*, babu *uunange*,
Washiriki: Babu *uunange*, babu *uunange*.
Mganga + Wazumi: *Pa nyumba pana lisoka.*

Mganga: *Pana lisoka, pana lisoka,*
Wazumi: *Pana lisoka, pana lisoka.*
Mganga + Wazumi: *Pa nyumba, pana lisoka,*

Mganga: Babu *uunange*, babu *uunange, pa nyumba pana lisoka,*
Wazumi: Babu *uunange*, babu *uunange, pa nyumba pana lisoka.*
Chanzo: Uwandani (2017).

Katika wimbo huo neno ‘nyoka’ linamaanisha hatari iliyomwingia mmoja wa wagonjwa. Mara nyingi ni jini mbaya aliyemuingia mgonjwa, amefananishwa na nyoka. Katika wimbo huo, anaombwa babu (mzimu wa tiba) aweze kutoa tiba kwa mgonjwa aliyepatwa na tatizo hilo. Kwa hiyo, matokeo ya matumizi ya lugha ya picha ni kuwafanya wagonjwa waendeleo kuwa watulivu hata pale wanapoelezwa masuala mazito kuhusu afya zao.

6.2.2.3 Uradidi

Katika ushairi-simulizi uradidi ni kitu cha kawaida kujitokeza. Katika utafiti huu, tumebaini kwamba, kiwango cha uradidi katika nyimbo za tiba asili kimekuwa kikibadilika kutegemea idadi ya beti za wimbo. Beti zikiwa chache, uradidi

hujitokeza zaidi kuliko beti zikiwa nyingi. Kuna nyimbo zenye kiwango kikubwa cha uradidi kama inavyoonekana kwenye wimbo uitwao ‘*Mjukuu Analia*’:

Mganga: Mjukuu aee,
Mjukuu analia aee.

Wazumi: Mjukuu aee,
Mjukuu analia aee.

Mganga: Mjukuu aeee,
Baba mjukuu analia aee.

Wazumi: Mjukuu aeee,
Baba mjukuu analia aee.

Mganga: Tukachimbie dawa,
Mjukuu aee,
Mjukuu analia aee.

Wazumi: Mjukuu aee,
Mjukuu analia aee.

Chanzo: Uwandani (2017).

Matokeo ya uradidi kwa wagonjwa ni kulifanya jambo linalowasilishwa lieleweke vizuri. Mtafiti alishuhudia akiwa uwandani kwamba, uradidi husaidia kumkaribisha jini au kumfanya mgonjwa aliyepandwa na pepo ili aweze kutoa maelezo kwa mganga. Kwa kufanya hivyo, matokeo ni kwamba, shida ya mgonjwa inakuwa imeeleweka vizuri na kuweza kusaidiwa. Hii inaonesha dhahiri kwamba, uradidi una matokeo mazuri kwa mgonjwa.

6.2.3 Urefu

Nyimbo zinazotumika katika tiba asili zinatofautina kwa urefu. Katika utafiti huu vigezo vilivyotumika kutofautisha urefu wa nyimbo ni idadi ya maneno, wakaa, beti, na mishororo ambayo kila moja ina matokeo mbalimbali kwa wagonjwa.

Ilishuhudiwa uwandani kwamba, wimbo mrefu kwa kigezo cha wakaa au idadi ya maneno na beti una matokeo mazuri zaidi katika tiba kuliko wimbo mfupi. Mahojiano tuliyofanya na mganga mmojawapo kuhusu hali hiyo, alikuwa na haya ya kusema:

“Kuna wakati nyimbo zinaimbwa kwa muda mrefu kwa sababu baadhi ya majini huwa hayajitokezi kwa urahisi. Kwa hiyo, inabidi muimbe tena na tena kama kumbembeleza hivi, maana tunataka afike, aeleze chanzo chake wapi na kwa nini anamsumbua mgonjwa! Baada ya hapo, utakuta mgonjwa anapata auheni kuliko pakiwa na ukimya au uimbaji kiasi tu. Nyimbo zina nguvu sana kwetu, eee bwana!” (Mtafitiwa 2: Mahojiano yalifanyika, 10. 09. 2017).

Dondoo ya hapo juu inaonesha nguvu na faida ya nyimbo kwa mgonjwa. Katika utafiti huu, hayo ndiyo yanayoelezwa kuwa ni matokeo ya nyimbo kwa mgonjwa. Katika kuzungumzia nguvu za nyimbo, Senkoro (1988) amesisitiza kwamba, nyimbo zina nguvu za ‘uchawi’ kutokana na ufanisi wake katika masuala ya kuondoa uchovu wa kimwili. Kwa hiyo, katika muktadha wa utafiti huu, nyimbo husaidia matibabu.

6.2.4 Daiolojia

Uwasilishaji wa nyimbo za tiba asili huwashirikisha fanani (mganga au kiongozi) na hadhira (wazumi) katika kuimba, kucheza na kupiga ala mbalimbali za muziki. Ushirikishwaji huo ni sawa na kusema mtindo wa mwitiko kwa sababu ndani ya mtindo huo kuna majibizano na kuimba kwa kupokezana baina ya mganga au kiongozi na wazumi kama inavyoonekana katika wimbo unaojulikana kw ajina la ‘*Tunakuomba Baba*’:

Mganga: Tunakuomba baba,
Majini yote mwana,
Tufungulie mwanga,
Tuonee huruma.

Wazumi: Tunakuomba baba,
Majini yote mwana,,
Tufungulie mwanga
Tuonee huruma

Mganga: Tunaomba majini yote,
Mtufungulie mwanga,
Mtuonee huruma.

Wazumi: Tunaomba majini yote,
Mtufungulie mwanga,
Mtuonee huruma.

Chanzo: Uwandani (2017).

Matokeo ya mtindo huo, ni kwamba, wagonjwa ambao ni sehemu ya wazumi wananufaika na uimbaji kwa kupata faraja na kusahau maumivu yao kwa muda wakati mchakato wa matibabu ukiwa unaendelea. Wagonjwa wanakuwa washiriki hai katika matibabu, jambo linaloongeza nafasi ya matumini ya kutatuliwa kwa shida zao. Katika nadharia ya Mitindo, daiolojia tumeiweka katika mhimili wa utengamano wa fanani na hadhira. Kupokezana katika uimbaji wa nyimbo za tiba asili hufanyika ili kukamilisha tendo la tiba.

6.2.5 Vina na Mizani

Katika ushairi wa kimapokeo vina na mizani hukuchuliwa kama uti mgongo au rohao ya ushairi (Abed, 1952). Dhana hiyo ni tofauti na nyimbo za tiba asili ambapo kanuni zake za utunzi hazifanani na mashairi ya kimapokeo. Mashairi ya kimapokeo ni sehemu ya ushairi wa Kiswahili (fasihi andishi na fasihi simulizi). Katika nyimbo, kuna ubadilikaji au ugeukaji wa tungo. Utungo unaowasilishwa jukwaani au

mbele ya hadhira unaweza kubadilika kutegemea mwasilishaji, hadhira pamoja na wakati. Vilevile, uwasilishwaji unaweza kuachwa au kubadilishwa. Hali hii hufanya mpangilio wa vina na mizani kutokuwa imara. Katika utafiti wetu, tumegundua kwamba, uradidi hufanya uwepo wa vina katika nyimbo. Vina hivi mara nyingi huwa vina vya mwisho. Kwa kuwa mishororo mingi ya nyimbo huwa ni kipande kimoja, hata zile nyimbo zenye vipande viwili haziwi na vina vya kati. Mfano mmojawapo wimbo wa ‘*Nipe Udi*’:

Mganga:	Nipe udi na ubani mwalimu, Nipe udi na ubani.
Wazumi:	Nipe udi na ubani mwalimu, Nipe udi na ubani.
Mganga:	Wee! Nipe udi na ubani mwalimu, Nipe udi na ubani tuombe.
Wazumi:	Nipe udi na ubani mwalimu, Nipe udi na ubani tuombe. Chanzo: Uwandani (2017).

Katika wimbo huu, uradidi katika uimbaji ndio ulifanya kuwapo kwa vina. Vina vinajitokeza kila baada ya kupokezana katika uimbaji, kwa kuwa wazumi huitikia maneno yale yale yaliyoimbishwa na fanani (mganga). Vina vilivyojipambanua ni -**mu** kila baada ya mstari mmoja na **-ni**; kisha, **-mbe**. Baadhi ya nyimbo zilizochunguzwa uwandani zilibainika kuwa na mchanganyiko wa vina. Faida ya mtindo huu ni kuongeza ladha na mahadhi ya wimbo kwa wagonjwa na kuwafanya waufurahie wimbo. Pia, huongeza juhudi ya kuimba ambayo ni muhimu katika matibabu. Aidha, kama ilivyo katika ushairi wa kimapokeo, vina husaidia kuonesha msisitizo wa jambo.

6.2.6 Uchezaji

Miondoko ya uchezaji hujumuisha tabia za kuigiza mwendo au mijongeo ya mwili. Mitindo hii hujidhihirisha kwa fanani pamoja na hadhira kwa kutumia uso, kichwa, mikono au kiungo kingine chochote cha mwili. Katika utafiti huu, mtafiti alishuhudia mitindo mbalimbali ya uchezaji wa nyimbo za tiba asili kama vile kujiviringisha, kuzungusha shingo, kutoa mkono wa shukrani, kuruka kwa kutumia makalio, kudondoka na kupoteza fahamu na kuweka mikono kichwani. Mitindo ya uchezaji hutofautiana kati ya aina moja ya wimbo na nyingine katika jamii za Kiafrika. Matokeo ya miondoko hiyo yote kwa mgonjwa ni kuwafanya wale wenye majini yasiyopenda uchezaji au kwa sababu ya kucheza kwa kushurutishwa kama ilivyo kwa miondoko ya kurukaruka kwa kutumia makalio waamue kuondoka katika mwili wa mgonjwa. Katika mahojiano na mganga mmojawapo alikuwa na haya ya kueleza:

“...ndugu yangu kuimba na kucheza ni muhimu katika matibabu. Majini wapo wanapenda kucheza na weingine hawapendi. Wale ambao hawapendi kucheza sana wanakasirika na kuamua kuondoka. Wakiondoka ni nafuu kwa mgonjwa na mganga kazi ya kumfukuza inakuwa imepungua. Kwa wanaopenda kucheza, wanaweza kumchezeshwa mgonjwa mpaka utumie nguvu za kuwatuliza, ee bwana, maana anaweza kuumia” (Mtafitiwa 3: Mahojiano yalifanyika, 14. 09. 2017).

Kwa hiyo, kwa dondoo ya hapo juu ni wazi kwamba, kuna nguvu kubwa inayotokana na matumizi ya nyimbo katika matibabu ya asili.

6.2.7 Utendaji wa Kimuziki

Mitindo ya utendaji wa kimuziki ina nafasi kubwa katika uwasilishaji wa ujumbe na maana katika nyimbo za fasihi simulizi ya Kiafrika. Niane (1995) anaeleza kwamba, muziki ndio uti wa mgongo wa waimbaji katika fasihi simulizi. Umuhimu wa muziki

katika nyimbo za tiba asili upo katika kuchochea hamasa za ushiriki wa wagonjwa na kukoleza ujumbe unaowasilishwa. Hivyo, mfungamano wa muziki na nyimbo za tiba asili unapatikana katika utendaji wake. Muziki huufanya ujumbe ueleweke vyema kwa wagonjwa na kuufanya utaratibu wa matibabu uvutie. Akiwa uwandani, mtafiti alishuhudia matumizi makubwa ya muziki miongoni mwa waganga mbalimbali walioshiriki katika utafiti huu. Kwa hiyo, ni wazi kwamba, muziki unaweza kuwa wa ala au wa sauti za uimbaji, lakini matokeo yake kwa wagonjwa yanafanana.

6.2.8 Maleba na Vifaa

Kuna maleba na vifaa anuwai vinavyotumika katika nyimbo za tiba asili za mkoa wa Ruvuma. Maleba ni aina ya mavazi maalumu yanayovaliwa na fanani na hadhira katika utendaji wa fani inayohusika (Mgogo, 2017). Wagonjwa wanapofika kwa mganga hupewa mavazi maalumu. Mavazi hayo hutokana na masharti ya mizimu; na ni shemu ya matibabu. Mtafiti alishuhudia kuwapo kwa mavazi ya aina tofauti tofauti yanayovaliwa na wagonjwa kulingana na shida au magonjwaa yao. Mavazi hayo hutofautiana kwa rangi na miuundo. Matokeo ya mavazi hayo ni kufanisha kwa tiba ya mgonjwa anayehusika. Vilevile, kuna matumizi ya vifaa kama ngoma, pembe, kilungu, mkuki au mkia wa nyumbu. Hivyo vyote ni vifaa vya tiba kwa mgonjwa. Mkia wa nyumbu hutumika kutabiri ikiwa maombi ya mgonjwa yamepokelewa na mizimu ama la.

6.3 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia uwasilishaji na uchambuzi wa data kwa kuzingatia lengo mahsus la tatu. Sehemu sita inahusu matokeo ya mtindo ya nyimbo za tiba asili kwa

wagonjwa. Uchambuzi wa data unaonesha kwamba, kila mtindo unaleteleza matokeo ya aina moja ama nyingine kwa mgonjwa. Baadhi ya matokeo hayo ni kuwatia moyo wagonjwa, kuwashirikisha katika mchakato wa tiba, kuburudika, kuwaongezea imani ya tiba na kufukuza majini wabaya. Sura ya saba ya mwisho inahusu muhtasari, matokeo na mapendekezo ya utafiti.

SURA YA SABA

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

7.1 Utangulizi

Sura hii ya saba ya mwisho inahusu muhtasari wa tasunifu nzima. Matokeo ya utafiti mzima yameelezwa katika sura hii kwa muhtasari. Baadhi ya vipengele vilivyomo katika sura hii ni pamoja na muhtasari wa tasunifu, utoshelevu wa nadharia zilizotumika katika uchambuzi, uhakiki na mjadala wa data zilizowasilishwa, matokeo ya utafiti na mchango wa utafiti. Pia, kuna mapendekezo na hitimisho la utafiti.

7.2 Muhtasari wa Tasunifu

Utafiti huu umejengwa na sura sita. Sura ya kwanza imeweka msingi wa tasunifu kwa kueleza vipengele vya utangulizi, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo mahsusi na maswali ya utafiti. Pia, kuna umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake, pamoja na mpangilio wa tasunifu nzima. Sura ya pili inahusu mapitio ya machapisho na nadharia zilizotumika katika uchambuzi, uhakiki na mjadala wa data zilizowasilishwa katika utafiti uliofanyika. Sura hii imetumika kujenga hoja ya kufanyika kwa tasunifu.

Sura ya tatu imeeleza mbinu za utafiti zilizotumiwa katika ukusanyaji, uchambuzi na uhakiki wa mjadala wa data. Sura ya nne na ya tano zilihusu uwasilishaji na mjadala wa data uliongozwa na nadharia za Mitindo na Simiotiki. Katika sura hizi, nyimbo za utanzu teule zimeainishwa. Uainishaji ulitumia kigezo cha dhima za nyimbo mbalimbali. Pia, vipengele mbalimbali vya mtindo vilibainishwa katika nyimbo

zilizochunguzwa. Vipengele vya mtindo vimesaidia kuwasilisha ujumbe katika nyimbo teule. Sura ya sita inahusu muhtasari wa tasnifu, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, mapendekezo na hitimisho la utafiti.

7.3 Utoshelevu wa Nadharia Zilizotumika

Nadharia za Mitindo na Simiotiki ndizo zilizotumika katika uchambuzi, uhakiki na mjadala wa data zilizowasilishwa. Nadharia ya Mitindo ilimsaidia na kumuongoza mtafiti kuwaweka watumiaji wa nyimbo za tiba za asili katika ulimwengu wao wa kawaida uliowazi na halisi katika uhakiki na uwasilishaji wa data zilizoshughulikiwa katika tasnifu hii. Watumiaji wa nyimbo za tiba za asili walichunguzwa kwa kina namna walivyoyashughulikia masuala ya uganga na tiba na kuyatumia kama yalivyo na kukubalika kupitia nyimbo zao. Nyimbo za tiba asili zilichambuliwa na kuhakikiwa kwa uwazi ili kufanya utafiti wa kina kwa kuzingatia historia yao, falsafa yao na utamaduni wao kuhusiana na masuala ya uganga na tiba zaa asili katika jamii zao. Nadharia ya Simiotiki ilimruhusu mtafiti kuchunguza kipengele cha mtindo katika data zilizowasilishwa. Matumizi ya nadharia hizi yalitokana na misingi ya kutegemeana na kukamilishana ili kukidhi malengo ya utafiti uliofanyika.

7.4 Matokeo ya Utafiti

Tasnifu hii ililenga kuchunguza mtindo katika nyimbo za tiba asili za jamii za mkoani Ruvuma. Utafiti wa data zilizowasilishwa uliongozwa na malengo mahsusi matatu. Uchambuzi, uhakiki na mjadala wa data zilizolengwa katika tasnifu hii uliongozwa na nadharia za Mitindo na Simiotiki. Matokeo ya mjadala wa data za utafiti yameelezwa katika sehemu inayofuata. mahsusimahsusi

7.4.1 Lengo la Kwanza

Lengo mahsusi la kwanza lilihusu kuainisha nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma. Matokeo yanaonesha kwamba, kuna aina saba za nyimbo za tiba asili. Uainishaji huu umetumia kigezo cha dhima za nyimbo mbalimbali. Aina ya kwanza ni nyimbo za maombi zinazotumika katika hatua mbalimbali za maombi pamoja na kuita mizimu. Tumeona jinsi zinavyojibainisha kabla ya maombi, wakati wa kuchimba dawa na wakati wa kutumia dawa. Pili, ni nyimbo za faraja zinazotumika kuwafariji wagonjwa wenye maumivu makali. Tatu, ni nyimbo za kufurahisha mizimu. Hizi huimbwa baada ya tendo la tiba kukamilika. Nne, ni nyimbo za historia zinainbwa kwa ajili ya kujikumbusha historia ya aina mbalimbali za dawa ambazo zisingejulikana kama zisingekuwa zimetungiwa wimbo. Tano, ni nyimbo za shukrani. Hizi hutumika kushukuru mizimu baada ya kukamilika kwa tendo la tiba. Sita, ni nyimbo za kutolea tiba. Hizi huimbwa wakati tiba ikitolewa. Saba, ni nyimbo za kuaga zinazoimbwa wakati wa kuwaaga mizimu baada ya tendo zima la tiba kukamilika.

7.4.2 Lengo la Pili

Lengo mahsusi la pili lilihusu kubainisha mtindo unaotumika katika nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma. Katika sehemu hii, dhana ya mtindo ilipanuliwa kwa kuhusisha vipengele vya lugha na viziadalugha kuwa ni sehemu ya mtindo katika nyimbo za tiba asili. Kwa kufanya hivyo, vipengele mbalimbali vya mtindo vilibainishwa. Baadhi ya vipengele vilivyobainishwa ni mtindo wa lugha, mtindo kwa kigezo cha urefu wa nyimbo, mtindo wa mishororo, mtindo wa matumizi ya fomula, mtindo wa matumizi ya dailojia, mtindo wa uzingatizi wa vina

na mizani, uchezaji, utendaji na matumizi ya maleba na vifaa. Upanuzi huu wa matumizi ya nadharia kwa kutumia mhimili wa viaziada-lugha ni mpya katika nadharia ya Mitindo. Vilevile, nadharia ya Simiotiki ilitumika katika kuchambua na kueleza maana ya ishara zilizojitokeza katika nyimbo zilizochunguzwa katika utafiti uliofanyika.

7.4.3 Lengo la Tatu

Lengo mahsusi la tatu lilihusu matokeo ya mtindo wa nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma. Katika kukamilisha lengo hilo, vipengele mbalimbali vya mitindo vilivyobainishwa katika lengo hilo. Imeelezwa kwamba, matokeo yaliyojitokeza zaidi pamoja na kuwatia moyo wagonjwa, kuwashirikisha katika mchakato wa uganga na tiba, kuwaburudisha, kuwaongezea imani ya tiba na kufukuza majini wabaya. Nadharia ya Mitindo ilitumia mhimili wa uchambuzi lugha ambapo vipengele vyote vya lugha vilibainishwa na kuonesha matokeo yake kwa wagonjwa. Mhimili wa wa uchambuzi wa viziada-lugha ulitumika katika kuonesha matokeo ya mtindo wa viziada-lugha katika nyimbo za tiba asili kwa wagonjwa. Aidha, nadharia ya Simiotiki ilitumika kuchambua na kueleza maana ya ishara mbalimbali zilizotumika katika utanzu uliochunguzwa. Katika sura hii, imebanika kwamba, mtindo wa nyimbo za tiba asili husaidia kufariji na kuponya wagonjwa na waganga kuoneshwa dawa.

7.5 Mchango wa Utafiti

Tasinifu hii imegundua kuwa nyimbo za tiba asili zinazoimbwa na waganga katika jamii za mkoani Ruvuma hutazamwa chombo mahsusi cha kijadi kinachorejelea

kaida za kiasili zilizonuia kukuza, kuimarisha, kuendelea na kuzienzi matumizi ya uganga na tiba za asili katika jamii nyingi hapa nchini, hasa katika kipindi hiki cha maendeleo ya sayansi na teknolojia, ambapo sanaa jadiya za Kiafrika zimeendelea kupunzwa na kufifia kwa kasi kimatumizi. Pia, utanzu huu unatazamwa kama kiungo maalumu cha mahusiano kati ya waganga, jamii na mizimu; na hutumika kama ensaiklopedia yenye urejelezi wa masuala yanayojenga mfumo wa kuifunza, kuiimarisha na kuiweka jamii pamoja katika misingi ya utamaduni na falsafa nzima ya maisha ya jadi yao tangu kale mpaka sasa kuhusu dhima na matumizi ya nyimbo za tiba asili.

7.6 Mapendekezo ya Utafiti

Katika sehemu hii tumetoa mapendekezo mbalimbali. Kwanza, serikali haina budi kuweka mikakati thabiti inayolenga kukuza, kuendeleza na kuhifadhi utamaduni wa taifa na kuwajali waganga wa tiba asili. Waganga wa tiba asili wanafanya shughuli zao katika mazingira magumu, licha ya kuwa wana mchango mkuwa katika jamii wa kutoa tiba na kuhifadhi utamaduni pamoja fasihi simulizi.

Jamii haina budi kuzienzi na kuzithamini tiba asili, kwa kuwa zimebeba mambo mengi ya kiutamaduni na kisanaa yenye faida kwa jamii. Baadhi ya mambo hayo ni nyimbo ambazo zinaimbwa wakati tiba asili inapotolewa. Nyimbo hizo ni hazina ambayo hudumu miaka mingi. Mtindo wa nyimbo za tiba asili umebeba falsafa, fikra na utamaduni wa jamii inayohusika na husawiri maisha halisi. Hivyo, mtindo wa nyimbo za tiba asili ni kielelezo cha maisha halisi ya jamii za Kiafrika.

Utafiti huu umechunguza mtindo katika nyimbo za tiba asili za waganga wa mkoa wa Ruvuma. Mtindo ni moja ya vipengele vingi vya kifani vinavyopatikana katika fasihi. Hivyo, utafiti mwingine unaweza kufanyika katika vipengele vingine vya fani na hata maudhui ya nyimbo hizo za tiba asili.

7.7 Hitimisho

Utafiti huu umebaini kwamba kuna aina saba za nyimbo za tiba asili zinazobainishwa kulingana na dhima zake. Kama ilivyokwishaelezwa, aina hizo zinahusu maombi, kufariji, kufurahisha mizimu, historia, shukurani, kutolea tiba na nyimbo za kuaga. Aina hizo zitumika kulingana na mahitaji ya kila hatua ya matibabu. Pia, utafiti huu umebainika kwamba, mtindo katika nyimbo za tiba asili hufungamana na muktadha wa kiutendaji. Mtindo haujipambanui kwa lugha tu kama watafiti wengi walivyotanabaisha. Utafiti huu umebaini kuwa mtindo hujipambanua kwa matumizi ya lugha na viziadalugha.

Utafiti huu umebainisha matokeo ya mtindo wa nyimbo za tiba asili kwa wagonjwa. Mtindo wa tiba asili umeonekana kuwa muhimu kwa wagonjwa kwa sababu unawasaidia katika mambo mbalimbali kama vile kuwatia moyo , kuwashirikisha katika mchakato wa tiba, kuburudika, kuwaongezea imani ya tiba na kufukuza majini wabaya. Kubainisha matokeo ya mtindo kwa hadhira kama ilivyo wagonjwa katika nyimbo za tiba asili ni hatua muhimu iliyofikiwa katika utafiti huu tofauti na kaida za awali za kuainisha mtindo bila kutathmini matokeo yake kwa hadhira inayohusika.

MAREJEO

- Abed, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amiri*. Nairobi: KLB.
- Alvuede, C. O. (2006). *Music Therapy in Traditional African Societies: Origin, Basis and Application in Nigeria*. Ekpoma: Ambrose Alli University.
- Babbie, E. (1992). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Bacharach A. L. (1979). *The Musical Companion*. London: Pan Book Ltd.
- Balisidya, M. (1987). “Tanzu za Fasihi Simulizi” katika Temu, C na Mbogo, E. (wah). Mulika na.19. Dar es Salaam: TUKI (Uk.2-11).
- Bakhtin, M. (1986). *Speech Genres and Other Late Essays*, Vern W. McGee (trans.), Caryl Emerson and Michael Holquist (eds.). Austin: University of Austin Press.
- Barthes, R. (1966). *Introduction to the Structuralism Analysis of Narratives. Criticism: The Major statements*. Ed. C. Kaplan. New York: St. Martin’s Press, Inc.
- Bauman, R. (1975). “Verbal Arts as Performance.” Katika American Anthropology New Series, juz. 77, na. 2, kur. 290 – 311. Ilisomwa tarehe 15/02/2020 katika <http://www.jstor.org>.
- Best, J. W., na Kahn, J. V. (1993). *Research in education*. Boston: Allyn and Bacon.
- Best, J. W., na Khan, J. V. (2006). *Research in Education*.(10th ed), New York: Pearson Education inc.
- Bryman, A. (2004). *Social Research Methods* (2nd edition). Oxford: Oxford University Press.
- Buchstaller, I., and Khattab, G. (2013). *Research Methods in Linguistics*. Cambridge University Press.

- Bukofzer, M. (1957). *The place of Musicology in American Institutions of Higher Learning*. New York: Liberal Arts Press.
- Campbell, D. (1991). *Imagery and the Physiology of Music*. In D. Campbell *Music – Physician for Times to Come*. Wheaton, IL: Theosophical Publishing House.
- Cohen, L., na Lawrence, M. (2000). *Research Methods in Education*. London: Route-led Ledge
- Dawson, C. (2002). *Practical Research Methods*. Magdalen Road Ox4IRE United Kingdom: Oxford University Press.
- Dickens, E. (1969). *Encyclopadia International* (Vol. IV). New York: Lexicon Publication Inc.
- Eagleton, T. (1978). *Criticism and Ideology*. New York: Schocken.
- Eco, U. (1984). *Semiotics & Philosophy of Language*. Bloomington: Indiana University Press.
- Encarta, (2009). *Microsoft Encarta Kids*. New York: Microsoft Cooperation.
- Erdtsieck, J. (2001). *Nambela Mganga wa Pepo*. Dar es Salaam: DUP.
- Erlich, V. (1955). *Russian Formalism: History-Doctrine*. The Hague
- Fenner, M. (2010). *Language As a Social Semiotic: The Social Interpretation of Language and Meaning*. University Park Press.
- Finnegan, R. (1977). *Oral Literature in Africa*. Clarendon: Press Oxford.
- Fokkema, D. W., na Kunne-Ibsch, E. (1977). *Theories of Literature in the Twentieth Century*. London: Hurst & Co. Publishers Ltd.
- Foley, J. (1995). *The Singer of the Tales Performance*. Bloomington. Indiana University Press.

- Frankfort-Nachmias, C., na Nachmias, D. (2000). *Research Methods in the Social Sciences* (6th ed). New York: Worth.
- Furlong, N., na Wenzake. (2000). *Research Methods and Statistics. Anintergrated Approach*. New York: Harcourt Collage Publications.
- Gioia, T. (2006). *Healing Songs*. Durham and London: Duke University Press.
- Gouk, P. (2000). *Music Healing in Cultural Contexts*. Aldershot: Ashgate.
- Haji, H. G. (2011). Mitindo ya Nyimbo za Uganga wa Pepo. Tasinifu ya Shahada ya Uzamilim(Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Holden, P. (2000). *Music as Medicine. The History of Music Therapy Since Antiquity*. Aldershot: Ashgate.
- Jakobson, R. (1975). *Fundamental of Language*. Mouton, Paris: The Hague
- Juma, S. U. (2007). Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Matumizi ya Uganga, Tasinifu ya Shahada ya Kwanza (Haijapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.
- Kadallah, R. T. (2018). Utendaji katika Nyimbo za Ngoma ya Wasambaa: Mifano kutoka Mdumange Nchini Tanzania. Tasinifu ya Uzamili Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kahigi, K. K., na Mulokozi, M. M. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam. T.P.H.
- Kezilahabi, E. (1981). "Ushairi na Nyimbo katika Utamaduni Wetu". Katika Omary C. K., na Mvungi, M. *Urithi wa Utamaduni Wetu* (uk.119-137) Dar es Salaam: TPH.
- Kombo, D. K., na Tromp, D. L. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publication Africa.

- Kothari, C. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delh: New Edge International (P) Limited Publishers.
- Kothari, C.R., na Garg, G. (2014). *Research Methodology (Third Edition)*. New Delhi: New Age International Publishers.
- Kumar, R. (1999). *Research Methodology: A step-by-guide for beginners*. New Delhi: SAGE Publication and Co
- Lane, M. (1977). *Structuralism: A Reader*. London: Jonathan Cape.
- Leech, G.N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.
- Leech, G., na Short, M. (1981). *Style in Fiction*. London: Longman.
- Lodico, M. (2010). *Methods in Educational Research: From Theory to Practice (2nd Edition)*. San Francisco, CA: Jossey-Bass.
- Mayoka, J. (1986). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mbiti, J. S. (1969). *African Religions and Philosophy*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Mgogo, Y. P. (2017). Kuchunguza Hadithi za Wanyiha katika Kurithisha Elimu ya Jadi. Tasinifu ya Uzamivu (Haijchapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Miall, D. S., na Kuiken, D. (1994). *Poetics*. University of Alberta
- Mlacha, S. A., na Hurskainen, A. (1995). *Lugha, Utamaduni na Fasihi ya Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mligo, E. S. (2012). *Jifunze Utafiti Mwongozo Kuhusu Utafiti na Utamaduni wa Ripoti Yenye Mantiki*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGY).Mturo, N. (2011). Dhima ya Semi Zilizoandikwa katika Daladala. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijchapishwa). Kikuu cha Dar es Salaam.

- Mulokozi, M. M. (1989). "Tanzu za Fasihi Simulizi". *Mulika* 21: 1-19.
- Mume, J. O. (1973). *Traditional Medicine in Nigeria*. Agbarho: Jom Nature Cure Publishers.
- Musyoka, E. (2012). *Uhakiki wa Kimtindo wa Nyimbo za Mazishi*. Tasinifu Umahiri (Haijachapiswa). Chuo kikuu cha Kenyatta.
- Mwanza, P. M. (2007). *Mtindo wa Nyimbo za Watoto wa Shule za Chekechea*. Tasinifu Umahiri (Haijachapiswa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Neuman, W. L. (2014). *Social Research Methods: Qualitative and Quantitative Approaches* (7th ed.). Essex: Pearson.
- Niane, D. T. (1995). *Sundiata: An Epic of Old Mali* (Revised Edition). Longman African Writers.
- Nketia, J. H. (1982). *The Music of Africa*. London: Victor Gollanez Ltd.
- Nzobe, R. L. (2012). *Fasihi Simulizi na UKIMWI: Mifano Kutoka katika Nyimbo za Ngoma ya Wigashe ya Wasukuma*. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds, Character, and Continuity*. Bloomington: Indiana University Press.
- Patrick, D. (1972). *Shorter Oxford English Dictionary*. Oxford: Oxford University Press.
- Pearce, M. (2019). https://guides.lib.ua.edu/literaturereview_imepakuliwa_04/03/19_12:06 jioni.
- Pearce, M. (2019). http://guides.libraries.psu.edu/emp_imepakuliwa_04/04/19_1:34 jioni

- Polit, D. F., & Hungler, B. P. (1997). *Essentials of Nursing Research: Methods, Appraisals and Utilisation*. 4th edition. Philadelphia: Lippincott-Raven Publishers.
- Pratt, R., and Jones, R. W. (1988). 'Music and Medicine: A Partnership in History.' *International Journal of Arts Medicine*, 6, 377–389.
- Rajabu, A. (2012). *Misemo ya Kiswahili katika Vazi la Fulana: Uchambuzi wa Dhamira na Matumizi ya Lugha. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Rajwayi, A. C. (2009). *Maudhui na Mtindo katika Nyimbo za Faustine Munishi. Tasinifu Umahiri (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Riffaterre, M. (1983). *Text Production*. New York: Columbia University Press.
- Robey, D. (1973). *Structuralism: Introduction*. Wolf College Lecture; 1972. Oxford: Clarendon Press.
- Schechner, R. (2013). *Performance Studies: An Introduction*. New York: Routledge.
- Scholes, R. (1974). *Structuralism in Literature: An Introduction*. New Haven: Yale University Press.
- Sengo, T. S. Y. M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: The Registered Trustee of Al-Amin Education and Research Academy.
- Sengo, T. Y. S. (1978). *Kudidimizwa kwa Fasihi na Wakoloni, Taamuli ya Fasihi Nadharia, Mtazamo na Mbinu za utafiti katika Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: TUKI.
- Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: PPC.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU LTD
- Southern, E. (1971). *Music of Black Americans*. New York: W. W. Norton & Company.

- Suleiman, H. K. (2012). *NyimboZa Ngoma ya Pungwa: Maana Dhima na Athari Yake katika Jamii ya Wazanzibari. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Dodoma.
- The Holy Bible, New International Version. New York: Harrap Collins Publishers.
- Thomson, G. (1946). *Marxism and Poetry*. New York: International publishers.
- Wafula, R. M., & Njogu, K. (2007). *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Sai Industries Limited.
- Wambua, S. (2001). *Mitindo katika Nyimbo za Kakai Kilanzo. Tasinifu Umahiri (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K. W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi*. Mombasa: Phoenix Publishers Limited.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.
- Wamitila, K. W. (2010). *Kichocheo cha Fasihi: Fasihi simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications.
- Wathome, R. W. (2009). *Mitindo katika Nyimbo za Tohara za Jamii ya Wakamba. Tasinifu Umahiri (Haijachapishwa)*. Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Welsh, K. (2010). *African Dance*. Chelsea: Chelsea House Publishers.
- Wigram, T., na Wenzake, (1995). *A Comprehensive Guide to Music Therapy: Theory, Clinical Practice, Research and Training*. London and Philadelphia: Jessica Kingsley Publishers.

Yin, R. K. (1984). *Case Study Research: Design and Methods* (1st ed). Beverly Hills, CA: Sage Publishing.

Yin, R. K. (2011). *Case Study Research: Design and Methods* (4th ed). Thousand Oaks, California: Sage Publications.

VIAMBATANISHO

KIAMBATANISHO A: NYIMBO ZA TIBA ASILI

1. Mababu na Malaika Mtusaidie

Mganga:	Mababu na Malaika kwa uwezo wenu baba mtusaidie	} × 5
Wasaidizi:	Mababu na malaika kwa uwezo wenu baba mtusaidie	
Mganga:	Maombi kwa malaika x 3	
	Maombi yetu wote x2	
Wasaidizi:	Maombi kwa malaika x 3	
	Maombi yetu wote x 2	
Mganga:	Maombi eee maombi eee x2	
Wasaidizi:	Maombi eee maombi eee x2	
Mganga:	Maombi yetu wote	
	Maombi eee x2	
Wasaidizi:	Maombi yetu wote	
	Maombi eee x 2	

2. GWALA MAGANZA (Kibena)

Mganga:	Babu gwala maganza
	Ndevilima x3
Wasaidizi:	Babu gwala maganza
	Ndevilima x 3
Mganga:	Babu gwala maganza
	Ndevilima x3
Wasaidizi:	Babu gwala maganza
	Ndevilima x 3

Tafsiri

- Mganga: Babu tengeneza njia
Tupite salama x3
- Wasaidizi: Babu tengeneza njia
Tupite salama x3
- Mganga: Babu tengeneza njia
Tupite salama x3
- Wasaidizi: Babu tengeneza njia
Tupite salama x3

3. Mgelengana

- Kiongozi: Mgelengana aae dawa x2
Toka zamani aee dawa x1
Tukachimbe dawa
Sisi ni wagonjwa
Mgelengana x 2
- Wazumi: Mgelengana aae dawa x2
Toka zamani aee dawa x1
Tukachimbe dawa
Sisi ni wagonjwa
Mgelengana x 2
- Kiongozi: Baba wote dawa
Mgelengana baba
Mama eee dawa x 3
- Wazumi: Baba wote dawa
Mgelengana baba
Mama eee dawa x 3

4. Walala chini

Kiongozi: Walala chini eee
 Wazumi: Wana nguvu sana
 Wananguvu sana
 Kiongozi: Kweli tuwaombe
 Wazumi: Wananguvu sana
 Kiongozi: Watusaidie
 Wazumi: Wana nguvu sana

5. Alalonga Lunoge (Kibena) Mganga: Nani alalonga lunoge

Alonga lunoge
 Wazumi: Nani alalonga lunoge
 Alonga lunoge
 Mganga: Nani alalonga lunoge (babu)
 Alonga lunoge (bibi)
 Wazumi: Nani alalonga lunoge (babu)
 Alonga lunoge (bibi)

Tafsiri

Mganga: Nani amesema utapona
 Amesema utapona
 Wazumi: Nani amesema utapona
 Amesema utapona
 Mganga: Nani amesema utapona (babu)
 Amesema utapona (bibi)
 Wazumi: Nani amesema utapona (babu)
 Amesema utapona (bibi)

6. Tucheze ngoma

Kiongozi: Twendeni jamani eee x 2

Twendeni jamani tucheze ngoma eee x 2

Wazumi: Twendeni jamani eee x 2

Twendeni jamani tucheze ngoma eee x 2

7. Nipe udi

Mganga: Nipe udi na ubani mwalimu } bila vifaa

Nipe udi wana ubani }

Wazumi: Nipe udi na ubani mwalimu } Mauunange

Nipe udi na ubani }

Mganga: Wee! Nipe udi na ubani mwalimu } Manyanga na ngoma

Nipe udi na ubani tuombe }

Wazumi: Nipe udi na ubani mwalimu }

Nipe udi na ubani }

8. Mjukuu analia

Mganga: Mjukuu aee

Mjukuu analia aee

Wazumi: Mjukuu aee

Mjukuu analia aee

Mganga: Mjukuu aeee

Baba mjukuu analia aee

Wazumi: Mjukuu aeee

Baba mjukuu analia aee

Mganga: Tukachimbie dawa

Mjukuu aee

Mjukuu analia aee

Wazumi: Mjukuu aee

Mjukuu analia aee

Nipe dawa nzuri

- Mganga: Nilikwenda Kisimani
 Nikamkuta jini
 Jini wangu **mganga** huyo
 Nipe dawa jini
- Wazumi: Nilikwenda Kisimani
 Nikamkuta jini
 Jini wangu **mganga** huyo
 Nipe dawa jini x 4
- Mganga: Nipe dawa nzuri
 Nipe dawa nzuri
 Nipe dawa nzuri
 Nipe dawa nzuri x 4
- Wazumi: Nipe dawa nzuri
 Nipe dawa nzuri
 Nipe dawa nzuri
 Nipe dawa nzuri x 4

Nole nole

Mganga: Nole nole
 Aee! Nole nole
 Nole nole aee
 Jini wa milima
 Fukuza homa

Wazumi: Nole nole
 Aee! Nole nole
 Nole nole aee
 Jini wa milima
 Fukuza homa

Mganga: Nole nole
 Aee! Nole nole
 Nole nole aee
 Jini wa milima
 Fukuza homa

Wazumi: Nole nole
 Aee! Nole nole
 Nole nole aee
 Jini wa milima
 Fukuza homa

Mganga: Aee! Nole nole
 Nole nole aee
 Jini wa bahari
 Punguza homa

Wazumi: Aee! Nole nole
 Nole nole aee
 Jini wa bahari
 Punguza homa

9. Furaha

- Kiongozi: Furaha furaha furaha ee
Furaha furaha furaha leo x 2
- Wazumi: Furaha furaha furaha ee
Furaha furaha furaha leo x 2
- Kiongozi: Furaha furaha furaha eeh
Furaha furaha furaha ya majini
- Wazumi: Furaha furaha furaha eee
Furaha furaha furaha eee
- Kiongozi: Ushindi ushindi ushindi ee
Ushindi, ushindi, ushindi ee
- Wazumi: Furaha, furaha, furaha ee
Furaha, furaha, furaha ee
- Kiongozi: Amani, amani, amani ee
Amani, amani, amani ee
- Waitikiaji: Furaha, furaha, furaha ee
Furaha, furaha, furaha ee

10. Ningalonga Ndauli (Kibena)

- Mganga: Ningalonga ndauli x2
- Wazumi: Ningalonga ndauli x 2
- Mganga: Ningalonga ndauli x 2
- Wazumi: Ningalonga ndauli x 2
- Mganga: Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lizoka
- Wazumi: Ningalonga ndauli, pa nyumba pana lizoka
- Mganga: Babu uunange, babu uunange
- Washiriki: Babu uunange, babu uunange
- Mganga + Wazumi: Pa nyumba pana lisoka
- Mganga: Pana lisoka, pana lisoka
- Wazumi: Pana lisoka, pana lisoka
- Mganga + Wazumi: Pana nyumba pana lisoka

Mganga: Babu uunange, babu uunange, pa nyumba pana lisoka
 Wazumi: Babu uunange, babu uunange, pa nyumba pana lisoka

11. Mganga

Kiongozi: Mganga uko wapi eee, dada
 Kuniacha peke yangu ee, naumia
 Wazumi: Mganga uko wapi eee, dada
 Kuniacha peke yangu eee, naumia
 Kiongozi: Mganga uko wapie eee, dada
 Kuniacha peke yangu nateseka
 Wazumi: Mganga uko wapie eee, mwalimu

12. Ubaya

Kiongozi: Ubaya wee, ubaya wee
 Binadamu ubaya, uache ubaya
 Wazumi: Ubaya wee, ubaya wee
 Binadamu ubaya, uache ubaya
 Kiongozi: Uache ubaya
 Wazumi: Ubaya, mwanadamu, ubaya
 Kiongozi: Uache ubaya
 Washiriki: ubaya, mwanadamu, ubaya

13. Mizimu

Mganga: Wee mizimu, wee mizimu
 Wazumi: Mizimu kalili mwana wee mizimu
 Mganga: Mababu wee mababu
 Wazumi: Mababu kalili mwana x 4
 Mganga: Mumsaidie
 Wazumi: Mababu kalili mwana mababu
 Mganga: Mumsaidie
 Wazumi: Mababu kalili mwana mababu

Mganga: Anahangaika
 Afanye nini mwana?
 Wazumi: Wanaitikia vivyo hivyo
 Mganga: Mmsaidie na maombi yake
 Wazumi: Anahangaika
 Mumhurumie

14. Tuombe

Kiongozi: Wee tuombe daima
 Aee daima
 Na majini wa milimani tabu sana
 Aee daima
 Wazumi: Wee tuombe daima
 Aee daima
 Na majini wa milimani tabu sana
 Aee daima

Kiongozi: Tuimbe wote daima aee, baba
 na majini wa milimani tabu leo
 aee daima

Wazumi: Tuimbe wote daima aee, baba
 na majini wa milimani tabu leo
 aee daima

Kiongozi: Ena ena daima
 Aee daima
 Na majini ya milimani tabu sana

Wazumi: Tuimbe wote daima aee, baba
 Na majini wa milimani tabu leo
 aee daima

Kiongozi: Tuombe na mababu
 Aee daima
 Na majini ya milimani tabu sana

Wazumi: Tuombe na mababu
Aee daima
Na majini ya milimani tabu sana

15. Hodi hodi Mwalimu

Kiongozi: Hodi hodi mwalimu ee
Hodi hodi mwalimu
tumetoka Kilimanjaro x3

Wazumi: Hodi hodi mwalimu ee
Hodi hodi mwalimu
tumetoka Kilimanjaro x3

Kiongozi: Naingia mwalimu x 3
Nimetoka Kilimanjaro
Hodi mwalimu

Wazumi: Hodi hodi mwalimu ee
Hodi hodi mwalimu
tumetoka Kilimanjaro x3

16. Nahuma kumwembe

Kiongozi: Nahuma kumwembe
Na wile kutoka mwalimu nawe njala

Wazumi: Nahuma kumwembe
Na wile kutoka mwalimu nawe njala

Kiongozi: Kutoka kumwembe

Wazumi: Nawe njala

17. Naluta

Kiongozi: Unene naluta

Wazumi: Ndegelela

18. Liyaule

Kiongozi: Liyaule

Wazumi: Kumagongo

19. Tuombe na Malaika

Mganga: Tuombe tuombe tuombe na malaika

Mganga + Wazumi: Tuombe tuombe tuombe watusaidie

Mganga + Wazumi: Tuombe tuombe tuombe na malaika

Mganga + Wazumi: Tuombe tuombe tuombe majini yote

20. Tumekuja

Mganga: Tulikuja na mzunguko

Wazumi: Tunarudi na mzunguko

Wee jini eee

21. Tunakuomba baba

Mganga: Tunakuomba baba

Majini yote mwana

Tufungulie mwanga

Tuonee huruma

Wazumi: Tunakuomba baba

Majini yote mwana

Tufungulie mwanga

Tuonee huruma

Mganga: Tunaomba majini yote

Mtufungulie mwanga

Mtuonee huruma

Wazumi: Tunaomba majini yote

Mtufungulie mwanga

Mtuonee huruma

Teleza

- Mganga: Tuleza teleza wee
Majini yote teleza wee
- Wazumi: Tuleza teleza wee
Majini yote teleza wee
- Mganga: Teleze majini yote
Teleza wamilima
Teleza wamabonde
- Wazumi: Teleze majini yote
Teleza wamilima
Teleza wamabonde
- Mganga: Tunakuomba
Teleza weee teleza
- Wazumi: Tunakuomba
Teleza weee teleza

22. Njoo Tuonane

- Mganga: Abubakari jini, njoo tuonane
- Wazumi: Abubakari jini, njoo tuonane
- Mganga: Panda milima jini, njoo tuonane
- Wazumi: Panda milima jini, njoo tuonane

23. Kalima

- Kiongozi: Kalima kale kadogo wee nashindwa kupanda
- Wazumi: Kalima kale kadogo wee nashindwa kupanda
- Kiongozi: Kale kadogo nashindwa kupanda
- Wazumi: Kale kadogo nashindwa kupanda
- Kiongozi: Ukamweleze mwalimu akapande
- Wazumi: Ukamweleze mwalimu akapande

Twende

Kiongozi: Twende twende kwa Hidaya

Wazumi: Twende twende kwa Hidaya

Kiongozi: Msiniache jamani

Chonde chonde

Kwa Hidaya kwende

Wazumi: Twende twende kwa Hidaya

Kiongozi: Umeniacha kusudi

Twende twende

Kwa Hidaya twende

Wazumi: Twende twende kwa Hidaya

24. Sina Wema

Mganga: Sina wema umekuja kufanya nini

Wazumi: Kuokoa kuoa

Mganga: Kuokoa binadamu

Wazumi: Kuokoa kuoa

Mganga: Kuokoa wenye homa

Wazumi: Kuokoa kuoa

Mganga: Sina wema

Wazumi: Kuokoa kuokoa

Mganga: Chonde chonde

Wazumi: Kuokoa kuokoa

25. Kwa herini

Mganga: Kwa herini, aee

Wazumi: Kwa herini, aee

Mganga: Tutaonana, aee

Wazumi: Tutaonana, aee

Mganga: Mungu akipenda, aee

Wazumi: Mungu akipenda, aee

Mganga: Bai bai tutaonana, aee
 Wazumi: Bai bai tutaonana, aee
 Mganga: Tuombe mungu, aee
 Wazumi: Tutaonana, aee

26. Fungua Milango

Mganga: Fungua milango x 2
 Fungua milango baba majini yapite
 Wazumi: Fungua milango x 2
 Fungua milango baba majini yapite
 Mganga: wee! fungua milango aeeh baba
 Fungua milango baba majini yapite
 Wazumi: wee! fungua milango aeeh baba
 Fungua milango baba majini yapite
 Mganga: wee! tunakuomba, aiee baba
 Tunakuomba, tunakuomba
 Tunakuomba baba utusaidie
 Wazumi: wee! tunakuomba, aiee baba
 Tunakuomba, tunakuomba
 Tunakuomba baba utusaidie
 Mganga: wee! Mungu wa milima
 Tunakuomba, utusaidie
 Wazumi: wee! mungu wa milima
 Aiee baba, aee baba, aiee babu
 Utasaidie
Wimbo wa kufungua
Unafuata wimbo wa kufagia uwanja.

27. Byagile

- Mganga: byagile, byagile kawanja eeh
 Wazumi: byagile, byagile kawanja eeh
 Mganga: byagile, byagile kawanja eeh
 byagile, kawanja, kakonde
 Wazumi: byagile, byagile kawanja eeh
 byagile kawanja kakonde
 (kiyao)

Tafsiri

- Mganga: fagia, fagia, uwanja eeh
 Wazumi: fagia, fagia, uwanja eeh
 Mganga: fagia, fagia, uwanja eeh
 fagia, fagia, upendeze
 Mganga: fagia, fagia, uwanja eeh
 fagia, fagia, upendeze
*tafsiri: neno kakonde kwa kiyao ni kustawi, hapa tumetafsiri kwa kuzingatia
 maana ya mshororo.
 Kupiga ngoma huku watu wanazunguka kufanya usafi*

28. Tangulia Twende

- Mganga: Nasema tangulia, tangulia twende, alaa
 tangulia twende, tangulia wee
 tangulia, tangulia twende, alaa
 wazumi: tangulia twende, tangulia wee
 tangulia, tangulia twende, alaa
 mganga: tangulia twende, tangulia twende
 tangulia twende, ukiwa mwalimu
 wazumi: tangulia twende
 mganga: tangulia twende, tangulia twende, alaa
 wazumi: tangulia twende, tangulia twende

mganga: tangulia twende, milimani
 wazumi: tangulia twende
 mganga: tangulia twende, baharini
 wazumi: tangulia twende
 mganga: tangulia twende, mapangoni
 wazumi: tangulia twende

29. Hodi pa Chilambo

mganga: hodi pa chilambo
 hodi pa chilambo aeheh
 wazumi: karibu pa chilambo
 karibu pa chilambo aeheh
 (wimbo unarudiwa rudiwa)
 (kiyao)

Tafsiri

Mganga: hodi duniani
 hodi duniani aeheh
 wazumi: karibu duniani
 karibu duniani aeheh

30. Mungu na Malaika

mganga: tunaomba dua
 wazumi: mungu na malaika
 mganga: tunaomboleza
 wazumi: mungu na malaika
 mganga: utusaidie
 wazumi: mungu na malaika

31. Chonde

Mganga: aaaa, eee, aaaa, eee, aaaa
 Wazumi: aaaa, eee, aaaa, eee, aaaa
 Mganga: chonde, eee, chonde, eee,
 chonde, eee, chonde, eee, malaika, aaaa
 Wazumi: aaaa
 Mganga: tusaidie tupate dawa, dawa za majini,
 dawa za mti mkubwa, dawa za pangoni
 dawa za milimani
 Wazumi: aaaa

32. Hodi

Mganga: Hodi hodi eee x 2
 Paluwanja hodi eee
 Wazumi: Hodi hodi eee x2
 Paluwanja hodi eee
 Mganga: Hodi, hodi, chonde hodi ee x2
 Paluwanja hodi eee
 Wazumi: Hodi, hodi, hodi ee x2
 Paluwanja hodi eee
 Mganga: Hodi, hodi, mababu hodi ee x2
 Paluwanja hodi eee
 Wazumi: Hodi, hodi, hodi ee x2
 Paluwanja hodi eee
 Mganga: Hodi, hodi, mizimu hodi ee x 2
 Paluwanja hodi eee
 Wazumi: Hodi, hodi, hodi ee x 2
 Paluwanja hodi eee

33. Daima

Mganga: daima wee, daima we, aee daima
 daima wee, milimani aee daima
 wazumi: daima wee, daima we, aee daima
 daima wee, milimani aee daima
 (Unarudiwa mara nyingi)

34. Mazoea

Mganga: Jamani mazoea, mazoea leo, mazoea eee
 Mazoea tuna tabu, mazoea leo, mazoea eee
 Kila siku milimani, mazoea leo, mazoea eee
 Kila siku mapangoni, mazoea leo, mazoea eee
 Kila siku hatulali, mazoea leo, mazoea eee
 Kila siku mapigano, mazoea leo, mazoea eee
 Ninasema chonde chonde, mazoea leo, mazoea eee

Wazumi: Mazoea tabu, kila siku tabu

Mganga: Jamani mazoea, mazoea leo, mazoea eee
 Mazoea tuna tabu, mazoea leo, mazoea eee
 Sikiliza maombi, mazoea leo, mazoea eee
 Wanao tuna shida, mazoea leo, mazoea eee
 Tunaomba ulinzi wako, mazoea leo, mazoea eee
 Tunaomba usaidizi wako, mazoea leo, mazoea eee
 Mazoea tunatabu, mazoea leo, mazoea eee
 Kila siku misituni, mazoea leo, mazoea eee
 Wazumi: Mazoea tabu, kila siku tabu

35. Ndembekulugwa

- Mganga: Ndembekulugwa, ndembekulugwa wewe?
Ndembekulugwa, ndembekulugwa eee
Ndembekulugwa, kupalapala mikongo
- Wazumi: Ndembekulugwa, ndembekulugwa uweje?
Ndembekulugwa, ndembekulugwa eee
Ndembekulugwa, kupalapala mikongo
- Mganga: kupalapala mikongo, uweje
- Wazumi: Ndembekulugwa, kupalapala mikongo
- Mganga: kupalapala mikongo, eee, uweje
- Wazumi: Ndembekulugwa, kupalapala mikongo

Tafsiri:

- Mganga: Mungu mkubwa, mungu mkubwa, wewe
Mungu mkubwa, mungu mkubwa, eee
Mungu mkubwa, tusaidie kupata dawa
- Wazumi: Mungu mkubwa, mungu mkubwa, wewe
Mungu mkubwa, mungu mkubwa, eee
Mungu mkubwa, tusaidie kupata dawa
- Mganga: Mungu mkubwa, wewe
- Wazumi: Mungu mkubwa, tusaidie kupata dawa
- Mganga: Mungu mkubwa, eee, wewe
- Wazumi: Mungu mkubwa, tusaidie kupata dawa

36. Randaranda

- Mganga: nasema randaranda, randaranda, randa eee
randaranda, randaranda, randa eee
milimani randaranda eee
- wazumi: aae, eee, eee
- Mganga: randaranda, randaranda, randa eee
randaranda, randaranda, randa eee

wazumi: aaeee, eee, eeee
 mganga: kuranda waranda usiku eee
 wazumi: aaeee, eee, eeee
 mganga: mchana mwaona haya eee
 wazumi: aaeee, eee, eeee
 Mganga: randaranda, randaranda, randa eee
 randaranda, randaranda, randa eee
 miungu yote randa eee
 wazumi: aaeee, eee, eeee
 Mganga: randaranda, randaranda, randa eee
 randaranda, randaranda, randa eee
 wazumi: aaeee, eee, eeee
 mganga: kuranda waranda usiku eee
 mganga: mchana mwaona haya eee
 wazumi: aaeee, eee, eeee

Sina Baba wala Mama

Mganga: Sina baba wala mama
 Siwezi kupanda mlima
 Miungu nisaidie
 siwezi kupanda mlima
 Wazumi: siwezi kupanda mlima
 Mganga: chonde, chonde nisaidie
 Wazumi: siwezi kupanda mlima
 Mganga: miungu yote nisaidie
 Wazumi: siwezi kupanda mlima
 Mganga: chonde, chonde nisaidie
 Wazumi: siwezi kupanda mlima
 Mganga: mahoka, nisaidie
 Wazumi: siwezi kupanda mlima
 Mganga: mti mkubwa, nisaidie
 Wazumi: siwezi kupanda mlima

37. Pepele Mahoka

Mganga: Pepe pepe

pepele mahoka

mganga: Pepe pepe

wazumi: pepele mahoka

tafsiri:

mganga: pepea, pepea

pepea mizimu/miungu

mganga: pepea, pepea

wazumi: pepea mizimu/miungu

38. Kumala Vandu

mganga: ngangana nangololo

chonde chonde

ngangana nangololo

wazumi: kumala vandu

Tafsiri

Mganga: mchawi mkuu

chonde chonde

mchawi mkuu

wazumi: unamaliza watu

39. Ndege

Mganga: ndege, ndege

Wazumi: ndege milimani

Mganga: nikawinde ndege

Wazumi: ndege milimani

40. Twakaribisha Wageni

Mganga: Tuwakaribishwe wageni

kutoka marikiti waganga

wazumi: Tuwakaribishwe wageni

kutoka marikiti waganga

mganga: kutoka marikiti waganga

wazumi: waganga

41. Ndendeuli

Mganga: Ndendeuli, ndendeuli

Na manyanga, ndendeuli x3

Wazumi: ndendeuli na manyanga, ndendeuli

Mganga: ndendeuli, ndendeuli

Pakuvina, ndendeuli

Wazumi: ndendeuli na manyanga, ndendeuli

42. Mwanakimbunga

Mganga & wazumi: Mwanakimbunga, mwanajojo

Mwanakimbunga, nyangalile

Nyangalile, mwanakimbunga

Mwanajojo, nyangalile

Nyangalile, mwanajojo

43. Nelele Mwanangu

Mganga: Nelele mwanangu, Nelele mwanangu

Wazumi: Nelele mwanangu

Mganga: Nelele mwanangu aee

Wazumi: Nelele mwanangu

Tafsiri

mganga: nilele wanangu, nilele wanangu

wazumi: nilele wanangu

mganga: nilele wanangu aee

wazumi: nilele wanangu

44. Vandu Vavava

Mganga: nole Vandu, Vandu vavava

Wazumi: Vandu, Vandu vavava

Tafsiri

Mganga: angalia watu, watu hawa hawa

Wazumi: watu, watu hawa hawa

45. Hodi Hodi

Mganga: Hodi hodi, nje x2

Wazumi: Hodi hodi, nje x2

Mganga: Hodi hodi, nje x2

Tutatue matatizo

Wazumi: Hodi hodi, nje x2

Tutatue matatizo

46. Nipeleke kwa Mganga

Mganga: Nipeleke, Nipeleke, Nipeleke aae

Nipeleke kwa mganga

Wazumi: Nipeleke, Nipeleke, Nipeleke aae

Nipeleke kwa mganga

47. Uganga wangu umechukuliwa

Mganga: Uganga wangu umechuliwa, na watu wabaya x2

Wazumi: na watu wabaya

Mganga: umechukuliwa wote

Wazumi: na watu wabaya

48. Twende Tukachimbe

Mganga: Panda mlima, telemka bonde

Wazumi: tukachimbe dawa

Mganga: ooo, iii, eee x2

Wazumi: tukachimbe dawa

49. Furahia

Mganga: Furahia furahia furahia x2

Wazumi: Furahia furahia furahia x2

Mganga: Maombi yetu yamepita, salama

Wazumi: Mganga: Maombi yetu yamepita, salama

50. Dawa ni Dawa

Mganga: Dawa dawa dawa ni dawa x 3

Wazumi: Dawa dawa dawa ni dawa x 3

Mganga: Kutoka milimani, pangoni hadi ziwani, aeeeh dawa x 2

Wazumi: Kutoka milimani, pangoni hadi ziwani, aeeeh dawa x 2

Mganga: Kutoka kwa mababu na mizimu aeeeh dawa x2

Wazumi: Kutoka kwa mababu na mizimu aeeeh dawa x2

Mganga: Dawa za mizizi dawa, aeeh dawa

Wazumi: Dawa za mizizi dawa, aeeh dawa

Mganga: Dawa za maji dawa, aeeh dawa

Wazumi: Dawa za maji dawa, aeeh dawa

Mganga: Dawa za majani dawa, aeeh dawa

Wazumi: Dawa za majani dawa, aeeh dawa

KIAMBATANISHO B: MWONGOZO WA MASWALI YA UTAFITI**Sehemu 1: Taarifa za Muhojiwa**

- (i) Majina Jinsia
- (ii) Kijiji unachotoka Kata

Sehemu 2: Maswali ya Utafiti

Tasinifu hii inahusu **KUCHUNGUZA MTINDO KATIKA NYIMBO ZA TIBA ASILI: Mifano kutoka Nyimbo za Waganga wa Mkoa wa Ruvuma**

Tafadhali tunaomba ushiriki wako katika kujibu maswali yafuatayo:

1. Je, kwanini nyimbo huimbwa wakati wa tiba asili?
2. Je, nyimbo zina umuhimu wowote katika tiba asili?
3. Je, kuna mavazi maalumu huvaliwa wakati wa kuimba nyimbo za tiba na kama yapo yana umuhimu gani?
4. Je, ni vifaa gani hutumika wakati wa kuimba nyimbo za tiba asili na vina umuhimu gani?
5. Je, kuna sehemu maalumu ya kuimbia nyimbo?
6. Je, washiriki katika uimbaji ni kina nani ?
7. Je, lugha gani hutumika wakati wa kuimba nyimbo za tiba asili ?

MWONGOZO WA USHUHUDIAJI

1. Kushuhudia matendo yanayoambatana na uimbaji
2. Kushuhudia matendo yanayoambatana na uchezaji
3. Kushuhudia matumizi ya vifaa vya kimuziki katika uimbaji
4. Kushuhudia kinachomtokea mgonjwa wakati wa uimbaji
5. Kushuhudia kinachomtokea mgonjwa baada ya uimbaji

KIAMBATANISHO C: VIBALI VYA UTAFITI



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA RUVUMA

Simu Nambari 025-2602256/2602

Fax No. 2602144

E-mail. rasuvuma@pmoralg.go.tz



OFISI YA MKU MKOA,

S. L. P. 74,

SONGEA

Kumb. Na. EA.152/283/01/W/80

18 Julai, 2017

Mkurugenzi wa Manispaa,
S.L.P 14,
SONGEA.

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
SONGEA.

YAH: KIBALI CHA KUFANYA UTAFITI

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.


Mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huria Tanzania Bw. Willy Migolela ameomba kufanya utafiti kuhusu “ **Kuchunguza Mtindo Katika Nyimbo za Tiba Asili; Mifano Kutoka Nyimbo za Waganga wa Mkoa**”.

Ofisi imempa ruhusa ya kufanya utafiti huo kuanzia tarehe 18 Julai, 2017 hadi tarehe 8 Septemba, 2017. Kwa barua hii namtambulisha kwako na kumpa ushirikiano ili aweze kutimiza lengo lake.



Joel Mbewa
**KNY: KATIBU TAWALA MKOA
RUVUMA**

KIAMBATANISHO D: MAKALA



**Mkwawa Journal
of
Education and Development**

Volume Number: 1

Issue Number: 1

Year: 2017




Table of Contents

**Maasai Girls' Education Aspirations and Socio-Cultural Const
from Monduli Tanzania.....**

Adella R. Mtey

Dhamira za Maandishi ya Kuta za Vyooni Jijini Dar es Salaam.....

Willy Migodela

The Swahili Noun Phrase in its Sentential Aspect

Amani Lusekelo

Tafsiri ya Majina Maalumu ya Kibantu: Umuhimu na Changamoto

Fokas Nehimbi

**Emerging Street Youth Violent Groups in Musoma: What is the
Parents' Socio-Ec.....**

Faustine Bwire I

Mustakabali wa I

wa Maudhui ya Si

Gervas Kawonga

Editorial Note

The Editor-In-Chief, on behalf of the Editorial Board and Reviewers, is pleased to announce the launching of Mkwawa Journal of Education and Development (MJED). MJED is a peer-reviewed multidisciplinary journal published by Mkwawa University College of Education (MUCE), a constituent College of the University of Dar es Salaam. The objective of MJED is to be an international forum for publishing high-quality research papers on education, science, humanities and social sciences. As such, the journal aspires to be vigorous, engaging and accessible, and at the same time integrative and challenging. The MJED will be published biannually.

The Editor-In-Chief and Editorial Board wish to thank and congratulate the authors who submitted papers to the first issue of MJED. This journal cannot be a success without the valuable contributions of readers. We hereby invite you to submit a research paper, short note or a review. We can also consider occasional publication of special issues which include updated and expanded papers presented at conferences, subject to acceptance following rigorous peer review. Papers that you wish to submit, either individually or collaboratively, are much appreciated and will make a substantial contribution to the early development and success of the journal.

Best wishes and thank you in advance for your contribution to MJED


Prof. William A. L. Anangisye
Editor-in-Chief



Printed by TUKI

ISSN: 2453-4040 (Print)
eISSN: 2453-4059 (Online)
Mwera Journal of Education and Development





2.2 Populesheni na Sampuli ya Utafiti

Populesheni ni idadi ya watu, makundi ya watu au vitu vyote ambavyo mtafiti hutumia kukamilisha utafiti wake (Babbie, 1999). Populesheni lengwa ya utafiti huu ni kuta za vyoo kumi ambapo vinne ni kutoka Manispaa ya Ilala na sita kutoka Manispaa ya Kinondoni. Vyoo hivi vinajumuisha vile vilivyopo katika sehemu za umma kama vile sokoni, kituo cha basi, shuleni na vyuoni. Sababu ya kuwa na mchanganyiko huu wa vyoo ni kuwezesha kupatikana data zenye mitazamo mbalimbali ya watumiaji wake.

Makala haya yametumia data za msingi. Data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine kwa minajili ya uchambuzi. Hivyo, data hizi ni halisi (Kothari, 1992). Kwa msingi huu basi, data za msingi za makala haya zilikusanywa kutoka katika kuta za vyoo kumi vilivyopo Manispaa ya Ilala na Kinondoni. Lengo la kuchagua vyoo hivyo ni kwamba vitasaidia kutoa data zitakazokidhi mahitaji ya makala haya.

2.3 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu iliyotumika katika utafiti huu ni uchambuzi matini. Uchambuzi matini ni mbinu ya kukusanya data ambapo mtafiti husoma matini au maandishi ya kitaaluma na yasiyo ya kitaaluma na kisha kubaini data na taarifa zihusuzo utafiti wake na kuzirekodi katika shajara (Kothari, 2008). Hivyo basi, mbinu hii imetumika kukusanya data za msingi. Mtafiti aliingia katika vyoo lengwa na kupiga picha maandishi yaliyoko katika kuta za vyoo hivyo kwa kamera. Baada ya hapo, aliyahamishia katika sharaja maalumu iliyoandaliwa na kisha kusoma data moja baada ya nyingine. Katika usomaji wa data hizo ndipo data za kukidhi mahitaji ya makala haya zilipatikana. Kwa mantiki hiyo, mbinu hizi zimetuwezesha kubaini maandishi yaliyoandikwa katika kuta za vyoo yenye dhamira mbalimbali na kuonesha nafasi ya dhamira hizo kwa jamii.

3. Kiunzi cha Nadharia

Makala haya yameongozwa na nadharia ya Elimu-mitindo. Uteuzi wa nadharia hii ulifanyika kutokana na utofauti wa mitindo ya uandishi unaopatikana kutoka kwa waandishi wa maandishi ya vyoo. Enkvist (1973) anasema kuwa elimu mitindo ni kaida za utofauti kati ya kazi mbalimbali za kisanaa kama ilivyo kwenye ushairi, riwaya na tamthiliya. Anaendelea kusema kuwa hatuwezi kujua mtindo wa mwandishi kwa kuangalia kazi yake moja tu, bali kwa kutumia kazi zake mbalimbali ndipo tutangundua mtindo wa mwandishi husika. Kwa jumla, tunaweza kusema kuwa mtindo ni namna lugha inavyoweza kutumika tofauti tofauti kuendana na muktadha na lengo. Hivyo, kwa kuangalia mtindo wa maandishi ya vyoo itasaidia kubainisha dhamira zinazoibuka kutoka kwa waandishi wa vyooni na nafasi za dhamira hizo katika jamii.

Mjall na Kuiken (1994) wanasema kuwa elimu mitindo ni miongoni mwa vipengele muhimu sana vinavyotofautisha baina ya kazi za kifasihi na zile zisizo za kifasihi. Kazi kama vile za ushairi hutofautiana na maandishi mengine kama ya hotuba na risala. Mitindo inayotumika kwenye kazi ya Fasihi ni tofauti na ile ya mawasiliano ya kawaida. Hivyo, nadharia hii imetuongoza katika uchambuzi wetu wa data, kwa minajili ya kudavua mtindo wa maandishi ya vyooni ili kubainisha dhamira zinazoibuka kutokana na mitindo hiyo na nafasi za dhamira hizo katika jamii.

4. Mapitio ya Maandiko kuhusu Maandishi ya Sehemu za Umma na Chooni

Watafiti mbalimbali wamefanya tafiti juu ya dhamira za maandishi ya sehemu za umma Tanzania. Mahenge (2009) alifanya uchunguzi wa fani na maudhui katika semi zilizoandikwa katika tiketi za daladala Dar es salaam. Daladala ni usafiri wa umma. Hivyo, maandishi yanayopatikana kwenye tiketi ni moja ya maandishi ya sehemu za umma. Katika fani, alichunguza baadhi ya vipengele kuhusiana na misemo iliyoko katika tiketi hizo. Vipengele hivyo ni tamathali za usemi, sitiari, metonimia, tashbihi, tashihisi, picha, takriri na wahusika. Vipengele vya maudhui alivyowichunguza ni dhamira. Alipata dhamira kuhusu maradhi ya UKIMWI, imani kwa Mungu, ibada, kazi na sala. Pia, miongozo ya maisha, wajibu wa abiria, ushoga kuwa laana, umuhimu wa tiketi, umuhimu wa kufanya kazi, tabia njema, subira, ukarimu, maadili, ukweli wa maisha na mapenzi. Vipengele vingine vya maudhui ni pamoja na falsafa, itikadi, migogoro na ujumbe.

Baada ya kuchambua fani na maudhui, kimaudhui, mtafiti alithibitisha kuwa misemo iliyopo kwenye tiketi za daladala inaakisi maisha ya kila siku. Kwa upande wa fani, mtafiti alionyesha jinsi vipengele hivyo vinavyoweza kuakisi maisha ya wanajamii, hasa kwa kupitia matumizi ya lugha na mitindo ya maandishi. Utafiti wa Mahenge ulikuwa ni msada mkubwa katika utafiti wetu wa maandishi ya vyoo kwa sababu chooni nako ni sehemu za umma. Hata hivyo, mandhari ya chooni na daladala ni tofauti. Hivyo, ilitazamiwa kuwa hata matumizi ya lugha ni tofauti, ingawa yangeweza kufanana kwa sehemu fulani. Utafiti huu ulifanywa ili kubainisha dhamira za maandishi ya vyooni na nafasi yake kwa jamii.

Fischer (2009) alifanya utafiti wake kuhusu mawasiliano yanavyoweza kufanyika kwa kutumia maandishi ya vyooni. Utafiti wake aliufanya katika vyoo vya wanawake. Fischer aligundua mijadala mbalimbali inayohusu masuala ya kidini, mapenzi na uhusiano (urafiki). Katika mawasiliano hayo, lugha inayotumika ni lugha ya kishairi, lugha ya nathari, maswali, majibu na mara chache, kuna mafumbo. Alihitimisha kwa kupata grafiti zenye maandishi yenye adabu, na yenye kutoa mwelekeo wa uhuru wa maamuzi kwa wasiojamini. Alifanya utafiti wake kwa kuegemea kwenye kipengele cha mawasiliano na uharabu. Utafiti huo haukuwa wa kifasihi, lakini unatoa mwanga na mwelekeo mzuri katika makala haya.

5.0 Dhamira za Maandishi ya Kuta za Vyooni

Msokile (1992) anasema kuwa dhamira ni mawazo yanayoelezwa katika kazi ya sanaa. Naye Wamitila (2003) alidai kwamba dhamira ni istilahi ambayo hutumiwa kuelezea wazo kuu katika hadithi au riwaya, tamthiliya, hadithi fupi, shairi, na kadhalika. Wazo hilo huhusiana na lengo la mwandishi wa kazi hiyo. Pia huweza kutumiwa kueleza lengo kuu la utunzi. Katika Fasihi kuna vipengele mbalimbali ambavyo ndivyo vijenzi vya maana ya utungo na hufanya kazi ya kuumba dhamira. Kwa hakika, suala la dhamira kama kiini cha tungo za kisanaa ndilo linalosawiriwa ndani ya kazi ya Fasihi. Katika utafiti wetu tumewasilisha na kuchambua dhamira mbalimbali zitokanazo na maandishi ya chooni kama ifutavyo:

5.1 Kuhusu Dini

Waumini wa dini za Kikristo na Kiislamu, wote kwa pamoja, wameonesha imani zao kwa kuasa na kuelimisha watu katika maandishi ya chooni. Kwa dini zote mbili, hofu ya maisha na kifo imejitokeza. Waandishi wa maandishi hayo wanasema, “Swali kabla hujaswaliwa kifo mbele yetu.” Pia mwingine anasema, “Moto uko tayari, heri uokoke leo” kabla hujafikia hukumu ya maneno yako! Mafundisho ya dini zote yanaonesha kuwa duniani tunapita tu, hivyo ni vema watu wakafanya yale yanayompendeza Mungu. Kwa kufanya matendo mema utakuwa na uhakika kuwa baada ya maisha ya hapa duniani utakuwa wapi. Mwandishi mwingine anauliza, “Yesu anakuja; utakuwa wapi baada ya kumaliza kipindi chako cha kuishi hapa duniani? Mbinguni au Jehanamu?” Pia waumini wa dini ya Kikristo wanasisitiza juu ya kumtegemea Yesu. Wanasema, “Hakika Yesu ni jibu”; “Mwombe Yesu akuongoze katika matendo”; “Yesu ni mwokozi wa ulimwengu. Mpe Yesu maisha yako nawe utakuwa salama.”

Pia, kuna uhimizaji wa kumwabudu Mungu kwa kusema kuwa “siku za mwisho zinakaribia,” “ni nyakati za rehema.” Waandishi mbalimbali wanasema, “Okokeni, ni nyakati za rehema”; “Heri tu ungeokoka sasa”; “Heri ungeokoka leo ili makosa yasitiriwe mbele za Mungu, kwani saa ya wakovu ni sasa.” Waandishi wanahimiza kila jambo kufanyika kwa wakati wake. Hivyo, wasomaji kama watafuata maelezo hayo yatawasaidia, kwani kama waandishi wa maandishi ya vyooni wanasema kuwa kila jambo na wakati wake, basi hatuna budi tumwombe sana Mungu.

5.2 Kuhusu Maradhi

Katika jamii mbalimbali watu wamekuwa wakiogopa sana kupata ugonjwa wa UKIMWI, ingawa wengi wanajua namna ugonjwa huo unavyoambukizwa bado hawachukui tahadhari, wanaendelea kufanya mapenzi yasiyo salama. Waathirika wengi wa ugonjwa huu wamekuwa wakiona aibu kujitangaza hadharani, kwani wapo watu wanaoona

muathirika wa ugonjwa huu ni mzinzi, hivyo inaonekana ni ugonjwa wa aibu. Katika utafiti wetu tuliona watu wakitoa hisia zao kwa kusema kuwa wameathirika. Mwandishi mmoja anasema, "UKIMWI unanimaliza." Mwandishi huyu anatoa hisia zake sehemu ambayo mtu hatamjua, yawezekana anatarajia mchango wa mawazo kutoka kwa watu ili ajue nini cha kufanya. Ametumia lugha ya kusononesha. Mwandishi mwingine naye ameandika, "Nina ngoma." Lugha aliyoitumia mwandishi wa mwanzo na wa pili ni tofauti, ingawa lengo ni moja kuelezea hisia zao kama wana ugonjwa wa UKIMWI. Mwandishi wa pili anatumia lugha ya mtaani ambayo si lugha rasmi, tofauti na mwandishi wa mwanzo. Kimsingi lugha zote zinafikisha ujumbe wa aina moja.

Mwandishi mwingine anawaasa vijana kwa kusema, "Vijana... mapenzi siyo ngono - AIDS KILL." Mwandishi huyu anaona kuwa vijana wengi wa jinsia tofauti wakiwa katika mahusiano ya urafiki wanadhani kuwa ni lazima wajihusishe na tendo la ngono. Ndiyo maana anawaasa kuwa UKIMWI unaua.

Katika kuendelea kuzungumzia ugonjwa wa UKIMWI mwandishi mwingine anaandika "Msiopiga puli mtapata ngoma." Kupiga puli ni neno lisilo rasmi lenye maana ya kupiga punyeto/kujichua. Hivyo mwandishi huyo ameandika inawezekana akawa anamaanisha kwamba watu wakipiga punyeto hawatakuwa na hamu ya kufanya ngono kwa kuwa punyeto inawaridhisha na hivyo kuepuka UKIMWI.

UKIMWI kama adhabu ni dhamira nyingine inayoibuka katika maandishi ya chooni, dai ambalo tunadhani si la kweli. Hii inajitokeza katika majibizano ambayo tumeyapatia herufi a, b, na c. Maandishi haya yameandikwa na watu tofauti na nyakati tofauti kwa mtindo wa majibizano:

- (a) Kuma tamu
- (b) UKIMWI, je?
- (c) Adhabu yake.

Dhamira hii inaonesha jinsi baadhi ya watu walivyo na mtazamo ambao si sahihi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI, kwamba ni sawa na adhabu. Watu wanapaswa kutambua kwamba ugonjwa wa UKIMWI unaweza kuupata kwa njia mbalimbali, na aliyepata ugonjwa huu siyo kwamba ametenda kosa linalostahili kuadhibiwa kwa njia hiyo.

5.3 Kuhusu Elimu

Elimu ni kitu muhimu katika maisha ya mwanadamu. Katika jamii, elimu hutolewa kwa namna mbalimbali. Kuna elimu inayotolewa katika mfumo maalumu na ile isiyotolewa katika mfumo maalumu, lakini zote lengo lake ni kuelimisha ili mtu aweze kupambana na mazingira yanayomzunguka. Katika utafiti wetu tumepata dhamira zinazozungumzia elimu kama ifuatavyo:

“Urithi wa mtoto ni elimu, siyo majumba.” Mwandishi huyu anasisitiza kwa wazazi au walezi kuwa kitu cha muhimu katika maisha ni kumuelimisha mtoto, na si kumjengea mazingira ambayo yatamfanya ategemea mali za wazazi bila yeye kujishughulisha. Katika jamii tumeona watu wengi ambao wanategemea mali za urithi na kisha wakashindwa kuzisimamia na, hatimaye, mali hizo hupotea. Mwandishi mwingine ameandika. “Elimu siyo kupanda vidato.” Katika msemu huo dhamira hii ya elimu inajitokeza pale ambapo mwandishi anasisitiza kuwa kuelimika si kusoma sana, kwani wapo waliosoma sana na wakafanya mambo ambayo hayaisaidii jamii.


Maandishi mengine yanasema, “Siku Polisi wakielimika, dola lipo matatani.” Polisi ni chombo cha dola ambacho husimamia na kulinda haki na mali za raia na nchi. Mara nyingi polisi hutumia nguvu katika kupambana na raia endapo kunatokea mtafaruku baina ya raia dhidi ya serikali. Wakati mwingine raia huwa wanatetea maslahi ya umma ambapo na polisi mwenyewe ni mmoja kati ya watu wanaotetewa, lakini kwa kuwa polisi ni mtu wa kutekeleza amri, akipewa amri ya kutuliza ghasia, hutekeleza amri hiyo. Kwa mtazamo wa mwandishi anaona kwamba polisi hawajaelimika kwa kuwa hutekeleza amri bila kuhoji. Lakini ukweli ni kwamba shughuli za kijeshi ni za kiimla/kidikteta, na wala si za kidemokrasia. Si kila muktadha katika maisha huhitaji demokrasia.

5.4 Maadili na Utamaduni

TUKI (2006) wanaeleza kuwa maadili ni mwenendo mwema. Katika utafiti wetu tumeona jinsi maadili mema yanavyozungumziwa katika maandishi hayo. Kwa mfano, kuna mwandishi anasema, “Acha kutembea na wake za watu.” Mwandishi huyu anatoa onyo kwa kuhimiza kuacha tabia ya kutembea (kufanya mapenzi) na wake za watu. Katika Kiswahili, kuna msemu usemao kuwa mke wa mtu ni sumu, msemu ambao unamaanisha kwamba ukitaka kufa fanya mapenzi na mke wa mtu, ndiyo maana mke anafananishwa na sumu.

5.5 Matabaka

Matabaka yapo katika jamii zote duniani, ambapo kundi la watu wenye hali moja linatokana na jamii yenye mfumo wa kiuchumi ambao hugawanya watu kufuatana na uwezo wao wa kumiliki na kutawala njia za kuzalisha mali. Kundi hilo lenye nguvu ndilo ambalo mara nyingi hunyonya kundi la wasionacho katika sekta mbalimbali (Shivji, 2006, 2009). Hali hii



Akiandika kuhusu uhusiano baina ya maarifa, ukweli wa maisha na matendo au uzoefu, Madumulla (1993, uk.142) anasema:

Katika nadharia ya falsafa ya ufahamu sheria ya msingi ya ukweli iko katika matendo. Matendo (au uzoefu) ni msingi na lengo la ufahamu (maarifa), na ni kigezo cha ukweli.

Kutokana na dondoo hilo hapo juu, falsafa ya ukweli, ufahamu na uzoefu wa mwanadamu yanafungamana na kwamba, yote kwa pamoja, yanatusaidia pia kuhusianisha na nafasi ya sanaa katika jamii. Katika utafiti wetu kuna mfano mmoja unaohusu jambo hili. Mfano huo tunaupata katika msemo usemao kuwa, “elimu si kupanda vidato.” Kutokana na msemo huu, tunapata mawazo kuwa jamii na kundi la watu waliofanyiwa utafiti linaamini kuwa maana halisi ya elimu si kuwa na vyeti vingi, bali elimu sahihi itapimwa kutokana na matendo ya mhusika. Kwa mantiki hiyo basi, elimu au maarifa sahihi yanategemea kiwango cha utendaji kazi alichofikia mtu. Baadhi ya watu wanaweza kuwa ama hawajasoma elimu ya namna yoyote au wamesoma, lakini wana kiwango kidogo cha elimu, ijapokuwa watu hao ni watendaji wazuri na watekelezaji bora wa majukumu yao kuliko hata wale ambao wanahesabika kuwa ni wasomi na wataalamu wa fani mbalimbali.

Kwa hivyo basi, kutokana na matokeo ya utafiti huu ni dhahiri kuwa matendo na uzoefu wa mwanadamu ni lengo na kigezo cha maarifa. Ubora na udhaifu wa elimu aliyo nayo mtu unatarajiwa kupimwa kutegemea kiwango cha ufanisi katika suala la kuwajibika.

6.3 Ubunifu, Maadili na Utamaduni

Utamaduni ni jumla ya mambo yote yanayobuniwa na jamii ili kukidhi utashi na maendeleo yake. Kwa maneno mengine, utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao wa mambo, na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha wao na jamii nyingine. Katika utamaduni kuna vitu kama vile lugha, mila na desturi hata maadili. Kimsingi, dhana za ubunifu, maadili na utamaduni zinahusiana kwa kiwango kikubwa. Katika utafiti wetu, kuna mambo kadhaa ambayo yanaashiria kuwa sanaa ya kuandika katika vyoo ni sehemu ya ubunifu wa wanajamii katika jamii ya Watanzania na jamii nyinginezo. Aidha, katika ubunifu huu suala la kimaadili linalojitokeza kwa sura tofauti tofauti. Sura ya kwanza ni mchakato mzima wa kuandika chooni, na sura ya pili ni matumizi ya lugha safihi.

Katika utafiti wetu, tulibaini kuwa idadi kubwa ya maandishi katika maeneo ya chooni ilitumia lugha safihi. Katika jamii ya wanadamu si kawaida kuona watu wanatumia lugha ya namna hiyo. Lakini katika maandishi tuliyochunguza, jambo hili lilikuwa la kawaida sana. Miongoni mwa misemo hiyo inayodokeza na kutumia lugha ya matusi ni pamoja na “okokeni kuma nyoko nyie,” “kufirwa ni bomba,” “napenda kufira,” na kadhhalika. Kutokana na hali hii tunaweza kuhitimisha kwa kutoa dondoo chache.

Kwanza, kwa kuwa si kawaida kutumia lugha safihi, wanajamii hutumia fursa yao pindi wawapo katika maeneo ya chooni kueleza hisia zao. Kwa hiyo, katika Fasihi, kuna fursa ambayo inampa mwanadamu uhuru wa kunena na kutenda zaidi ya yale ambayo hayatarajiwi kutokea. Matakwa na utashi wa mwanadamu hujidhihirisha zaidi katika sanaa, hususani

Fasihi, kuliko katika tasnia nyingine yoyote. Hivyo, maandishi haya yanaonesha asili ya 'unyama' au uhayawani iliyojificha kwa mwanadamu. Mwanadamu huyu afanyapo uhayawahi huo ndipo roho/nafsi yake huridhika.

Pili, kutokana na matokeo ya utafiti huu, sehemu mojawapo na mahali pa kuweza kumfahamu mwanadamu kwa usahihi ni faraghani. Hii ni sehemu ambayo mwanadamu yuko peke yake, haathiriwi na mihemko wala matakwa ya jamii. Hivyo, huwa ameitoroka mihemko na kupata muda wa 'kiasi' wa kupambana na mihemko hiyo kwa kificho, akichelea kuwa akijitokeza katika uwazi atadhibitiwa. Aidha, ana kuwa hayuko katika upweke, kwa sababu anajua anapoandika haandikii ombwe, bali jamii. Na anajua kama hatajibiwa, wamesikia, 'wataipata.'

7.0 Hitimisho

Katika makala haya tumewasilisha na kujadili matokeo ya utafiti kuhusu dhamira ya maandishi ya vyooni na nafasi yake katika jamii. Kutokana na matokeo tuliyojadili, imebainika kuwa ubunifu unaojitokeza katika maandishi maeneo ya vyooni umefumbata mbinu maridhawa za kisanaa. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa katika maandishi tuliyoyatafiti kuna dhamira mbalimbali na ambazo zinahusiana na mambo yaliyopo katika jamii. Dhamira zilizojadiliwa zilikuwa ni maradhi, maarifa, maadili, matabaka, umuhimu wa lugha yako, mapenzi na suala la dini. Pia nafasi ya dhamira hizo katika jamii imejadiliwa.

Marejeo

- Adedeji, A. (1993). *Africa within the World: Beyond Dispossession and Dependence*. London: Zed books.
- Babbie, E (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Crewswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.
- Enkvist, N. E. (1973). *Linguistic stylistics*, Mouton: The Hague & Paris.
- Fischer, K. (2009). *Latrine Literature*. <http://www.dw.com/en/german-student-gets-degree-in-latrine-literature/a-4540624>, Jumanne, 01-03-2011.
- Isaac and Michael, (1981). *Handbook of research and evolution: A collection of principles, methods and strategies useful in the planning, design and behavioural science*, San. Diago: Edips.
- Kothari, C. R. (1992). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Limited.
- Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.
- Madumulla, J. S. (1993). *Mwandishi wa Riwaya ya Kiswahili na Suala la Ukweli wa Maisha: Fasihi, Uandishi na Uchapishaji*, Dar es Salaam: DUP.
- Mahenge, E. (2009). "Uchambuzi wa Fani na Maudhui katika Semi zilizokwenye tiketi za Daladala: Dar es Salaam" Kioo cha Lugha, Juzuu 7, Dar es salaam, TATAKI.
- Miall, D. S., & Kuiken, D. (1994). *Poetics*, University of Alberta.
- Mkandawire, T (1995). "Beyond Crisis: Towards Democratic Development State in Africa", Dakar: CODESRIA Eighth General Assembly.

- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*, Dar es Salaam, DUP.
- Mutembei, A. K. (2005). Beyond the Similaritude of AIDS to the Miscellany of its culture A Comparison of Figurative Language on AIDS Billboards across Africa” (Hajachapishwa).
- Shivji, I. G. (2006). Let the People Speak: Tanzania down the road to neo-liberalism, Dakar: CODESRIA.
- Shivji, I. G. (2009). Accumulation in an African Periphery: A Theoretical Framework. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.
- Tempels, P. (1954). *Bantu Philosophy*, Paris. Presence Africaine.
- TUKI. (2006). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Nairobi. O.U.P.
- Uislamu.org (2011). Utangulizi wa Dini na Uislamu, <http://www.uislamu.org/utangulizi.htm> Jumatano, 09-06-2011.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*, FPL, Nairobi